

# Karibu MAREKANI

**Kitabu cha Mwongozo kwa Wakimbizi**
*Swahili Version*

CAL
COR Cultural Orientation Resource Center

# Karibu MAREKANI

**Kitabu cha Mwongozo kwa Wakimbizi**

**Toleo la Nne**

**2014**

**Kimetayarishwa na Cultural Orientation Resource Center**

**Center for Applied Linguistics**

**Washington, DC**

Yaliyo katika kitabu hiki ilikuzwa na mchango kutoka Bureau of Population, Refugees and Migration, United States Department of State, lakini si lazima kuwakilisha sera ya shirika hayo, na watumiaji hawapaswi kudhani ina madaraka kutokea serikali ya shirikisho.

***Yanayo patikana katika toleo hili la Karibu Marekani: Kitabu mwongozo kwa wakimbizi inatowa msingi kwenye taarifa zilizotolewa kwa Center for Applied Linguistics na wawakilishi kutoka mashirika yafuatayo:***

- Church World Service
- Department of Health and Human Services, Administration for Children and Families, Office of Refugee Resettlement
- Department of State, Bureau of Population, Refugees, and Migration
- Episcopal Migration Ministries
- Ethiopian Community Development Council
- Hebrew Immigrant Aid Society
- International Catholic Migration Commission
- International Organization for Migration
- International Rescue Committee
- Lutheran Immigration and Refugee Service
- U.S. Committee for Refugees and Immigrants
- United States Conference of Catholic Bishops
- World Relief

***Waliyo changiya picha:***

- Center for Applied Linguistics
- Jibril Mohamed Hirsi
- Lutheran Social Services of Fargo, North Dakota
- Mike Stanley, Mike Stanley Productions
- Resettlement Support Center Africa (Church World Service)
- Resettlement Support Center East Asia (International Rescue Committee)
- Resettlement Support Center South Asia (International Organization for Migration)
- Resettlement Support Center Turkey and the Middle East (International Catholic Migration Commission)
- Sichan Siv
- Tri-Cities World Relief Office, Richland, WA
- Youth Co-Op, Inc.
- Zohra Daoud

***Tunawashukuru wale wote ambao wamechangia kwa toleo hili. Tunashukuru hasa Vituo vya misaada vya makazi mapya na wanachama wa Kundi la Mwelekezo wa Utamaduni.***

Meneja wa Mradi: Michal Panner
Mhariri: Donald A. Ranard
Jadala: Uchoraji na Ahmad AlKarkhi
Jadala na Usanii wa ndani & toleo: SW Creatives

Majina zilizo tumiwa katika sehemu za shuguli za chapisho hili ni za uwongo. Ufananishi wowote wa watu wa kweli ni mapatano tu.

# KARIBU KWA MAELEZO YA UTAMADUNI!

Kitabu cha mwongozo hiki *Karibu Marekani* kita kusaidia kujitayarisha kwa miezi michache za kwanza nchini Marekani. Kinakueleza kuhusu mambo ya kuyataraji wakati wa kutafuta mahali pa kuishi, kutafuta kazi, kukutana na Wamarekani, na kujirekebisha kwa utamaduni na jamii ya Marekani.

# Yaliyomo


**SURA YA KWANZA:** Safari ya Makazi Mapya 6

**SURA YA PILI:** Marekani na Utamaduni wa Marekani 14

**SURA YA TATU:** Kusafiri Marekani 26

**SURA YA NNE:** Shirika la Makazi Mapya 44

**SURA YA TANO:** Nyumba 56

**SURA YA SITA:** Huduma za Jamii 68

**SURA YA SABA:** Usafiri 80

**SURA YA NANE:** Huduma za Afya 90

**SURA YA KENDA:** Matumizi ya Fedha 108

**SURA YA KUMI:** Kujirekebisha Utamaduni na Kubadilisha Wajibu 126

**SURA YA KUMI NA MOJA:** Haki na Majukumu chini ya Sheria nchini Marekani 144

**SURA YA KUMI NA MBILI:** Kazi 160

**SURA YA KUMI NA TATU:** Kujifunza Kiingereza 182

**SURA YA KUMI NA NNE:** Elimu 196

**SURA YA KUMI NA TANO:** Safari Inayoendelea 212

**VIAMBATISHO** 220

A. MAJIBU 220

B. KAMUSI YA MANENO YA KAWAIDA YA MAKAZI MAPYA 223

C. NYUSO ZA HISIA 226




1

# Sura ya Kwanza
## SAFARI YA MAKAZI MAPYA

Kama wakimbizi wengine wengi, umeamua kupata makazi mapya na kuanza maisha mapya katika Marekani. Makazi mapya ni hatuwa ya kwanza ya kuwa makazi wa kudumu na, kwa wengi, raia wa Marekani siku moja. Makazi mapya ni mchakato wa muda mrefu ambayo inabadilisha maisha yako, na inaleta changamoto nyingi na fursa. Uzoefu ni tofauti kwa kila mtu. Ni kawaida kusikiya msisimuko na mwenyi wasiwasi unapojiandaa kwa safari yako.

---

### Sura Hii Itajadili

» Jukumu la wafanyakazi wa makazi mapya kama mwongozo wako wa kwanza
» Kujitegemeya kama muhimu kwa mafanyikio yako

**Makazi mapya ni mchakato wa muda mrefu na changamoto nyingi na fursa njiani. Katika kipindi cha miezi yako chache ya kwanza Marekani, wafanyakazi wa makazi mapya watakuwa viongozi wako wa msingi.**

## MANENO MUHIMU YA KIINGEREZA

Maneno ya Kiingereza yafuatayo hutumiwa wakati wa kuzungumza kuhusu makazi mapya nchini Marekani. Maneno haya itakuwa na mafaa kwako kuyajifunza.

***Sema neno katika kiingereza. Andika neno katika lugha yako ya asili. Kisha chapa picha ya neno, andika maana yake, au uitimiye katika msemo. La kwanza limefanyika kwa ajili yako.***

| Katika Lugha yako | Katika Kiingereza | Chapa picha ya neno, andika maana yake, au uitumiye katika msemo. |
|---|---|---|
| ujasiri | courage | *Ujasiri ndiyo kusema kuwa jasiri na kubaki bila woga ya hofu na hatari.* |
| | determination | |
| | goals | |
| | independent | |
| | journey | |
| | resettlement | |
| | self-reliance | |

**Wafanyakazi wa makazi mapya watakuwa viongozi wako wakuu, kwa hivyo changiya maswali na wasiwasi zako pamoja nao.**

## MATAKWA NA WASIWASI

*Katika visanduku hapa chini, chora au andika kuhusu matakwa yako na wasiwasi kwa ajili ya baadaye.*

| | |
|---|---|
| UNAYOTAKA | WASIWASI |
| UNAYOTAKA | WASIWASI |

*Umekwisha kusikiya nini kuhusu maisha Marekani? Chapa au andika kuhusu mambo uliyo ya sikiya hapa chini. Unapomaliza na kitabu hiki, rudi kwa ukarasa huu. Tiya katika duara nini bado ni kweli na uweke msalaba kwa hiyo ambayo bado si kweli.*

Maisha nchini Marekani haitakuwa rahisi, hasa kwa mwanzo, lakini kutakuwa watu ambao watakusaidiya kwa kuanza. Katika kipindi chako cha miezi yako chache ya kwanza nchini Marekani, wafanyakazi wa makazi mapya watakuwa viongozi wako wa msingi. Watatumika na wewe kwa kukuunganisha na huduma, kama vile huduma za ajira na madarasa ya kiingereza. Wanaujuzi na azoefu wa kukusaidiya, kwa hivyo changiya maswali na wasiwasi zako pamoja nao.





***Maisha itakuwa vigumu wakati mwingine, lakini jaribu kuwa na tumaini na kumbuka kwamba mabo yatakuwa mazuri!***

Utacheza sehemu kubwa katika makazi yako mapya yako mwenyewe. Zaidi ya wakimbizi milioni tatu kabla yako, walijenga upya maisha yao na kuleta mchango yao katika jamii nchini Marekani, wewe piya utafanya hivyo! Hapa unamifano michache ya baadhi ya Wamarekani wenyi mafanikio ambao walianza maisha yao nchini Marekani kama wakimbizi:



*Madeleine Albright: Waziri wa mambo ya nje wa Marekani, kutoka Jamhuri ya Czech Republic (Czechoslovakia ya zamani)*



*Zohra Daoud mmoja wa wanzilishi wa chama cha kusaidia wanawake wa Afghanistani katika Marekani, kutoka Afghanistan*



*Albert Einstein: Tuzo ya Nobel, Kutoka Ujerumani*




*Gloria Estefan: Mwimbaji maarufu, Kutoka Cuba*



*Jibril Mohamed Hirsi: Mkurugenzi wa shirika lisilo na faida kwa kusaidiya wa Marekani wapya, kutoka Somalia*



*Wyclef Jean: Msanii maalum na mwimbaji, kutoka Haiti*



*Sichan Siv: Balozi wa Marekani, kutoka Cambodia*

---

Kumar aliomba shauri kutoka kwa meneja wa kesi yake na mtaalamu wa ajira katika shirika lake la makazi mapya, na alijifunza jinsi ya kutafuta kazi kwa ajili yake mwenyewe. Krishna alibaki nyumbani au katika ofisi ya makazi mapya na kusubiri wafanyakazi wapate kazi kwa ajili yake. Ni nani unadhani pengine alipata kazi wa kwanza? Ni nani unadhani alikuwa na mafanikio zaidi baada ya muda?

---

Hutakiwe ujulikane vizuri ili upate mafanyikio Marekani. Wakimbizi wengi wanafanikiwa kila siku tu kwa kufanya kazi kwa bidii kufikia malengo maalum, kama vile kukinga jamaa zao salama na afya, kutafuta kazi iliwajitegemee, kujifunza Kiingereza, na kusaidia watoto wao na jamii. Na vipaji vyako, maarifa, ujasiri, na uamuzi, unaweza kufanikiwa pia.



Wakati Naw Paw alifika Marekani mara ya kwanza pamoja na watoto wake watatu, kazi yake ya kwanza ilikuwa kusafisha ofisi, ingawa yeye alikuwa na kazi kama katibu katika nchi yake. Hakuipenda kazi yake, lakini alifanya hivyo kwa sababu alipashwa kusaidia jamaa lake. Ingawa alijua baadhi ya Kiingereza, hakuweza kuwasiliana vizuri sana katika kiingereza. Leo hii, miaka 6 baadaye, anafanya kazi kama mpokea wageni katika ofisi alikuwa akisafisha kwa miaka mingi, na anasoma sasa ili awe katibu. Yeye anatumaini kuwa maneja wa ofisi siku moja. Je, nini Naw Paw alifanya ili apate na mafanikio?

## MALENGO YAKO

***Sasa ni wakati nzuri kwa kufikiri kuhusu malengo yako mwenyewe. Fikiria mahali ambapo umefikia na ambapo unakwenda. Chora picha katika vipande hivi hapa chini kwa kueleza safari yako.***

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Wewe ni nani?** | **Ulipokuwa mtoto ulifanya nini nchini mwako?** | **Ulifanya nini kama mtu mkubwa nchini mwako?** | **Ulifanya nini katika nchini yako ya ukimbizi?** |
| **Nini unataka kufikia katika mwezi yako ya kwanza ya makazi mapya?** | **Nini unataka kufikia katika mwaka yako ya kwanza ya makazi mapya?** | **Nini unataka kufikia miaka 5 baada ya makazi mapya?** | **Nini unataka kufikia miaka 10 baada ya makazi mapya?** |

## KAMILISHA*

***Kweli au uongo? Ni kwa kiasi gani unafikiri kujua kuhusu makazi mapya nchini Marekani? Pima maarifa yako na kauli chini. Soma kauli hizi na zungusha neno* Kweli *kama unadhani taarifa ni haki na zungusha* Uongo *kama unadhani taarifa si sahihi.***

1. Utakuwa na nafasi muhimu katika mafanikio yako katika makazi mapya yako. **Kweli** **Uongo**
2. Kuna watu kutoka duniani kote wanaoishi Marekani. **Kweli** **Uongo**
3. Jamii zote nchini Marekani zinafanana sana. **Kweli** **Uongo**
4. Unahitaji kufanya kazi na shirika lako la makazi mapya kwa urahisi wa marekebisho yako Marekani. **Kweli** **Uongo**
5. Kutakuwa na huduma za umma na msaada wa serikali kwa ajili yako katika jamii yako. **Kweli** **Uongo**
6. Unahitaji kununua gari baada ya kuwasili Marekani, hivyo unaweza kutembea katika jamii yako mpya. **Kweli** **Uongo**
7. Watu wazima wengi, wanaume na wanawake, wanapashwa kufanya kazi nchini Marekani. **Kweli** **Uongo**
8. Hauta hitaji kujifunza kiingereza. **Kweli** **Uongo**
9. Shule la umma ni bure na linalazimishwa na sheria kwa watoto wote wenye umri 6-16. **Kweli** **Uongo**
10. Madaktari hawawezi kuzungumza kuhusu afya yako na mtu yeyote bila ruhusa yako lakini wewe tu. **Kweli** **Uongo**

---

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 220.

11. Watu wote Marekani, hata wakiwa wakimbizi, wana haki za msingi za binadamu. **Kweli** **Uongo**

12. Unahitaji kuacha baadhi ya utamaduni wako na maadili na kukabiliana na utamaduni na maadili za Marekani. **Kweli** **Uongo**

Ni sawa kama haukujua majibu yote sahihi. Kitabu hiki kitakagua ukweli muhimu wa makazi mapya na kusaidia kujiandaa kwa ajili ya nini cha kutarajia wakati unaoishi Marekani.




2

# Sura ya Pili
## MAREKANI NA UTAMADUNI WA MAREKANI

Marekani ni nchi ya tatu kwa ukubwa na idadi ya watu duniani. Ni nchi ya mikoa na hali za hewa mbalimbali, na inaundwa na watu, makabila, rangi, dini, na lugha asili tofauti. Hata hivyo ni taifa moja: taifa ya Wamarekani. Hata ingawa Wamarekani wanakuja kutoka duniani kote, kuna baadhi ya imani za msingi na njia ya kufanya mambo ambazo Wamarekani wengi wanashiriki. Imani na tabia hizi zinaweza kuwa tofauti na hizo ambazo unatumia.

### Sura Hii Itajadili

» Tofauti kati ya jamii
» Utamaduni na Maadili za Marekani



## MANENO MUHIMU YA KIINGEREZA

Maneno ya Kiingereza yafuatayo hutumiwa wakati wa kuzungumza kuhusu Marekani na utamaduni wa Marekani. Maneno haya itakuwa na mafaa kwako kuyajifunza.

***Sema neno katika kiingereza. Andika neno katika lugha yako ya asili. Kisha chapa picha ya neno, andika maana yake, au uitimiye katika msemo. La kwanza limefanyika kwa ajili yako.***

| Katika Lugha yako | Katika Kiingereza | Chapa picha ya neno, andika maana yake, au uitumiye katika msemo. |
|---|---|---|
| utamaduni | culture | *Jamaa la Yahya inajivunia utamaduni wao wa Darfur na inahamu ya kujifunza kuhusu utamaduni wa Marekani.* |
| | community | |
| | customs | |
| | diversity | |
| | identification | |
| | language | |
| | newcomers | |
| | population | |
| | tradition | |

**Kila jamii Marekani ni tofauti. Yale uliyasikiya kuhusu Marekani kutoka watu wengeni inaweza kuwa uongo kwako wewe.**



## TOFAUTI KATI YA MAJAMII

Nchini Marekani, jamii zinatofauti katika njia nyingi. Mchanganyiko wa makundi ya rangi na kikabila. Sheria za mitaa pia zinatofautiana kutoka jamii kwa jamii. Na kila jamii ina njia yake mwenyewe yaku shurulikiya wageni. Kwa sababu hii, uliyosikiya kuhusu Marekani, hata kutoka kwa jamaa na marafiki tayari katika Marekani, inaweza kuwa siyo kweli kwako. Shirika lako la makazi mapya itakusaidia kujifunza kuhusu jamii yako mpya na kuelewa nini utarajie.

---


Wakati binamu wa Dina na jamaa lake waliihamishwa Marekani miaka 3 iliyopita, waliishi katika nyumba kumbwa. Dina hakufurahi wakati alipewa chumba katika fleti ya vyumba tatu pamoja na wanawake wengini wawili wenyi umri yake. Alidhani anapashwa kuishi katika nyumba kubwa kama binamu yake. Kwa sababu gani nyumba ya Dina ilikuwa tofauti na nyumba ya binamu yake? Yeye angeli paswa kutambua nini?

---



CAL COR Cultural Orientation Resource Center

## RAMANI YA MAREKANI




***Fikiria kuhusu utamaduni yako mwenyewe au usuli.***

- ❒ Unazungumza lugha gani?
- ❒ Unakula chakula gani?
- ❒ Nyumba yako iko namna gani?
- ❒ Desturi na mila yako muhimu ni gani?

***Chapa au andika hapa chini kuhusu utamaduni, usuli, kama vile mila, desturi au vyakula.***

**Wamerikani wengi wanathamini kujitegemea na kufanya kazi sana na wanaheshimu watu wanaouliza maswali.**

**Wamerikani wana cheka wanapo salimu marariki na hata wageni.**

*Watu wengine unaowakuta Marekani wanaweza kuwa na niya ya kujifunza zaidi kuhusu utamaduni na usuli wako. Fanya mazoezi kwa kumwambiya mwenzako kuhusu yale uliyo chapa au uliandika katika ukarasa wa mbele.*

## KUHUSU MAREKANI NA UTAMADUNI WA MAREKANI

Hakuna utamaduni moja wa Marekani. Marekani ni nchi ya wetu kutoka nchi nyingine ambao walileta pamoja nao mila nyingi za kitamaduni na desturii tofauti. Hata hivyo, kuna tabiya mbalimbali za kawaida zinazo kubaliwa na zaidi ya Wamarekani. Haya yanaweza kuwa tofauti na hizo za utamaduni na nchi yako. Utafanikiwa zaidi Marekani kama unaangalia nini inaendelea pembeni yako na ujifunguwe kwa njia mpya za kufanya vitu, na kama ukotayari kuuliza ma swali kuhusu tabia hizo usiyozielewa.

Hapa chini kuna vitu vyakujuwa kuhusu maadili, mienendo na tabia za Marekani:



**KUJITEGEMEYA.** Wamerikani wengi wanathamini kujitegemea na kufanya kazi kwa bidii. Wanatarajia ya kuwa wageni wapate kazi haraka iwezekanavyo ili wajitunze wenyewe na pia jamaa zao. Pia, wanatarajia wageni wasiozungumuza kiingereza wakijifuze haraka kama vile wataweza.



**KUULIZA MASWALI.** Wamarekani wanaheshimu watu wanaouliza maswali. Wanaamini kwamba kuuliza kunaonesha kwamba unajaribu kujifunza na kuelewa. Wakati hujuwi kufanya kitu, usiogope kuuliza. Wamarekani wengi watafurahi kukusaidia.

Bikash alikuwa wakujitoleya kwenyi makumbusho ya jamii.Katika makumbusho, alikutana na mfanyakazi mwengine wakujitolea, Mwanamke Mmarekani mzee. Alikuwa mfurahivu sana na alitaka kujifunza yote kuhusu Bikash na utamaduni wake. Lakini maswali zingine mwanamke aliuliza zilionekana kuwa binafsi sana ngambo ya Bikash. Unafikiri Bikash alisikiya namna gani? Ungelikuwa Bikash, ungelifanya nini?

***Pamoja na mtu mwengine, fanya mazoezi kuulizana maswali kuhusu mwengine. Hapa kuna maswali fulani unaweza kuuliza:***

- ❒ Unatoka wapi?
- ❒ Umeishi hapa tangu wakati gani?
- ❒ Unaishi pamoja na nani?
- ❒ Una watoto?

***Nini ingine unaweza kutaka kujuwa kuhusu mwenzako? Tunga maswali zako mwenyeye zakuuliza!***

Hapa kuna maadili, forodha na tabia mengine ya kawaida Marekani:



**YASIO RASMI**. Wamarekani ni watu mara nyingi rasmi kuliko watu wa nchi zingine. Katika hali ya kijamii, wana tumiya majina za kwanza. Katika hali ya biashara, wanatumiya majina za jamaa na vyeo (mheshimiwa, Bi, au Dr. hutuimiwa kabla rasmi kuanzishwa, lakini wakubwa wa kazi na wenzako wa kazi wengi wanaweza kupendeleya kutumia majina za kwanza.

Nchini mwake, Maug Thein alikuwa kiongozi katika jamii yake. Katika jamii yake mpya Marekani, meneja wa kesi yake, mwanamke wa miaka michache kuliko Maug Thein, anamwita Maug Thein kwa jina lake la kwanza, anamuangalia machoni, na kwa namna nyingine anamkamata Maug Thein kama mwenzake. Ungelikuwa Maug Thein, ungeli sikiya namna gani? Ungeli fanya nini?



**SALAMU:** Wamarekani wanacheka sana, na wanatumiya cheko wanapo wasalimu marafiki na hata wageni. Pia, wanaume na wanawake wana peana mikono kwa ku kujitambulisha, ao wanapotambulishwa kwa mtu mwengine.

**Kuwa kwa wakati ni muhimu sana kwa Wamarekani, na unaweza kupoteza kazi yako kama unachelewa kila mara.**

**Uchukuwe pamoja nawe aina fulani ya kitambulisho kila mara unatoka nyumbani kwako. Kama hauzungumze kiingereza, beba nambari ya simu yako na anwani yako.**



**KUHESHIMU WAKATI.** Wamarekani wanaamini kwamba kuwa kwa wakati ni muhimu kabisa. Wamarekani wanajaribu kuwa kwa wakati na wanategemea wengine wawe kwa wakati, pia. Kukuwa na kuheshimu miadi ni muhimu. Kama hauwezi kuchunga miadi kabla yakutembelea mtu kwa ofisi, huyo mtu anaweza kuwa hana uwezo wakukutana nawe au utachelewa zaidi ya dakika 15, lazima uite, nakufasiriya yakuwa utachelewa, na uombe msamaha. Pia, kuwa kwa wakati kazini kilasiku ni muhimu sana, na unaweza kupoteza kazi yako kama unachelewa kila mara.



**FARAGHA.** Wamerikani wanaweka thamani ya juu kwa siri ya binafsi. Watu hawatembeleye wengine nyumbvani kwao kabla ya kuita kwanza au kualikwa. Mambo ya kifedha inachukuliwa binafsi, na wamarekani wanafikiri yakuwa si adabu kuuliza mshahara ya mtu au hata ngapi alilipa kwa nyumba ama kwa gari. Wamarekani wanafikiri piya yakuwa si adabu ku muuliza mtu usiye mjuwa kabisa maswali kuhusu fedha, umri ao maisha binafsi.

---

Anna alifurahiwa na kufanya urafiki na majirani njiyani. Alipiga kengele malangoni mwao jioni moja, njiani akirudi nyumbani kwa kuwatembeleya, na alishangaa na aliumizwa wakati walimwambia yakuwa hii haikukuwa wakati nzuri ya kutembeleyana kwa sababu walikuwa wakila chakula cha jioni. Je, majirani wa Anna hawataki kuwa rafiki yake tena? Kama ungelikuwa anna, ungeli fanya nini?

---



**BAHASHISHI.** Kwa kawaida Wamarekani wanapana bahashishi ya 15% mpaka 20% ya mswada kwa mtumishi katika mkahawa, dereva wa teksi, ao mtengeneza nywele. Kama mtu anakusaidiya na mzigo yako, $1 inatarajiwa. Hupaswi kumpa fedha kwa polisi ao mfanyakazi yeyote wa serkali  kwa sababu inaweza kukamatwa sawa rushwa.



**KUNYWA POMBE NA KUVUTA SIGARA.** Kuna sheria nyingi kuhusu matumizi na uuzaji wa pombe nchini Marekani. Uamuzi wa kunywa pombe ni uchaguzi binafsi, na kamwe kukosa heshima kukataa kinywaji nchini Marekani. Kuendesha gari ukiwa chini ya ushawishi wa pombe ni kinyume cha sheria. Huwezi kuvuta sigara katika majengo na katika maeneo mbalimbali mengi ya umma (kama vile migahawa), na katika miji mbalimbali huwezi kuvuta sigara karibu na ujengo. Wamarekani wengi hawavuti sigara, na wanatarajia wengine wasivute nyumbani mwao. (Angalia sura ya 11 kwa habari zaidi kuhusu ma sheria za Marekani.)

---

Moe Aung, akiwa na umri wa myaka 19, alialikwa nyumbani kwa Smith kwa chakula cha jioni. Alipokuwa hapo, Moe Aung alitolewa glasi ya mvinyo na chakula cha jioni. Moe Aung hakujuwa afanye nini. Je, atavunja sheria kama anakubali hiyo kinywanji? Je, Moe Aung anapaswa kukubali mvinyo?

---



**KUKAA SALAMA**. Popote unapoishi, ni lazima uchukue hatua ya msingi ya kukaa salama, kama vile kufunga nyumba yako na gari yako, usijaribu kuchukuwa kiasi cha fedha nyingi nawe, na kujua mitaa gani inabidi uepuke wakati wa usiku.




**KUBEBA KITAMBULISHO**. Wamarekani wanatumiya vitambulisho mbalimbali katika shiguli zao na serikali na biashara. Unapaswa kubeba daima picha ya kadi yako ya I-94 na kadi yako ya EAD, vilevile, jina, anuani, na nambari ya simu ya shirika la makazi mapya. Kama hauzungumzi kiingereza, chukuwa nambari ya simu yako na anuani yako, ao anuani na nambari ya simu ya mtu ambaye unamtembeleya. Usipeleke kadi yako ya ruzuku ya serikani. Uiweke mahali salama katika nyumba yako.



**KUFWATA SHERIA**. Wamarekani wanaamini kwamba ni muhimu kufuata sheria. Hii ni pamoja na kusubiri katika mistari njiani na kusimama mbele ya alama ya kusimama wakati mtu anaendesha gari.



***Zungusha maadili, mitazamo, au tabia yaliotajwa kwenye ukarasa 18, 19, 20 na 21 ambayo ni tofauti na uzoefu wako uliopita.***

***Fikiria kuhusu maadili gani yaliozungumzwa katika ukarasa wa 18 mpaka ukarasa 21 ambayo inawezakuwa ngumu zaidi kwako ili ujirekebishe. Kamilisha chati hili hapa chini. Hii ni mfano kwako.***

| **Maadili gani, mila na tabia gani zinaweza kuwa ngumu kwako kuzoea Marekani?** | **Jinsi gani utajaribu kujisaidiya mwenyewe kuzoea mabadiliko haya?** |
|---|---|
| *Nita tarajia kupeana mikono na wanaume na wanawake wakati nitakutana nao.* | *Nitawasalimu watu na cheko, na nitawaambiya jina langu na wapi ninatoka.* |

Maryam alijaribu kuzoea desturi mpya na maadili zote nchini Marekani. Alijaribu kujitegemea, kufika mahali kwa wakati, hata mbele ya wakati, na kuheshimu faragha za majirani yake. Lakini, kila siku alijisikiya vibaya na alikumbuka kwao sana. Unafikiri ni kwa sababu gani Maryam hafurahi? Ungekuwa Myriam, ungefanya nini?

***Zungumza na mwenzako kuhusu njia za kuepuka kusikia unazidiwa nchini Marekani.***

## KAMILISHA*

***Chagua majibu bora zaidi kwa maswali hapa chini ukifanya chaguo bora.***
***Hii ni mfano:***

*Lugha gani ndio inazungumzwa na watu wengi zaidi Marekani?*

a. Kichina.

(b.) Kiingereza.

c. Kijerumani

***Watu wengi Marekani wanazungumza Kiingereza. Kwa hiyo, Jibu ni b. Kiingereza.***

1. Je, jamii zote ziko sawa nchini Marekani?

   a. Ndiyo.

   b. Hapana.

2. Nikwa njia gani zifuatazo Wamarekani hutumiya kwa kawaida kwakusalimiya wageni?

   a. Kwa kukumbatiyana.

   b. Kwa cheko.

   c. Kwa kushikana mkono.

   d. Kwa kubusu kwenye shavu.

   e. Chaguo b na c.

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 220.

3. Ni gani ifatao Wamarekani wana thamani zaidi?
   a. Kujitegemea.
   b. Kuuliza maswali.
   c. Kusema kwa sauti kubwa.
   d. Kuheshimu wakati.
   e. Uchaguzi a, b, na d.
4. Nani kati ya watu hawa katika mifano hizi hakujitegemeya?
   a. Mtu ambaye ameanza kujifunza kiingereza mara moja.
   b. Mtu ambaye anawauliza marafiki na jamaa zake kama kuna kazi yoyote katika eneo.
   c. Mtu ambaye hana nia ya kutafuta kazi na anajisikia kuwa shirika la makazi mapya linapaswa kumutolea kila kitu.
   d. Mtu ambaye anajaribu kujifunza kuhusu maisha katika Marekani kwa kuchunguza na kuuliza maswali.
5. Fikiria kwamba majirani zako Mmarekani wanakualika nyumbani kwao na watakupa pombe. Hii ni tatizo kwako kwasababu wewe hunywi pombe. Je, ni kukosa adabu kukataa kunywa nchini Marekani?
   a. Ndiyo.
   b. Hapana.



3

# Sura ya Tatu
## KUSAFIRI MAREKANI

Baada ya kuitikiwa kuingiya Marekani, kuna hatua chache zaidi za kukamata kabla ya usafiri. Katika hatua hizi kuna uchunguzi wa kiafya na ukaguzi wa usalama. Tumiya wakati hii ya kungoja kwa kuanza kujifunza kiingereza kama inawezekana.

### Sura Hii Itajadili

» Uchunguzi wa kiafya na Ukaguzi wa usalama
» Shirika lako la makazi mapya
» Mipango za safari
» Maelezo kuhusu safari yako Marekani

**Kabla ya kusafiri Marekani, utahitaji uchunguzi wa kiafya na ukaguzi wa usalama.**



## MANENO MUHIMU YA KIINGEREZA

Maneno ya Kiingereza yafuatayo hutumiwa wakati wa kuzungumza kuhusu makazi mapya nchini Marekani. Maneno haya itakuwa na mafaa kwako kuyajifunza.

***Sema neno katika kiingereza. Andika neno katika lugha yako ya asili. Kisha chapa picha ya neno, andika maana yake, au uitumiye katika msemo. La kwanza limefanyika kwa ajili yako.***

| Katika Lugha yako | Katika Kiingereza | Chapa picha ya neno, andika maana yayo, au uitumiye katika msemo. |
|---|---|---|
| *mifuko* | bags |  |
| | departure | |
| | identification | |
| | luggage | |
| | medical | |
| | occupation | |
| | passport | |
| | travel | |

**Uchunguzi wa kiafya utapana kwa shirika lako la makazi mapya habari kuhusu hali yoyote ya afya ambayo inaweza kuhitaji uangalifu Marekani.**

**Kabla ya kufika Marekani, shirika lako la makazi mapya litajuwa jina, miaka, kabila yako na lugha unayosema.**

**Makazi mapya yatatumia habari kuhusu wewe kwa kuchagua eneo la makazi mapya.**

## UCHUNGUZI WA KIAFYA



Uchunguzi wa kiafya utahitajiwa kwa watu wote katika jamaa lako. Uchunguzi wa kiafya ni bure, na, wafanyakazi wa shirika la makazi mapya watafanya miadi ya tarehe yakufaniwa uchunguzi wa kiafya. Habari za za afya yako zita zitajulikana tu kwa watu ambao wanakusaidia katika mchakato wa makazi mapya.

Kuna sababu tatu kwa uchunguzi wa afya:

- ❒ Kujuwa kama wewe au watu wengine katika jamaa lako ana matatizo ya kiafya na wanahitaji matibabu.
- ❒ Kuhakikisha kwamba hakuna mtu yeyote anaye kuwa na ugonjwa ya kuambukia na ambayo inaweza kufanya wewe ama mwengine katika jamaa lako asiweze kuingia Marekani.
- ❒ Kuiipa shirika lako la makazi mapya habari kuhusu hali yoyote ya afya inaweza kuhitaji uangalifu Marekani.

## MWELEKEZO YA KIUTAMADUNI (CULTURAL ORIENTATION)




Kabla ya kuja Marekani, wakimbizi wengi wanahudhuria mwelekezo wa kiutamaduni kutoka kwa wafanyakazi wa shirika la makazi mapya. Mwelekezo wa kiutamaduni huwapa habari kuhusu maisha ya Marekani, kutokana na habari zinazo patikana katika kitabu hiki. Lengo la mwelekezo ya kiutamaduni ni kukusaidia kuendeleza matarajio ya kweli kuhusu maisha ya Marekani na kuelewa uelevu wa yale utakutana nayo katika myezi yako ya kwanza nchini Marekani.

## UKAGUZI WA USALAMA

Wakimbizi wote wanapaswa fanya ukaguzi wa usalama unaofanywa na wakubwa wa serikali ya Marekani kabla ya kusafiri kwenda Marekani. Kwa kawaida, ukaguzi huu unafanyika kabla ya mahojiano na Idara ya Usalama. Wakati mwingine ukakuzi wa usaalama ungine unalazimishwa kabla ya kuondoka.

## SHIRIKA LAKO LA MAKAZI MAPYA



Kila mkimbizi anayekubaliwa kuiingia Marekani anapewa shirika la makazi mapya kabla ya kuondoka. Kituo cha taratibu za safari kitapeleka habari zifuatazo kwenye shirika lako la makazi mapya:

- ❐ Jina lako, umri wako, kiwango chako cha elimu, na kazi yako.
- ❐ Majina, umri, kiwango cha elimu, na kazi za watu wa jamaa lako watakaoenda na wewe.
- ❐ Asili yako, nchi ya asili, na dini yako.
- ❐ Matatizo yoyote ya kiafya ambayo yatahitaji kuangaliwa utakapofika Marekani.
- ❐ Majina, Anwani, na nambari ya simu za wandugu ao marafaki zako ambao tayari wanaishi Marekani.

### KUCHAGUA ENEO LA MAKAZI MAPYA YAKO



Shirika la kitaifa la makazi mapya litatumia habari hizi kuchagua eneo la makazi mapya yako. Kama ndugu yako wa karibu (bibi, mtoto, mzazi, kaka ao dada) iko tayari nchini Marekani, na umewapa wafanyakazi wa kituo cha taratibu za makazi mapya nambari ya simu na/au anuani yao, shirika la makazi mapya litajaribu kukupa makazi yako katika mji wanaoishi. Kama unaomba upelekwe karibu na rafiki au ndugu ambaye si ndugu wa karibu, shirika la makazi mapya litatizama kama itawezekana katika eneo hilo kupata huduma utakazohitaji na kama itawezekana kupata kazi huko. Kama kuna wandugu ambao si wakaribu, watachukuliwa  kupatiwa makazi mapya Marekani, unaweza kuomba makazi mapya katika jamii moja nao, lakini hakuna uhakika kwamba hii itawezekana.

Kama shirika la makazi mapya halina habari kamili ya sasa ya ndugu yako na marafiki ambao tayari wako Marekani, unaweza kupata makazi mapya kwenye mji mabli nao.

**Nimuhimu kutoa taarifa ya sasa kuhusu jamaa yako na marafiki Marekani kama unataka kupelekwa karibu nao.**

**Lazima ujulishe IOM au wafanyakazi wa shirika la makazi mapya kuhusu mabadiliko yoyote unapo subiri kusafiri. Kutofanya hivyo inaweza kukuchelewesha kutoenda kwa wakati.**

**Nyaraka katika mfuko wako wa IOM ni ya muhimu sana. Weka mfuko wako karibu nawe kila mara unaposafiri.**

Wape wafanyakazi wa kituo cha taratibu za safari wa Shirika la Makazi mapya habari za kutosha kama uwezavyo ili shirika la makazi mapya liweze kuchagua mahali ambayo ni bora kwako. Kutoa habari hizi haita badilisha hali yako ya uhamiaji au harikisha wakati utaondoka. Zina badilika tu wakati unaweza kupewa makazi mapya Marekani. Ni kwa mafaa yako kutoa habari hizi.

Wakati shirika lako la makazi mapya limeamua mji ambapo utaishi, kituo cha taratibu za safari cha Shirika la Makazi a mapya litakusaidiya kutayarisha safari yako. Kabla ya kuondoka, utajulishwa wapi utaishi Marekani.

***Wakati utajuwa, jaza habari hapa chini. Inawezekana usijuwe habari zingine mpaka kisha kufika Marekani.***

Mji/jiji yangu mpya: ________________________________________

Dala yangu mpya: __________________________________________

Shirika langu la makazi mapya: ______________________

Anuani na namba ya shirika langu la makazi mapya: __________


__________________________________________________________

## MATAYARISHO YA SAFARI

International Organization for Migration (IOM) litatayarisha safari yako ya Marekani. Kama kuna mabadiliko yoyote katika jamaa lako wakati unaposubiri, kama vile ndoa, kifo, au kuzaliwa, lazima uarifu IOM au wafanyakazi wa kituo chako cha taratibu cha makazi mapya. Kama haufanyi hivyo, unaweza chelewesha safari yenu.

## MIKOPO YA SAFARI

Jamaa yako inaweza kupata mkopo wa kugharimia safari yenu Marekani. Watu katika familia yako wenye umri zaidi ya miaka kumi na nane wanapata kila mmoja mkopo wake. Katika hatua nyingine, Utaweka sahihi kwenye karatasi iitwayo waraka wa kuahidi. Waraka wa kuahidi huu ni ahadi unayoifanya kulipa mkopo yako ya safari katika miaka mitatu kisha kufika Marekani.



Kisha miezi michache, jamaa ya Pooja ilipata hati ya deni kutoka kwa posta kwa ajili ya waraki wa kuahidi wa IOM. Pooja alikumbuka yakuwa aliweka sahihi kwenye karatasi kuhusu hayo, lakini hakuweza kukumbuka ilikuwa kwa sababu gani. Vipi unaweza kumfasiria Pooja hati hii? Nini unaweza kumueleza kuhusu maana ya kulipa deni hii? Ikiwa Pooja anamaswali mengine, kwa mtu gani anaweza kuuliza?

Kisha miezi michache baada ya kufika Marekani, shirika lako la makazi mapya litaanza kukutumia kila mwezi hati ya deni ao taarifa ya kukutaka uanze kulipa sehemu ya pesa ya deni. Pesa unazolipa zinakwenda kwenye mfuko wa kuwasaidia wakimbizi wengine kusafiri Marekani. Unapolipa deni ya mkopo hii, unaanza kujenga historia nzuri ya mkomo Marekani. (Angalia sura ya 9 kujifunza zaidi kuhusu historia ya mkopo). Kutolipa inaweza kutuma unakuwa na historia mbaya ya mkopo. Kama huwezi kulipa kwa sababu fulani, zungumza na shirika lako la makazi mapya mara moja.

## MFUKO WA IOM NA BAHASHA YA KUFIKA




Kabla ya kuondoka, wafanyakazi wa IOM watakupa mfuko wa plastiki ambayo ina bahasha ya nyaraka za kufika na bahasha nyingine ndogo. Bahasha hizi zitakuwa na kadi yako ya I-94 na fomu za forodha, fomu za afya, nakala za X-ray ao CD, nyaraka halisi za makazi mapya, baruwa ya bweni, na tiketi yako. Utahitaji vitu hivi kwa kuingiya katika Marekani na kusafiri mpaka unapoenda mwishoni. Uwenaungalifu mkubwa kuhusu mfuko wako wa IOM na nyaraka zako. Uziweke karibu nawewe kwa nyakati zote. Usifunguwe bahasha na wala usiweke mfuko wako wa IOM au yaliyomo kwenye sanduku yako ya safari au miziko ulizo ziandikisha. Utakapofika kwenyi uwanja wa ndege utakapo ingilia Marekani pa kwanza (uwanja wa ndege wa kwanza ambapo utafikia), mfanyakazi wa IOM atakutana nawe na atakusaidia katika taratibu za uhamiazi. Tafadhali, ukumbuke yakuwa mfanyakazi wa shirika la makazi mapya tu au maofisa wa uhamiaji wa Marekani wanaweza kufungua nyaraka.


**Kuna baadhi ya vitu ambavyo huwezi kuchukua nchini. Uwe na ufahamu wa vitu hivi kabla ya kufunga mifuko yako.**

***Hapa chini kuna mifano ya baadhi ya nyaraka unaweza kutaka kuchukua mapoja nawe. Chapa duara kwa nyaraka ambazo wewe na jamaa yako mtachukua zaidi ya nyaraka katika mfuko yako ya IOM.***



Dawa ulizopewa na daktari


Nkala ya Elimu


Degri, Diploma, au Vyeti


Rekodi ya chanjo


Vyeti vya kuzaliwa


Vyeti vya ndoa


Tafsiri ya kiingereza ya hati yoyote muhimu


Rekodi ya matibabu

***Chapa au andika nyaraka nyingine yoyote ya lazima ambayo utahitaji.***


CAL COR Cultural Orientation Resource Center

**_Kumbuka kufunga nyaraka zako za lazima kwenyi mfuko wako wa kubeba!_**

## MIZIGO YA SAFARI



Kampuni za safari kwa ndege yanakiwango juu ya ukumbwa na uzito wa mifuko ambazo kila mtu anaweza kuchukua. Viwango hizi zinatofautiana kulingana na ambapo unaenda na kwa kampuni gani ya ngege anasafiri. Utaambiwa mifuko ngapi unaweza kuchukua pamoja nawe kabla ya kusafiri, Kwa kawaida inaruhusiwa mfuko moja mkononi. Mfuko wa mkono ni mfuko ambayo unachukua katika ndenge pamoja nawe. Utaruhusiwa pia kuchukua mfuko moja kama mfuko wa kuandikisha. Mfuko wakuandikisha ni mfuko ambayo inaenda chini katika ndege aambapo mifuko inawekewa. Uwena uhakika ya kwamba mfuko yako yanafungiwa vizuri na usiweze kupoteza kitu chochote wakati wa safari.

---

Pray Meh alifunga mifuko yake na uangalifu wote lakini hakujuwa chakufanya wakati watoto wake watatu walinungunika kuhusu baridi katika ndege. Pray Meh angelipaswa kufunga nini katika mfuko wake wa mikononi ili watoto wasi hisi baridi kwenyi ndege?

---

## VITU AMBAVYO HUWEZI KUCHUKUA MAREKANI

Sheria za Marekani haziruhusu baadhi ya vitu kuletwa Marekani. Huwezi kuleta silaha. Huwezi kuchukua vitu kama visu, au mikasi kwenye mzigo wako wa mkononi unaouchukua ndani ya ndege, lakini unaweza kuyafunga katika mifuko yako unayo andikisha. Vitu vingine ambavyo huwezi kuchukua katika Marekani ni mimea, matunda, mboga, nyama, au madawa ya kulevya. Unaweza kuleta dawa ulizopewa na daktari wako lakini lazima ziwe kwenye vikopo vyenye maelezo. Lazima uwe na agizo la daktari kuhusu agizo lolote la dawa anayo.

---

Farah alifunga sindano ya kushona yake ndogo kwenyi mfuko wake wa mkono na alikuwa na huzuni sana wakati wa mamlaka wa uwanja wa ndege alimuambia yakuwa hawezi kuichukuwa sindano hiyo kwenyi ndege. Farah angalipaswa fanya nini tofauti?

---

Ikiwa unamaswali kuhusu ambavyo unaweza kuchuwa Marekani, uulize mfanyakazi wa IOM.

# 3 KUSAFIRI MAREKANI

***Ukarasa huu na ukarasa ufwatao unaonesha picha ya makundi matatu ya vitu. Andika namba 1 katika kundi la vitu ambavyo lazima vifungwe katika mizigo yako yakuandikishwa. Andika namba 2 katika kundi la vitu ambavyo lazima vifungwe kwenyi mzigo wako wa mikononi. Andika namba 3 kwenyi kundi la vitu ambavyo huwezi kuchukua.****

1. Vitu hivi lazima vifungwe katika mzigo wa kuandikishwa.
2. Vitu hivi lazima vifungwe katika mzigo wa mikononi.
3. Huwezi kuchukua vitu hivi.

**a.**



Chakula, chupa na napi kwa ajili ya watoto




Kitabu cha Mwongozo



Mchezo tulivu ya watoto



Nyaraka za masomo, za kusika na afya na nyingine muhimu



Mavazi ya joto



Kiasi kidogo cha tumbaku



Vitabu ao magazeti



Kiasi kidogo cha maji katika plastiki ya waji



Pesa



Agizo la daktari lenyi agizo



Saa



Vitafunio



Mwavuliu



Mapambo ya vitu

*Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 220.

**b.**


Silaha au kitu chochote ambacho kinaweza kutumiwa kama silaha


Mimeya na wanyama


Programu haramia, musiki, cinema, nk.


Matunda na mboga


Dawa za kulevya


Kibiriti


Madawa zisijo julikana


Maji/kinywaji


Mbegu na Viungo

**c.**


Vyombo vya muziki


Vyupa viwili vya kileo vyenyi kufungwa na vyenyi maelezo kwa upeo


Picha/kumbukumbu


Vitabu


Mavazi


Vyoo


Vitu vyenye ncha kali


Radio


Koti ya msimu wa baridi

**Huwezi kuvuta kwenyi ndege.**

**Kumbuka kula na kunywa unapopewa chakula, ili uweze kuwa na nguvu pia na afya wakati wa safari.**

*Fikiri kuhusu ambavyo utachukua kwakuhamia Marekani. Jibu maswali zilimo katika chati ilio hapa chini kwa kuandika wala kwa kuchapa, wala yote mawili.*

| Vitu gani mbali mbali utasafiri navyo? | Vitu gani mbali mbali utaacha? |
| --- | --- |
| | |

# SAFARI YAKO

## SAFARI YA NDEGE

Hii inaweza kuwa mara ya kwanza wewe una safiri katika ndege.

*Fikiri kuhusu wasiwasi yote ambayo wewe ama mtu mwengine wa jamaa lako mnayo kuhusu safari. Unapaswa kutoa wasiwasi haya wakati wa darasa la mwelekeo wa kiutamaduni, kabla ya kupanda ndege.*

Hapa kuna baadhi ya mambo muhimu ya kukumbuka:

**MKANDA WA USALAMA WA KITI**. Lazima uvae mkanda wako wa usalama wakati wa kuondoka, kutua, na wakati ishara ya mkanda wa usalama inawaka. Ni wazo nzuri kuvaa mkanda wako wa usalama wakati wote.



**KUVUTA.** Sigara hairuhusiwe kwenyi ndege yoyote.



**WAHUDUMU WA NDEGE.** Wahudumu wa ndege wana hakikisha wasafiri wako salama na wanastarehe. Sikiliza maelezo ambazo wahudumu wa ndege wanapana. Kama unahitaji kitu chochote, kama vile maji ama blanketi, uliza muhudumu wa ndege.



---

Win Tun hakula chakula chake cha bure kilichopewa kwenyi ndege kwenda Marekani kwa sababu haikuwa ya kawaida. Alifika Marekani akiwa na njaa sana. Jinsi gani unaweza kuepuka hali hii? Ukiwa na njaa ama kiu kwenyi ndege, nani ndiye ambaye unapaswa kuomba msaada?

---

**CHAKULA.** Chakula na vinywaji katika ndege za kimataifa ni bure. Utapewa vyakula mara kadhaa wakati wa safari ndefu. Uhakikishe yakuwa unakula chakula ambacho unapewa ili uweze kuwa na nguvu na kuwa na afya katika safari yako ndefu.




**MAJI.** Katika ndege hewa ni kavu, kwa hivyo ni muhimu unywe maji. Kama hunywi maji unaweza kujisikia mgonjwa ama wakuchoka sana.



**POMBE.** Unaweza kunywa pombe kwenyi ndege nyingi, lakini si wazo nzuri kunywa pombe kwenyi ndege kwa sababu inaweza kusababisha mwili wako upotezo wa maji na kuwa kavu.



**MAZOEZI.** Kwa sababu utakuwa bado umekaa kwa masaa mengi, ni vizuri kusimama, kujinyosha na kutembeya kweye ndege mara mengi, mnapo safari.



**MABADILIKO KATIKA PRESHA YA HEWA.** Masikiyo yako inaweza kuwa kama yenyi kufungwa. Kwakutoa presha, tafuna ubani (Bazoka), mwayo, ama kunywa maji.



**KUBADILISHA VITI.** Kila mtu katika ndege anapewa kiti chake na ni lazima abaki katika kiti kile kwa safari nzima. Mnaweza kubadilisha viti na wandugu ama marafiki kama wanakubali.



**Waakilishi wa IOM wanaweza kumsindikiza mkimbizi ambaye ni mgonjwa sana ama anayehitaji msaada kwa kutembeya.**

**Mnapofika kwenye uwanja wako wa ngede wa mwisho, ndugu, rafiki ama mfanyakazi wa shirika la makazi mapya watakuwa hapo kwa kuwakaribisha.**



**WATOTO.** Watoto wenyi umri chini ya miaka miwili wanasafiri kwa beyi rahisi kama wanakaa katika mikono ya wazazi wao wakati wa safari nzima. Kumbuka kumleteya mtoto chakula na mengi ya nepi kwa safari.



**VYOO**. Kuna vyoo kwenye ndege. Karatasi ya choo tu ndiyo inapaswa kutupwa katika choo. Maji kwenyi sinki inapaswa kutumiwa kwa kunawa mikono tuu, hapana kwa kunywa.



**UGONJWA KATIKA SAFARI.** Ikiwa unagonjwa kwenye ndege na unahitaji kutapika, kuna mifuko katika mfuko nyuma ya kiti cha mbele yako. Kisha kutumiya mfuko, uitupe katika takataka katika choo.

## MAHALI PA MABADILISHO

Wakimbizi wengine wanaweza kuhitaji kupitia kwa viwanja vya ndege vingine kabla ya kufika Marekani. Pahali pa mabadilisho ni kituo, kwa kawaida kwakubadilisha ndege. Kwenye mahali pa mabadilisho, unaweza kuhitaji kupitia kwa kituo cha ugaguzi cha uhamishaji. Mwakilishi wa IOM ama kampuni ya ndege watakusaidia kupata jinsi ya kuchukuwa ndege yako ifwatayo. Utakapofika Marekani, wawakilishi wa IOM watakutana nawe kwenye uwanja wa ndege ya kwanza na kukusaidia katika taratibu za kufika. Watakusaidia pia kupata pahali pa kulala, ikiwa inayahitaji, ama kukusaidia kusafiri mpaka mahali pako pa uhamishaji mpya. Ikiwa unagonjwa, IOM itahakikisha ya kwamba una mtu wa kukusaidiya wakati wa safari yako.

## TARATIBU ZA UHAMIAJI

Maofisa wa uhamiaji wa Marekani watafungua bahasha yenye nyaraka za kufika na kuangalia nyaraka hizo. Kwa mara chache, makosa yanafanywa kwenye nyaraka za kuingia, kama vile maandiko ya jina lako yasiyo sahihi. Ukiona makosa yoyote kwenye nyaraka hizi, jambo bora lakufanya ni kuwaambiya shirika lako la makazi mapya unapofika ili waweze kuyasahihisha.




### *I-94 na kadi za EAD*

Kadi yako ya I-94 itapigwa muhuri na watakuirudishia. Uta pigwa picha na kuchukuliwa chapa ya vidole kwa ajili ya waraka wa kukuruhusu kufanya kazi (Employment Autorization Document [EAD]) kadi yako ya EAD itafanywa na kutumwa kwa shirika lako la makazi mapya. Kadi yako ya I-94 na waraka wa kazi wa EAD ni nyaraka muhimu kwa sababu zinaonesha kwamba hali yako kama mkimbizi Marekani ni ya kisheria na unaruhusiwa kufanya kazi.

## FORODHA


Utakapo maliza taratibu za uhamiaji utachukua mizigo yako na utaendelea kwenda kwenye sehemu ya farodha. Maofisa wa farodha wataangalia fomu yako ya maelezo ya forodha na kwenda wakapewe mzigo yako. Vitu vilivyo kwenye mabegi yako vikipata kibali cha forodha, utakuwa tayari kwenda kwenye sehemu ya mwisho ya safari yako.

## KATIZO LA SAFARI YA USIKU

Unaweza kulazimishwa kupitisha usiku kwenye uwanja wa ndege wa kwanza ulipofikia mpaka kesho kama huwezi kuchukua ndege yako ifwatayo. Kama jambo hili linatokea, IOM litafanya mipango ya chumba katika hoteli (na kukulipia) na pia litafanya mipango ya safari za ndege zitakazokufikisha unapokwenda siku ifwatayo.

## MWISHO WA SAFARI

Kwenye bandari ya kuingilia, utapokea kadi IOM yenyi habari kuhusu wewe na namba dharura ya simu ya kuita ikiwa unahitaji msaada. Kadi itakuwa kwenye Kamba ambayo unaweza kuvaa shingoni mwako. Utakapofika kiwanja cha ndege cha mwisho, jamaa, rafiki, ama mwikilishi kutoka shirika lako la makazi mapya atakutana nawe kwenye sehemu ya kuchukua mizigo. Ikiwa, kwa sababu yoyote, hakuna mtu aliyekuja kukutana nawe, tafadhali wasiliana na polisi wa uwanja wa ndege mara moja. Mtu yule atakusaidia kufanya mawasiliano na shirika lako la makazi mapya, ndugu, ama IOM kwakutumiya namba dharura ya simu kwenye kadi IOM.



Jamaa ya Rai ilifiki kwenye uwanja wa ndege ya mji wao mpya wakichoka lakini wakifurahi pia. Ila hakukuwa mtu wakuwangojea kwenyi uwanja wa ndege. Lazima jamaa ya Rai ifanye nini?

***Ikiwa hakuna mtu yeyote aliye kuja kukutana nawe kwenye uwanja wa ndege, usiwe na woga! Uwe mtulivu tu na uwasiliyane na polisi wa uwanja wa ndege kwa msaada.***



***Fikiri kuhusu vipi unaweza kujisikia anapofika kwenye uwanja wa ngege wa mwisho wa safari yako. Kwenda kwa kiambatisho C: Nyuso za mhemuko kwenye ukarasa 226 na ufikiri kuhusu sura gani inaweza kukabiliana na hisia hizo. Uzichape kwenye duara hapa chini.***

- ❒ Utakuwa ukichoka? Ukiwa na njaa? Ukiwa na kiu?
- ❒ Utajisikiya mwenyi furaha? Wa wasiwasi?
- ❒ Utakuwa mwenyi msisimko? Wa kusikitika?
- ❒ Unafikiri, itakuchukua mda gani iliuweze kuzoweya mazingira yako mapya?

***Unaweza kuwa mwenyi kuchoka kisha safari yako ndefu, lakini utaanza kujisikia vizuri kisha siku moja ama mbili!***

## KAMILISHA*

***Chagua jibu bora zaidi kwa maswali hapa chini ukifanya chaguo bora.***
***Hii ni mfano:***

*Lugha gani ndio inazungumzwa na watu wengi zaidi Marekani?*

a. Kichina.

(b.) Kingereza.

c. Kiugerumani.

***Watu wengi Marekani wanazungumza kiingereza. Kwa hiyo jibu ni b. Kiingereza.***

1. Rafiki yako alikamilisha uchunguzi wa kiafya na ukaguzi wa usalama na iko tayari kusafiri Marekani. Kisha mke wake anazaa. Anawasiwasi kuhusu nini atapaswa kufanya. Lazima awajulishe IOM ama wafanyakazi wa kituo cha Shirika lake la makazi mapya kuhusu mtoto mwengine katika jamaa lake?

   a. Ndiyo, kwa sababu kama hawajulishi, safari yake inaweza kuchelewa.

   b. Hapana, kwa sababu kama anawajulisha, safari yake inaweza kuchelewa.

2. Ni lazima ufunge mfuko wako wa IOM kwenye mizigo za kuandikisha?

   a. Ndiyo.

   b. Hapana.

   c. Haijalishi mahali unafungisha mfuko wako wa IOM.

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenye ukarasa 220.

3. Unapofunga mzigo yako, vitugani HUPASHWI KUFUNGA kwa sababu haviruhusiwi kupelekwa nchi Marekani?

    a. Mimeya.

    b. Kibiriti.

    c. Madawa ya kulevya.

    d. Dawa ulizopewa na daktari wako (zenyi maelezo).

    e. Chaguo a, b, na c.

4. Je, lazima ulipe pesa kwa ajili ya chakula unayo pewa katika safari ya ndege ya kimataifa?

    a. Ndiyo.

    b. Hapana.

5. Unapofika kwenye uwanja wa ngede wa mwisho wa safari yako, nani ndiye unaweza kukuta akikungojea kwakukupokea?

    a. Rafiki.

    b. Ndugu.

    c. Mfanyakazi wa shirika la makazi mapya.

    d. Yote (au moja) ya hizo juu.

6. Kwa kutia saini kwenye waraka wa kuahidi, unakubali kulipa mkopo wako wa kusafiri katika myaka mingapi kisha kufika Marekani?

    a. Mwaka 1.

    b. Miaka 3.

    c. Miaka 5.

    d. Miaka 10.




# Sura Ya Nne
## SHIRIKA LA MAKAZI MAPYA

4

Wafanya kazi wa shirika lako la makazi mapya watakuwa viongozi wako wakuu katika jamii yako mpya. Usikilize kwa makini yale wanayo kueleza, na kuwapatia habari nyingi kama iwezekanavyo kuhusu wewe mwenyewe na jamaa lako. Wana uzoefu kwa kuwaongoza wakimbizi kwa juma zao za kwanza Marekani na wanaweza kukutolea habari sahihi kuhusu maisha katika jamii yako mpya.

### Sura Hii Itajadili

- Jukumu la shirika lako la makazi mapya
- Huduma ambazo shirika lako la makazi mapya litakutolea ama litahakikisha unayapata
- Haki zako na majukumu wakati wa kufanya kazi na shirika lako la makazi mapya

**Usikilize kwa makini yale wafanyakazi wa shirika lako la makazi mapya wanakueleza. Wanaweza kukutolea habari sahihi kuhusu maisha Marekani.**

## MANENO MUHIMO YA KIINGEREZA

Maneno ya kiingereza yafuatayo hutumiwa wakati wa kuzungumza kuhusu jukumu la shirika lako la makazi mapya nchini. Maneno haya yatakuwa na mafaa kwako kuyajifunza.

***Sema neno katika kiingereza. Andika hilo neno katika lugha yako ya asili. Kisha chapa picha ya neno, andika maana yake, au uitimiye katika msemo. La kwanza limefanyika kwa ajili yako.***

| Katika lugha yako | Katika kiingereza | Chapa picha ya neno, andika maana yake, au uitumiye katika msemo. |
|---|---|---|
| *shirika* | agency | *Shirika ni kampuni au shirika ambayo inasaidiya makampuni zingine au watu.* |
| | assistance | |
| | case manager/ caseworker | |
| | help | |
| | responsibilities | |
| | rights | |
| | services | |
| | staff | |

**Serikali inafanya kazi na mashirika ya makazi mapya kuwapatia wakimbizi makazi mapya.**

**Shirika lako la makazi mapya litakusaidia na gharama za msingi na vitu unahvyo vihitaji katika masiku 30 zako za kwanza Marekani.**

***Ni mambo gani ya muhimu unapaswa kushiriki na shirika lako la makazi mapya kuhusu wewe mwenyewe na jamaa lako? Kwa mfano, majina yenu, miaka yenu, na kadhalika.***

## JUKUMU LA SHIRIKA LAKO LA MAKAZI MAPYA



Marekani, serikali inafanya kazi na mashirika ya makazi mapya kuwapatia wakimbizi makazi mapya. Serikali inaweka sheria na miongozo na inatoa fegda za huduma za lazima wanazopata wakimbizi. Mashirika ya makazi mapya yanatoa huduma hizi na inawezekana yatowe misaada zingine pia. Shirika lako la makazi mapya litakusaidia na gharama za msingi na huduma unazo zihitaji katika masiku na miezi zako za kwanza za maisha yako Marekani. Shirika la makazi mapya litakuunganisha pia na huduma zingine unazohitaji kwa kuanza maisha yako mapya.

---

Janet, kijana mwanamke ameishi Marekani kwa zaidi ya mwezi 1. Wakati huo, wafanya kazi wa shirika la makazi mapya walimutolea huduma ambazo wakimbizi wote wanapata. Siku moja, Janet alimwita maneja wa kesi yake na alimuomba ampeleke kwenye duka. Maneja wa kesi alimuambia Janet ya kwamba anakazi nyingi yakuwapeleka jamaa mpya ya wakimbizi kwenye kliniki na hawezi kuja. Akamukumbusha Janet kwamba amekwenda naye dukani mara chache, na kwamba anajua jinsi ya kutumia kadi yake ya chakula kwa kununua chakula. Anamwambia piya ya kwamba duka ni karibu na nyumba yake na ya kwamba anaweza kwenda huko kwa miguu. Alimuambia Janet ya kwamba lazima sasa ajaribu kufanya mambo haya yeye mwenyewe, na ya kwamba anaweza kuomba msaada kwa kaka yake, ambaye anaishi karibu naye. Janet anahasira na anahisi kuwa meneja wa kesi hamujali. Kwa nini Janet anamtaka meneja wa kesi amuchukue? Kwa sababu gani meneja wa kesi hanauwezo wa kumchukua Janet dukani? Nini unaweza kueleza Janet akikunungunikia kuhusu meneja wake wa kesi?

---

# SURA YA NNE 4

## MASIKU 30 ZA KWANZA


Mashirika ya makazi mapya yatakusaidiya na gharama za lazima na gharama za kuishi kwa siku 30 za kwanza nchini Marekani. Baadhi ya mashirika yatalipa gharama mara moja. Wengine watakupa pesa, na wewe utalipa gharama mwenyewe.

## MPAKA SIKU 90

Kipindi cha siku 30 kinaweza kuongezewa hadi siku 90 baada ya kuwasili kama misaada ya makazi mapya unazozihitaji haziwezi kukamilika katika muda wa masiku 30. Lakini kumbuka: Wamerikani, wanathamani kujitegemea, hivyo utatarajiwa kufanya kazi na kuchukua haraka jukumu kwa maisha yako mwenyewe iwezekanavyo.



***Chapa duara kwenye picha za vitu 5 muhimu hapa chini ambavyo vinaonesha yale unayoweza kuyapenda zaidi kujifunza kuhusu maisha Marekani.***



Haki na madaraka



Usafirishaji



Darasa la kiingereza



Makao



Matumizi ya fedha



Jukumu za shirika la makazi mapya



Huduma za Jamii



Kazi



Elimu




Afya



Marekebisho ya utamaduni Marekani

**Unaweza kumuona mfanyakazi wa shirika la makazi mapya akifanyakazi pamoja na wale aliojitolea, wandugu, na watu wengine wa jamii nyingine kwakutoa huduma hizi kwa ajili yenu.**

***Pamoja na mwengine, cheza-jukumu kuzungumza na meneja wa kesi yako kuhusu mambo ambayo unataka kujifunza zaidi. Jaza misemo:***

- ❒ Unaweza kunieleza zaidi kuhusu …
- ❒ Ninachanganyikiwa kuhusu …
- ❒ Unaweza kunisaidia na …
- ❒ Nataka kujifunza zaidi kuhusu …
- ❒ Sijuwi maana ya ______.

***Kisha, badili majukumu!***

---

Kabla ya kufika Marekani, Phurba na Sita Maya waliandika mada ambayo walitaka kujua kuhusu: Makao, elimu ya watoto, madarasa ya kiingereza, na kutafuta kazi. Baada ya kuishi marekani kwa muda mrefu kidogo, Phurba na Sita Maya wametambua yakuwa maswali yao yalibadilika. Sasa walitaka kujua zaidi kuhusu kuendeleya kufanya kazi, matumizi ya fedha, huduma za jamii, na jinsi ya kukabiliana na mshtuko wa utamaduni. Kwa nini unafikiri maswali yao yalibadilika? Unafikiri ya kwamba yako pia itabadilika baada ya muda? Kama vitu ambavyo unahitaji kujifunza vitabadilika, hii inaweza kuwa changamoto kwako?

---

## HUDUMA ZINAZO HITAJIKA

Ukarasa huu na unayo fwata, unaonesha picha ya huduma ambazo mashirika yote ya makazi mapya lazima zizitowe au kuhakikisha kwamba mwengine atayatoa, kwa wakimbizi wote kwa mda wa siku 30 yao ya kwanza Marekani. Unaweza kumwona mfanyakazi wa shirika la makazi mapya akifanya kazi na waliojitolea, ndugu, na watu wengine wa jamii kwa kutoa huduma hizi kwa ajili yenu:



Kukuta kwenye uwanja wa ndege na kukupeleka nyumbani kwako.



Kutoa mavazi muhimu za msimu. Silazima mavazi yale yawe mapya, lakini ni lazima ziwe safi na katika hali nzuri.




Kukupa nyumba iliyo salama, nzuri na safi.



Kukupa wewe na kila mtu mzima katika jamaa lako fedha ya mfukoni kwa ajili ya matumizi binafsi.




Kutoa samani na vitu vya nyumbani. Silazima vitu viwe vipya, lakini lazima viwe safi na katika hali nzuri.



Kutoa chakula ma posho ya chakula kulingana na ukubwa wa jamaa mpaka mtakapo pokea misaada ya chakula au kujitolea chakula chenu wenyewe.



Kukusaidiya kwakuomba fedha na msaada wa matibabu.





Kukusaidiya kupata kadi yako ya ruzuku ya serikali.


**Muda mfupi kisha kuingia Marekani, utahitaji kuanza kutafuta kazi kwa ajili ya kuilipa gharama yako mwenyewe.**



Kukusaidia kujiandikisha katika darasa la lugha la kiingereza ikifaa.




Kutoa usafiri kwa mahojiano ya kazi na mafunzo ya kazi.



Kukusaidia kujiandikisha katika huduma za kazi, ikifaa.



Kutoa usafiri na tafsiri kama zinahitajika kwa ajili ya huduma zote zinazohitajika.



Kukusaidiya kupata vipimo vyote vya afya na huduma yoyote ya afya unayohitaji.



Kukusaidia kujiandikisha na huduma la chaguzi ukiwa mme wa kati ya umri wa miaka 18 hadi 25.



Kuwaandikisha watoto wako katika shule.



Kutolea mwelekeo mpya kuhusu jamii lako na maisha Marekani.

Shada na Jamaa lake walifika katika nyumba yao mpya na walikuwa na walivunjwa moyo kuona vitu vya nyumba yao havikukuwa vipya. Shada alishangaa pia kujua ya kwamba shirika lake la makazi mapya halikumtayarishia kazi kabla ya kufika kwake. Lazima atumike na mtaalumu wa kazi kwa kupata moja. Kwa nini Shada alishangazwa? Ungelikuwa Shada ungekumbuka nini?

Maana ya huduma hizi ni kukusaidia kupata kuanza katika maisha yako mapya. Utahitaji kutumia vizuri huduma ambazo shirika lako la makazi mapya litakutolea, kwa sababu kwa kawaida itakuyapatia kwa siku 30 tu baada ya kufika. Huduma hizi zinaweza kuendelea kwa muda wasiku 90, lakini kama tu hawawezi kukamilishwa katika siku 30 za kwanza.

Unapoingia Marekani, utachukuwa mzigo wa jamaa lako na wewe mwenyeye. Lazima uanze kutafuta kazi haraka iwezekanavyo. Shirika la makazi mapya hailazimishwi kukutafutia kazi. Shirika la makazi mapya hailazimishwi pia kukutolea simu ya mkono, televisheni, gari, ama kompyuta, au kulipa mkopo yako ya safari na bili zengine. Utahitaji kutafuta kazi na kupata fedha kwa kukununua vitu hivi na kulipa deni zako mwenyewe.

## HAKI ZAKO NA MAJUKUMU WAKATI WA KUFANYA KAZI NA SHIRIKA LAKO LA MAKAZI MAPYA

Una haki na majukumu wakati wa kufanya kazi na shirika lako la makazi mapya.
Haki unazo ni:



- ❒ Kupata huduma zinazohitajika katika siku 30 zako za kwanza Marekani.
- ❒ Kuchukuliwa na heshima na haki na wafanyakazi wa makazi mapya.
- ❒ Kujua maelezo ya kesi yako.
- ❒ Kuweka habari za kesi yako binafsi. Wafanyakazi wa shirika la makazi mapya hawawezi kushiriki habari za siri kuhusu wewe ama jamaa lako bila ighini yako, isipokuwa habari hizi zinahitajika kwa kukulinda wewe ama mtu mwengine.

**Unapo fanya kazi na wafanyakazi wa shirika lako la makazi mapya, heshimu wakati, na uwaulize maswali yoyote na kuwapa matatizo yako.**

Pia, una majukumu kwa shirika la makazi mapya inayo kukusaidia. Kati ya jukumu hizo kuna:

- ❒ Kuheshimu wakati.
- ❒ Kuwa na subira wakati unaomba mambo isiyo ya haraka.
- ❒ Kujadiliana na wafanya kazi wa makazi mapya na heshima.
- ❒ Kuwasiliana na wafanyakazi wa shirika la makazi mapya ukiwapa taarifa kuhusu mabadiliko katika hali yako (kwa mfano, kazi mpya au ugonjwa mbaya), au kwa kuuliza maswali na kuwapa matatizo yako.




**Ijapokuwa baadhi ya mashirika ya makazi mapya ni shirika la kidini, hayaruhusiwi kuwashawishi wakimbizi kuingia kwenye kikundi cha dini fulani.**

***Chapa duara haki na jukumu zinazotajwa kwenye ukarasa 51 na 52 ambazo zitakuwa mapya kwako kama mkimbizi katika Marekani.***

***Mwambiye mwenzako kuhusu haki na jukumu ambazo wewe na shirika lako la makazi mapya munazo kwa upande wa kila mmoja.***

***Haki na jukumu zako zitajenga uwiano, uhusiano nzuri na shirika lako la makazi mapya. Kwenye kipimo cha ukarasa ufwatao, chapa au andika kuhusu haki na majukumu utakayo kuwa nayo pamoja na shirika lako la makazi mapya Marekani.***



# SURA YA NNE 4

## AINA ZA MASHIRIKA YA MAKAZI MAPYA

Shirika la makazi mapya linaweza kuwa ni shirika la kidini, shirika binafsi, au shirika la watu wa asili fulani. Ijapokuwa baadhi ya mashirika ya makazi mapya yana uhusiano na vikundi vya kidini, hutarajiwi kushiriki katika shuguli za dini zao. Mashirika ya makazi mapya hayaruhusiwi kuwashaushi wakimbizi kuingia kwenye kikundi cha dini fulani.

***Hapa chini kuna picha ya shirika la makazi mapya. Unaona nini? Unatambua nini?***



**Kuna sababu nyingi nzuri za kubaki katika jamii yako ya makazi mapya.**

**Kama unafikiri kuhamia kwenye jamii nyingine, ujulishe shirika lako la makazi mapya.**

## KUHAMIA MJI MWENGINE



Kuna sababu nyingi nzuri za kubaki katika jamii yako ya makazi mapya kwa miezi 6 mpaka mwaka 1. Wewe na jamaa lako mtapata huduma zote zinazo tolewa, na utapata msaada na mwongozo wa shirika lako la makazi mapya.

Hii itakupa wakati unayohitaji kuanza kujifunza kuhusu maisha ya Marekani. Lakini, kama unafikiri kuhamia kwenye jamii nyingine, kumbuka kwamba shirika lako la makazi mapya halina jukumu la kukuhamisha, na shirika la makazi mapya la eneo unapohamia halihitajiwi kukusaidia. Ujulishe shirika lako la makazi mapya ikiwa unampago wa kuhama.

Kama unaamua kuhama, utahusika na msaada yoyote utakayo hitaji katika jamii yako mpya. Lazima ujulishe serikali ya Marekani anwani yako mpya katika ya siku 10 ya kuhama.

---

Kisha mwezi moja Marekani, Aung Chit hakuweza kupata kazi. Rafiki yake Tun Kyaw anayeishi kwenye mji ingine alimwambia Aung Chit ya kwamba angeweza kupata kazi ambapo Tun Kyaw alifanya kazi. Tun Kyaw alisema pia ya kuwa Aung Chit na jamaa lake wangeweza kukaaa pamoja naye katika nyumba yake. Aung Chit na jamaa lake, wali funga mizigo yao nakuhamia kwenye mji wa Tun Kyaw. Nyumba ndogo ya Tun Kyaw ilikuwa yenyi kujaa, shirika la makazi mapya la mtaa halikuweza kumsaidia Aug Chit, na kazi haikupatikana mara moja kwa Aung Chit ambapo Tun Kyaw anafanya kazi. Je, unafikiri Aung Chit alifanya amuo nzuri? Ungelikuwa Aung Chit, ungefanya nini?

---



***Fikiri kuhusu msaada ambayo shirika lako la makazi mapya litakutolea.***

- ❒ Namna gani shirika lako la makazi mapya litakusaidia?
- ❒ Kwa nini itakuwa changamoto ku hamia kwa jamii nyengine bila msaada ya shirika lako la makazi mapya?

## KAMILISHA*

***Kweli au Uongo? Pima ufahamu wako na maelezo hapa chini. Soma kauli hizi na zunguusha neno* Kweli *kama unadhani taarifa ni haki na zunguusha* Uongo *kama unadhani taarifa si sahihi.***

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mashirika za makazi mapya yanalazimishwa kukusaidia na mahitaji ya lazima na kiwango cha msingi cha maisha kwa masiku 30 ya kwanza. | **Kweli** | **Uongo** |
| 2. | Shirika la makazi mapya linapaswa kuwapa fanicha mpya. | **Kweli** | **Uongo** |
| 3. | Shirika la makazi mapya linapaswa kukutafutia kazi. | **Kweli** | **Uongo** |
| 4. | Una haki ya kujua maelezo ya kesi yako. | **Kweli** | **Uongo** |
| 5. | Wafanya kazi wa shirika la makazi mapya ni viongozi wako kwa jamii yako mpya na unapaswa kujisikia huru kuwauliza maswali yoyote anayo. | **Kweli** | **Uongo** |
| 6. | Kama unaamua kuhamia kwa jamii mpya, shirika lako la makazi mapya linapaswa kukusaidia kuhama na kukuunganisha na huduma katika jamii mpya. | **Kweli** | **Uongo** |

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 220.



5

# Sura Ya Tano
## NYUMBA

Nyumba nchini Marekani ni mara nyingi bei ghali, na kupata mahali pazuri kwa kuishi inaweza kuwa vigumu. Mwanzoni, utakuwa na pato ndogo, hivyo nyumba yako ya kwanza inaweza kuwa isiyo bora. Shirika lako la makazi mapya litahakikisha kwamba una nyumba wakati wa mwezi wako wa kwanza nchini Marekani. Shirika lako litatafuta nyumba iliyo safi, nafuu, na katika eneo yenyi usalama salama.

---

### Sura Hii Itajadili

» Mkataba ya kupangisha nyumba
» Usalama na matengenezo nyumbani

**Shirika lako la makazi mapya litahakikisha kwamba una nyumba wakati wa mwezi wako wa kwanza nchini Marekani.**



## MANENO MUHIMU YA KIINGEREZA

Maneno ya Kiingereza yafuatayo hutumiwa wakati wa kuzungumza kuhusu makazi mapya nchini Marekani. Maneno haya itakuwa na mafaa kwako kuyajifunza.

***Sema neno katika kiingereza. Andika hilo neno katika lugha yako ya asili. Kisha chapa picha ya neno, andika maana yake, au uitimiye katika msemo. La kwanza limefanyika kwa ajili yako.***

| Katika lugha yako | Katika kiingereza | Chapa picha ya neno, andika maana yake, au uitumiye katika msemo. |
|---|---|---|
| *fleti* | apartment |  |
| | bathroom | |
| | cost | |
| | furniture | |
| | home | |
| | house | |
| | landlord | |
| | lease | |
| | rent | |
| | room | |
| | safety | |
| | utilities | |

# 5 NYUMBA

Unapofika Marekani mara ya kwanza, unaweza kukaa na wandugu ambao tayari wamehamia Marekani. Au unaweza kuwekwa kwenye fleti, kwenye hoteli, au kwenye kituo cha shirika fulani cha kukaribisha watu. Kama hauna mke ama mme, unaweza kuwekwa, pamoja na wakimbizi wengine walio peke yao.



Amal anajitayarisha kwenda Marekani. Anawajuwa watu wawili huko. Mmoja ni bintiamu yake, na mwengine ni rafiki yake. Bintiamu anamuambiya Amal ya kwamba ataishi katika nyumba atakapofika mara ya kwanza Marekani. Lakini rafiki yake anasema ataishi katika fleti ndogo. Je, ni kwa nini  Amal anapata habari mbali mbali kutoka kwa watu wawili Marekani?

***Fikiri kuhusu nyumba au manyuma yako ya mwisho.***

- ❒ Nyumba yako ilikuwa namna gani?
- ❒ Nini ilifanya nyuma yako kuwa muhimu kwako?
- ❒ Kwa nini ulipaita nyumbani?

***Chapa picha ambayo ilifanya nyumba (manyumba) yako muhimu kwako.***

***Mweleze mwenzako kuhusu yale umechapa. Haya yatakuwa mazoezi kwa wakati utawaambiya watu utakaowakuta Marekani kuhusu nyumba au manyuma yako ya zamani.***



CAL COR Cultural Orientation Resource Center

## AINA YA MAKAZI

Mengi ya majamii za Marekani zina  aina mbalimbali ya makazi.

***Patanisha aina ya makazi na picha inayo stahili.****

1. Fleti

a. 

2. Nyumba ya jamaa ya kipekee

b. 

3. Nyumba za Trela

c. 

4. Chumba katika nyumba ama fleti

d. 

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 220.

**Shirika lako la makazi mapya ni wajibu wa kutoa fanicha ya msingi na vitu vya nyumbani.**

**Beyi ya makazi unatofautiana kutoka mji moja hadi mwingine.**

**Unapopanga nyumba lazima uweke sahihi kwenye makubaliano ya kupanga au mkataba wa kupanga.**

**Unapoweka sahihi kwenye mkataba wa kupanga nyumba, unakubali ku panga nyumba kwa myezi fulani na kulipa nyumba kwa wakati.**

Marekani ni jambo la kawaida kwa watu ku panga katika nyumba ama fleti. Kwa kawaida nyumba ama fleti ina jiko yenyi mafiga, sinki na friji, sebule na chumba cha kulia, chumba moja au zaidi ya bafu moja na kabati ya kuwekeya mavazi.

## VYOMBO

Shirika lako la makazi mapya ni wajibu wa kutoa fanicha ya msingi na vitu vya nyumbani katika nyumba ma fleti ambayo wamechagua kwako wewe na jamaa lako. Kati ya vitu kuna, funicha, vifaa vya bafu, vifaa vya jikoni na vitu vya huduma vyakimwili. Shirika hailazimishwe kukupa vitu vipya. Lazima vitu viwe na hali nzuri, lakini silazima viwe vipya.



Hadeel na jamaa lake walishangaa walipofika katika nyumba yao mpya wakikuta fanicha haikukuwa yenyi kufanana. Walijuwa yakuwa, fanicha haitakuwa mpya lakini kwanini vitu si vya kundi moja?

## BEYI YA MAKAZI

Beyi ya makazi inatofautiyana kutoka jimbo moja hadi jimbo linguine, kutoka mji mmoja hadi mji mwingine, na hata jamii katika eneo moja. Popote unapoishi, beyi za nyumba ni beyi kuu katika matumizi yako ya kila mwezi.



CAL COR Cultural Orientation Resource Center

# SURA YA TANO 5

***Fikiri kuhusu beyi ya nyumba nchini mwako au katika nchi yako ya ukimbizi.***

- ❒ Umewahi kutumia fedha kwa makazi?
- ❒ Kiasi gani ulitumia juu ya makazi?
- ❒ Ulilipa kwa ajili ya huduma kama vile maji, joto au umeme?
- ❒ Malipo gani nyingine ulikuwa nayo?

## MKATABA WA KUPANGA NYUMBA




Unapolipa fleti au nyumba Marekani, lazima uweke sahihi kwenye karatasi inayoitwa makubaliano ya kupanga au mkataba wa kupanga nyumba. Mkataba wa kupanga nyumba ni waraka wa sheria ambao inaeleza haki na majukumu za mpangaji wa nyumba (wewe) na mwenye nyumba anayepangisha.

Mkataba wa kupanga nyumba unaeleza kiasi gani inabidi ulipe fleti au nyumba kila mwezi. Kodi ya kupanga inaweza kuwa pamoja na beyi za kulipia nishati (umeme, mafuta ya kuiweka nyumba katika hali joto, maji, na undoaji wa takataka), au huduma inaweza kulipishwa mbali mbali. Kabla ya kuweka sahihi kwenye mkataba huo, ni muhimu kumwuliza mwenye nyumba kama beyi za nishati zitakuwemo katika kodi.

### MAJUKUMU ZA MPANGAJI

Unapoweka sahihi kwenye mkataba wa kupanga nyumba, unakubali mambo yafuatayo:

- ❒ Idadi ya watu watakaoishi kwenye fleti au nyumba.
- ❒ Malipo ya kila mwezi.
- ❒ Siku maalum ya mwezi ambayo itabidi nyumba ilipwe.
- ❒ Hali ya fleti (itabidi iwe safi na bila uharibifu wowote).
- ❒ Idadi ya myezi ambayo utakaa (kwa kawaida miezi 12).
- ❒ Masharti ya kuhamia pengine kabla muda wa mkataba wako kumalizika.


---

Durga ataenda Marekani kisha siku chache na ana wasiwasi kuhusu kitu moja. Anajuwa ya kwamba ataweka sahihi kwenyi mkataba wa kupanga nyumba atakapo panga fleti, na anajuwa hayo kutokana na darasa lake la mwelekeo wa kiutamaduni ya kuwa wakati wowote ana weka sahihi kwenye karatasi lazima aelewe maneno yote yanayo andikwa kwenye karatasi hayo. Lakini kuna maneno mengi sana kwenye mkataba wa kupanga nyumba. Namna gani anaweza kuelewa maneno yote? Nini unaweza eleza Durga kuhusu mkataba wa kupanga nyumba? Na, wapi anaweza kupata msaada kwa kuelewa mkataba wa kupanga nyumba?

---

**Usiondoe kamsa za moshi. Ziko hapo kwa kukulinda na moto wewe na wakazi wengine.**

## KUFUKUZWA



Kama unavunja makubaliano ya mkataba unaweza kufukuzwa ( kulazimishwa kutoka kwenye fleti yako). Kwa mfano, kama haulipi kodi ya nyumba au ukiharibu nyumba sana, unaweza kufukuzwa.

## MAJUKUMU YA MWENYE NYUMBA

Sheria za kukodisha nyumba zinawahusu wenye nyumba na wanaopanga nyumba. Lazima wenye nyumba wahakikishe kwamba fleti au nyumba wanayokodisha zinafuata matarajio ya usalama na hali ya usafi ya mahali panapokodishwa. Lazima mwenye nyumba ahakikishe kwamba umeme, mabomba ya maji, na mitambo ya moto yanafuata sheria, lazima aweke mitambo ya kuhadharisha watu moto ukitokea na ahakikishe ya kwamba eneo analopangisha alina panya wala vidudu. Sheria za nyumba pia zinasema kwamba mwenye nyumba hawezi kukataa kukodisha watu kwa sababu ya asili yao, dini yao au nchi wanayotokea.

---

Baada ya myezi michache katika fleti yake, Kyaw Oo alikuta kuna mende zinazo ishi humo na karibu na sinki yake. Fleti yake pia imekua chafu. Nani anajukumu za kukinga fleti safi? Nani anajukumu ya kuondoa mende? Nini Kyaw Oo anapaswa kumwomba mwenyi nyumba kama msaada?

---



***Fikiri kuhusu namna gani haki na majukumu za mwenyi nyumba na za mpangaji ni sawasawa au tofauti Marekani na uzoefu wako uliopita.***

- ❒ Je, umekwisha kukodi nyumba kabla ya sasa?
- ❒ Majukumu za mwenye nyumba zilikuwa gani?
- ❒ Wewe kama mpangaji, jukumu zako zilikuwa gani?
- ❒ Haki zako kama mpangaji ni zilikuwa gani?

## USALAMA NYUMBANI

Lazima ukinge nyumba yako salama.

***Patanisha ncha za usalama na picha inayo stahili hapa chini.****



1. Milango na dirisha



2. Wageni (Watu hujui)



3. Kamsa ya moshi



4. Kizima moto



5. Jiko

a. Usiondoe au kuzima kamsa za moshi katika nyumba yako. Zina piga kamsa kunapotokea moshi kwa kukujulisha ya kuwa kanaweza kuwakitu kyenyi kuungua nyumbani mwako.

b. Weka kitambaa na vitu vingine ambavyo vinaweza kupata moto mbali na jiko. Usiende mbali na jiko ama mafiga unapopiga.

c. Usiwaruhusu wageni nyumbani mwako. Kama mgeni anakuja nyumbani kwako, uwaulize wao ni wanani na wahitaji nini kabla ya kuwaacha waingie. Kama hauwezi kuzungumza nao na wanakusababisha kusikiya wasiwasi, silazima uwaitikie kuingia.

d. Funga mlango kila mara. Hata kama ukiwa nyumani, funga mlango na dirisha unapotoka.

e. Tumiya kizima moto kwa kuzima moto ndogo nyumbani mwako ambayo inaweza kutokea. (kwa mfano, wakati wa kupika). Usitumiye maji kwa kuzima moto ya mafuta. Kuhusu moto kubwa, toka kwenye ujengo mara moja na ita huduma za dharura ukipiga 9-1-1. (Angalia sura ya 6 ya kujifunza zaidi kuhusu kupiga simu ya 9-1-1).

***Chapa duara kwa hatua za usalama zinazo pendekezwa hapa juu ambazo ulizojifunza sikuzilizo pita. Ambiya mwenzako jinsi ulijifunza hatua hizi. Kisha tambulisha hizo ambazo ni zipya kwako.***

---

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 220.

**Weka chakula ikifunikwa na kwenye friji. Ukiacha chakula wazi inaweza kuleta vidudu na panya.**

## MATENGENEZO YA MAKAZI

Ni muhimu nyumba yako iwe safi na katika hali nzuri.

❒ Funika chakula na uiweke kwenye friji. Kuacha chakula bilakuifunika nje, kwenye jiko inaweza kuvuta vidudu au panya.



❒ Weka takataka yote kwenye kopo ya takataka kila siku. Ikifungwa kwenye mfuko ya plastiki. Tupa takataka yako katika shimo la takataka nje kila siku ikiwezekana. Takataka nyumbani mwako inaweza kuvuta vidudu, mende, au panya.



❒ Jikoni, usiweke kombe ya mayayi, mifupa, au maganda ya matunda au mboga chini ya sinki wala utupaji wa uchafu. Usiweke vitu kama vile nywele chini ya sinki ya bafu au kitoa maji au choo. Tupa vitu hivi kwenye kikombe cha takataka.



❒ Usiweke vitu (kama vile vitu za usafishaji wala nepi) kwenye choo ingine kama siyo karatasi ya choo. Uwafundishe watoto wako kusito mwanga kitu chochote lakini karatasi ya choo tuu.



❒ Funga mlango wa bafu vizuri kabisa, kuweka mapazia ya kuoga vizuri ndani ya baseni, na tumia mkeka ya bafu juu ya sakafu nje kisha kuoga.



❒ Wakati kigunduzi ya moshi inaanza mlio kama hakuna moshi, hiyo ina maanisha kuwa inaitaji betri mpya. Badilisha betri mara moja. Kumbuka ku hakikisha kwamba kigunduzi ya moshi ni daima yenye kuwaka na inatumika.



# SURA YA TANO 5

Wakati Taw Meh anarudi nyumbani kutoka kazini, kuna arufu mbaya inayotokea jikoni. Ni baadhi ya vitu gani ni lazima kuangalia kuona wapi arufu inatokea? Ni baadhi ya vitu gani Taw Meh anaweza kufanya ili asiwe na harufu mbaya jikoni mwake kwa siku zijazo?

***Namna gani nyumba yako ya Marekani inaweza kuwa sawa au tofauti na nyumba yako ya zamani? Andika kuhusu hayo au chapa picha au maji inaonyesha mfanano na tofauti katika kasha zilizo hapa chini – Kwa mfano, idadi na aina ya vyumba, aina ya bafu, mwanguko wa maji au maji ya moto, na namna ya kusafisha.***

| YANAYOFANANA | TOFAUTI |
|---|---|
| | |

***Unafikiri ya kwamba yanayofanana na/au tofauti zitafanya kuwa marekebisho rahisi au ngume zaidi?***

***Pamoja na mtu mwengine cheza-jukumu ya mpangaji anazungumza na mwenye nyumba ili ujuwe yale utahitaji kujuwa kuhusu nyumba yako mapya. Unaweza kuuliza:***

- ❐ Kodi ya kulipa nyumba ni kiasi gani?
- ❐ Siku maalum ambayo lazima kulipa nyumba?
- ❐ Huduma ziko ndani ya kodi ya kulipa nyumba?
- ❐ Ikiwa kuna tatizo fulani, ni nani ndiye nitaita?
- ❐ Kodi ni ya myenzi mingapi?

***Tafadhali kuja na maswali yako mwenyewe!***

## KAMILISHA*

***Chagua jibu bora zaidi kwa maswali hapa chini ukifanya chaguo bora.***
***Hii ni mfano:***

*Lugha gani ndio inazungumzwa na watu wengi zaidi Marekani?*

a. Kichina.

(b.) Kiingereza.

c. Kigerumani.

***Watu wengi Marekani wanazungumza Kiingereza. Kwa hiyo, Jibu ni b. Kiingereza.***

1. Ni gani kati ya hatua zifwatazo inaweza kuleta vidudu au panya ndani ya nyumba yako?

   a. Kuacha chakula wazi juu ya jiko.

   b. Kuweka chakula kwenye friji.

   c. Kuacha takataka ya jikoni kwasiku nyingi.

   d. Chaguo a na c.

2. Kama unapanga katika nyumba ama fleti Marekani, ni lazima uweke sahihi yako kwenye kodi ama mkataba wa kukodisha?

   a. Ndiyo.

   b. Hapana.

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 220.

3. Nini unapaswa fanya kama mgeni usiyemjua mlangoni kwako?

    a. Kufungua mlango na kuwaacha waingiye.

    b. kuwauliza wao ni wanani na wanahitaji nini, ikiwa unazungumza kiingereza kidogo.

    c. Usiwa ache kuingiya nyumbani ikiwa wanakusababisha kusikiya wasiwasi.

    d. Chaguo b na c.

4. Unapotia sahihi yako kwenye mkataba wa kupanga nyumba, unakubali nini?

    a. Kiasi cha kodi cha kila mwezi.

    b. Idadi ya mwezi utakaa.

    c. Idadi ya watu ambao wataishi katika nyumba au fleti.

    d. Yote ya juu.

5. Shirika lako la makazi mapya linalazimishwa kukupa vitu vipya?

    a. Ndiyo.

    b. Hapana.

# 6



# Sura Ya Sita
## HUDUMA ZA JAMII

Pamoja na shirika lako la makazi mapya, kuna mashirika mengine ya huduma katika jamii yako. Huduma na upatikanaji wao utatofautiyana kulingana na nafasi.

### Sura Hii Itajadili

» Misaada za serikali
» Misaada za mashirika binafsi
» Misaada za umma



## MANENO MUHIMO YA KIINGEREZA

Maneno ya Kiingereza yafuatayo hutumiwa wakati wa kuzungumza kuhusu makazi mapya nchini Marekani. Maneno haya itakuwa na mafaa kwako kuyajifunza.

***Sema neno katika kiingereza. Andika hilo neno katika lugha yako ya asili. Kisha chapa picha ya neno, andika maana yake, au uitumiye katika msemo. La kwanza limefanyika kwa ajili yako.***

| Katika lugha yako | Katika kiingereza | Chapa picha ya neno, andika maana yake, au uitumiye katika msemo. |
|---|---|---|
| *ulinzi wa watoto* | child care | *Fatimah anatafuta nafasi ya uangalifu ya watotot ili aweze kuenda kwa shule la Kiingereza kama lugha ya pili.* |
| | community | |
| | emergency | |
| | library | |
| | parks | |
| | public | |
| | recreation | |
| | translation | |

**Mashirika ya serikali ya huduma za jamii zinasaidiya watu wenyi mahitaji maalum.**

**Serikali inatoa msaada wa chakula kulingana na ukubwa na mapato ya jamaa kwa jamaa yenye pato ya chini.**

***Fikiri kuhusu aina za misaada ungepata nchini mwako ama nchi yako ya ukimbizi.***

## MSAADA WA SERIKALI

Mashirika ya serikali ya huduma za jamii zinatoa huduma mbali mbali. Mashirika haya yana saidia watu wenye mahitaji maalum, kama jamaa zenye pato ndogo, wasio na mahali pa kukaa, na walemavu. Programu za serikali zimeweka muda fulani unaobidi kufuatwa na miongozo inayoeleza namna wakimbizi wanaweza kushiriki kwenye programu hizi. Jamii zinatofautiana katika aina na kiasi cha huduma wanazopana. Programu zifuatazo ni programu mbalimbali za serikali zinazosaidia makimbizi.



**PROGRAMU ZA MSAADA WA FEDHA**. Kwa watu wenye shida kwa kupata kazi, programu mbili zinatoa msaada wa fedha kwa muda. Msaada wa muda kwa jamaa zenye mahitaji (Temporary Assistance to Needy Families "TANF") kwa wazazi wenye watoto, na msaada wa pesa (Refugee Cash Assistance "RCA") kwa wakimbizi ambao wako peke yao na wakimbizi walio owa wala kuolea ambao hawana watoto.



**PROGRAMU ZA MSAADA WA KUSAWANISHA (MATCHING GRANT PROGRAM).** Mashirika mengi ya makazi mapya yanatoa programu hii badala ya kutoa misaada ya fedha kwa wale wakimbizi wanaotaka kufanya kazi lakini wanahitaji msaada wa fedha kwanza. Wakimbizi wanaojiandikisha kwa programu hii wanaahidi kupata kazi haraka iwezekanavyo. Kwa kuahidi hivyo wanapata msaada wa fedha na ushauri kwa kupata kazi, na huduma zitakazowasaidia kupata kazi katika miezi 4 mpaka 6 ya kwanza baada ya kufika Marekani.



**PROGRAMU ZA MSAADA YA ZAIDI KWA CHAKULA (SNAP).** Programu huu wa shirikisho unatoa misaada ya kifedha kwa watu wenyi pato ya chini Marekani kwa kununua chakula. Mtu aliye katika programu hii anapewa kadi ambayo inaweza kutumika kununua kiasi fulani cha chakula kila mwezi. Wakimbizi wanaweza kuomba msaada wa chakula katika ofisi za serikali za mitaa. Kiasi cha msaada kinalingana na ukubwa na pato ya jamaa.



**PATO LA ZIADA KWA WELEMAVU (SUPPLEMENTAL SECURITY INCOME "SSI").** Hii ni programu ya serikali kuu ya nchi ya msaada wa fedha kwa vipofu, walemavu, au wenye umri zaidi ya miaka 65, au wenyi pato ya chini au hawana pato yoyote.

**PROGRAMU ZA HUDUMA ZA UTUNZAJI WA WATOTO.** Baadhi ya jamii zinatoa huduma za kutunza watoto kwa bure au kwa malipo ya chini kwa watu wenye pato ndogo ili waweze kwenda kazini au waweze kutafuta kazi. (Angalia sura ya 12 kwa habari zaidi juu ya programu za huduma za utunzaji wa watoto)

---

Abbas anaamini atapata msaada wa serikali wakati atahamia Marekani. Wakati anakutana meneja wa kesi yake katika uwanja wa ndege, anatarajia meneja wa kesi amupe fedha au cheki, lakini hapati chochote. Kwa nini hii haitokei? Katika tokeo gani unaweza kupata misaada wa serikali?

---

## MSAADA WA MASHIRIKA BINAFSI

Mashirika binafsi yanatoa pia misaada ambazo zinawasaidia wakimbizi. Idadi na aina ya huduma hizi kutofautiana kutoka sehemu moja hadi sehemu nyingine, lakini jamii nyingi yanatoa huduma zifuatazo:

- ❐ Ushauri.
- ❐ Msaada kwa hali yako ya uhamiaji.
- ❐ Madarasa ya Kiingereza.
- ❐ Msaada wa kutafuta ajira (ushauri kuhusu kupata kazi na ushauri juu ya mafunzo ya kazi).
- ❐ Huduma za kutafsiri.

---

Gopi anajuwa ya kuwa anahitaji kuanza kujifunza kiingereza. Yeye amegundua ya kuwa shirika lake la makazi mapya halitoi lugha ya kiingereza, lakini shirika lake litamsaidia kupata darasa mahali fulani katika jamii. Wapi Gopi anaweza kuchukua madarasa?

---

**Makundi ya kidini yanaweza kutoa misaada. Wakimbizi hawalazimishwi kushiriki katika shuguli za kundi za kidini kwa kupokea huduma.**

**Kuna aina tatu ya huduma za dharura nchini Marekani: idara ya moto, polisi, na gari la wagonjwa au ambulensi.**

Aina mbili ya kawaida ya mashirika ya misaada binafsi ni mashirika ya kijamii na mashirika ya kidini.

## MASHIRIKA ZA KIJAMII (COMMUNITY BASED ORGANIZATIONS–CBOs)



Mashirika haya yanafanya kazi katika jamii na kutoa burudani, kijamii, na huduma za kielimu kwa wanajamii. "CBO" moja unaweza kupata katika jamii yako ni mashirika ya kijamii ya kikabila (ethnic community-based organizations "ECBOs"). Haya ni mashirika yaliyoundwa na wakimbizi wa zamani kwa madhumuni ya kusaidia wakimbizi na wahamiaji wapya katika jamii zao. Baadhi yanatoa madarasa ya elimu kwa watu wazima, yanaandaa vikundi vya wanawake,na kushikilia matukio ya kiutamaduni na burudani.

## TAASISI ZA KIDINI



Makanisa, masikiti, na mahekalu yanaweza kutoa huduma tofauti. Baadhi ya taasisi hizi, huwa na madarasa ya Kiingereza kama lugha ya pili kwa watu wazima au kama shule za jioni (baada ya shule) kwa wanafunzi wa shule, na baadhi hutoa nguo za zamani na vyombo vya nyumbani. Hakuna yeyote anaye tumia huduma hizi analazimishwa kushiriki katika shuguli za kidini za kundi. Nchini Marekani, una uhuru wa kuabudu katika njia unayochagua, ama kutoabudu tu.

Kanisa la kikristo linajitolea kumpa Zaw Min na jamaa lake sanduku ya chakula kwa bure kila wiki. Zaw Min na Jamaa lake wanahitaji chakula, lakini si wakristu na hawataki kuwa waKristo. Lazima Zaw Min aitike chakula? Kwa nini ndiyo ama hapana?

## HUDUMA ZA UMMA ZA KIJAMII

Kila jamii ina huduma za umma zinazoweza kutumiwa na watu wote wa jamii. Lazima ujuwe kuhusu huduma hizi ili uweze kufaidika nazo. Huduma zifuatazo ni baadi ya huduma muhimu za umma:

**HUDUMA ZA HALI YA DHARURA NA KUITA 9-1-1.** Jamii zote zina idara za kuzima moto na huduma za magonjwa ya ghafula. Kupata msaada wakati ya dharura, piga simu 911 na opereta atajibu. Ni lazima uwe tayari kumwambia operetta unachohitaji "Police" (Polisi), "Fire" (moto), au "Ambulance" (Ambulensi). na pia mahali ulipo. Kama hauwezi kueleza tatizo lako kwa kiingereza, sema "Help" (msaada) au "Emergency" (hali ya hatari) na usikate simu. Kubaki kwenye simu kutamsaidia operetta kujua mahali ulipo.

Gori Maya aliwasha mushumaa na ilianguka nchini, nakuwasha moto kwenye sakafu. Yeye hazungumzi kiingereza bado, lakini anakumbuka kuita 9-1-1. Wakati opereta anajibu, Gori Maya anasema, "No English. Fire." Kwa nini ni muhimu kwake kusema "fire moto"? Nini ingine lazima Gori Maya angekumbuka kufanya?

Kuna aina tatu kuu za huduma za dharura nchini Marekani.

***Chapa mustari kutoka jina la idara mpaka kwenye picha ya gari ambayo inatumiwa.**** 

1. 


2. 

3. 

a. Fidara ya kuzima moto

b. Polisi

c. Ambulensi

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 220.

**Wapolisi wanalinda na pia wanasaidia watu. Unapaswa kufanya ambacho wanakuomba ufanye na usiwe na hofu.**

***Amua kama tukio hizi hapa chini ni dharura. Ikiwa ni hayo, amua huduma gani ya dharura italazimishwa.****

| Hii ni hali ya dharura?** | Ndiyo, ita 911 | | | Hapana, usiite 911 |
|---|---|---|---|---|
| | Moto | Polisi | Ambulensi | |
| 1. Unaamka katikati ya usiku na unaona moto nyuma ngambo ingine ya barabara.  | | | | |
| 2. Mtoto wa jirani wa miaka nane anachukua mpira ya mtoto wako.  | | | | |
| 3. Binti yako anaanguka juu ya mti na anamaumivu sana.  | | | | |
| 4. Kengele ya moto inafanya fujo, lakini kisha kuangalia nyumbani mwako, unaona hakuna moto.  | | | | |
| 5. Unamwona mtu usiye mujuwa akitafuta kuingiya kwa kingufu kwenye nyumba ya jirani yako ambaye haiko nyumbani.  | | | | |
| 6. Kwa bahati mbaya unajikata kidole unapokata mboga na kuweka bendeji kwa kusimamisha damu.  | | | | |

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 220.

** Wazo kwa ajili ya shuguli hii ilitokea kwenye kitabu cha wanafunzi wa Mwelekezo wa kiutamaduni wa Marekani iliyotengenezwa na kituo cha usaidizi wa Shirika la makazi mapya katika Asia ya mashariki (International Rescue Committee).



**POLISI**. Maafisa wa polisi ni watumishi wa umma ambao wanalinda watu nakuwasaidia. Unapaswa kufanya ambacho maafisa wa mapolisi wanakuomba ufanye na usiwaogope. Kama afisa wa polisi anakusogelea na anakuomba usimame, usikimbie. Kukimbia inaweza kuonekana kama umefanya kitu kibaya na inaweza kusababisha matatizo. Kama huwezi kuwasiliana na polisi, omba mkalimani ama ujulishe shirika lako la makazi mapya.

---

Tee Reh anakwenda kwenye duka na anavuka katikati ya njia. Kisha anaona nafasi nyingine pa kuvukia ambayo angeli tumia. Afisa wa polisi anaanza kutembeya kuelekea Tee Reh, halafu Tee Reh anakimbia. Polisi anamufwata Tee Reh kumukamata. Anampa Tee Reh tiketi kwa sababu yakuvukia mahali isiyo ruhusiwa na malipizi kwa kukimbia. Vitu gani viwili ambavyo Tee Reh angelipaswa fanya? Nini unaweza kumweleza Tee Reh kuhusu polisi nchini Marekani?

---




**MAKTABA**. Maktaba za umma zina vitabu na vifaa vingine, kama vile CD na DVD, ambazo wakazi wanaweza kukopa bure ama kubadilisha. Lazima kuomba kadi ya maktaba iliuweze kuchukua vifaa nje ya maktaba. Maktaba mara nyingi unatoa madarasa kama vile kiingereza au kuandika, na inaweza kuwa na kompyuta kwa matumizi ya umma.



**BUSTANI YA MAPUMZIKO NA BURUDANI**. Bustani za mapumziko zinatoa nafasi yakuji furahisha, viwanja vya watoto kuchezea, na kufanya michezo ya riadha kwa watu. Bustani nyingi zina kanuni zinazohusu aina ya shuguli zinazoruhusiwa. Baadhi ya bustani hizi ni bure lakini nyingine zina ada ya kiingilio.

---

Amina anaishi katika ujengo na hakuna nafasi yakuchezea kwa watoto wake. Anajuwa ya kwamba hawezi kuacha watoto wake kucheza njiani. Wapi watoto wake wangeweza kuchezea?

---

***Linganisha huduma inayopatika Marekani na yale yaliyo nchini mwako au nchi yako ya ukimbizi.***

- ❐ Huduma gani ni sawa?
- ❐ Huduma gani ni tofauti?

***Chora au andika kuhusa kufanana na tofauti hapa chini.***

## KAMILISHA*

***Chagua jibu bora zaidi kwa maswali hapa chini ukifanya chaguo bora.***
***Hii ni mfano:***

*Lugha gani ndio inazungumzwa na watu wengi zaidi Marekani?*

a. Kichina.

(b.) Kiingereza.

c. Kigerumani.

***Watu wengi Marekani wanazungumza Kiingereza. Kwa hiyo, Jibu ni b. Kiingereza.***

1. Kundi gani hapa chini inafanya huduma za serikali hapana msaada?

   a. Watu/jamaa wenyi kipato cha chini.

   b. Watu wenye ulemavu.

   c. Wasio kuwa na pakukaa.

   d. Matajiri.

2. Uliwasili nchini Marekani wakati moja na jirani yako. Unaishi katika ujengo moja, lakini unatambua ya kwamba jamaa lake la watu 5 inapata msaada ya fedha zaidi kutoka serikali kuliko jamaa lako la watu 3. Je, serikali ilifanya makosa?

   a. Ndiyo.

   b. Hapana, kwasababu huduma za serikali za kijamii zinatofautiana kulingana na ukubwa wa jamaa na mabo mengine.

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 220.

3. Kama una hudhuria madarasa ya kiingereza katika taasisi za kidini, lazima ujiunge na dini hii ili uendeleye kuhudhuria madarasa.

    a. Kweli.

    b. Uongo.

4. Namna gani Wamarekani wengi wanaji sikiya au wanajibu wakati wanaona afisa wa polisi?

    a. Wanahisi salama na kulindwa.

    b. Wana hofu.

    c. Wanawatusi afisa wa polisi.

    d. Wana kimbiya mbali.

5. Maktaba ya umma ni nafasi ambapo unaweza kukopa vitabu, CD za muziki, na DVD kwa bure?

    a. Ndio.

    b. Hapana.



7

# Sura Ya Saba
## USAFIRI

Unapofika mara ya kwanza nchini Marekani, labda utatumia muda mwingi kutembea kwa maeneo unahitaji kwenda. Hivi karibuni utaanza kuchukua usafiri wa umma. Usafiri wa umma unatafautiana sana kutokana na mahali moja na pengine. Katika baadhi ya maeneo mengine, usafiri wa umma unaweza kukupeleka popote unataka kwenda. Katika maeneo mengine, usafiri wa umma haupatikani sana au halipo. Shirika lako la makazi mapya litakutolea taarifa kuhusu usafiri wa umma katika jamii yako mpya hivi ukishafika.

### Sura Hii Itajadili

» Aina za usafiri wa umma
» Taa zinazo ongoza magari na usalama barabarani
» Kuwa na gari na kuendesha gari

**Usafiri wa umma inatofautiana kutokana na jamii kwa jamii. Ina weza kuwa kubwa katika inaweza kutokuwa mahali, na inaweza kutopatikana sana pengine.**

## MANENO MUHIMU YA KIINGEREZA

Maneno ya Kiingereza yafuatayo hutumiwa wakati wa kuzungumza kuhusu makazi mapya nchini Marekani. Maneno haya itakuwa na mafaa kwako kuyajifunza.

***Sema neno katika kiingereza. Andika neno katika lugha yako ya asili. Kisha chapa picha ya neno hilo, andika maana yake, au uitimiye katika msemo. La kwanza limefanyika kwa ajili yako.***

| Katika lugha yako | Katika kiingereza | Chapa picha ya neno, andika maana yayo, au uitumiye katika msemo. |
|---|---|---|
| *baisikeli* | bicycle |  |
| | bus | |
| | car | |
| | driver's license | |
| | road | |
| | street | |
| | traffic light | |
| | transportation | |

**Mara nyingi utalazimishwa kununua tiketi kwa kutumia usafiri wa umma.**

## AINA ZA USAFIRI WA UMMA

Usafiri wa umma unaruhusu watu katika mji, kusafiri katika mji bila gari. Nchini Marekani, kuna aina tatu kuu ya usafiri wa umma mabasi, gari la moshi, na treni ya abiria. Zinatembea kulingana na wakati uliopangwa na kwa kawaida zinasimama kwa maeneo fulani kwa kuwaruhusu wasafiri kuingia na kutoka. Mara nyingi utalazimishwa kununua tiketi kwa kutumia usafiri wa umma. Teksi pia inaweza kupatikana, lakini ni beyi ghali kwa kawaida.









***Fikiri kuhusu jinsi ulitembea nchini mwako au nchi yako ya ukimbizi.***

- ❒ Ulitembea, ulitumia baisikeli, au ulitumia usafiri nyingine?
- ❒ Kama unatumia usafiri nyingine, ulikuwa wa umma wala wa pekee?
- ❒ Namna gani ulipata gari yako?

*Chapa au andika kuhusu njia ambazo ulitumia kwaku tembea mjini au katika nchi yako ya ukimbizi katika duara iliyo hapa chini*

**Namna gani ulienda sokoni?**

**Namna gani ulimtembelea rafiki?**

**Namna gani ulitembelea jamaa?**

**Namna gani ulienda kazini?**

**Namna gani ulisafiri mbali?**

**Uwe na ufahamu wa alama na ishara za barabarani ili uwe salama wakati unatembea katika jamii yako.**

Inaweza kuwa vigumu mara ya kwanza, lakini kama unachukua muda, utaweza kujuwa mfumo wa usafiri. Pia, lazima ujuwe ya kwamba katika baadhi ya maeneo fulani unweza lazimishwa kusafiri kwa masaa mengi au zaidi ya mfumo moja wa usafiri wa umma kutoka sehemu moja hadi nyingine.

***Kujua namna gani kutembea mjini katika mji mpya unachukua muda, kwa hivyo usijisikii vibaya. Siku mojautajua njia yako mjini!***




## ALAMA ZA BARABARANI NA USALAMA BARABARANI

Unapotumia usafiri wa umma na kutembea njiani katika jamii, utatambua alama na ishara za barabarani nyingi. Sheria hizi za barabarani na na nyingine zinasaidia kuwakinga watu wanapotembea na kuendesha gari.

***Patanisha alama na sheria inayoeleza.*** *

1. 

2. 

3. 

4. 

5. 

a. Alama hii inaonesha mahali ya kuvuka barabara. Uvuke daima barabara kwa mahali pa kuvuka.

b. Hii inamaanisha "Kusimama" ("Stop"). Si salama kuvuka.

c. Hii inamaanisha "Kutembea" ("Walk"). Ni salama kuvuka.

d. Mataifa mengi yanalazimisha watoto kuvaa kofia ya baiskeli wakati wanaendesha baiskeli.

e. Wakati unaendesha gari lazima kuvaa mkanda wa usalama. Mataifa yote yanalazimisha viti vya usalama kwa watoto.

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 221.

**Ni bei ghali ku nunua na kutembeza gari. Jaribu kutumia usafiri wa umma.**

**Kuendesha gari wakati ukiwa katika hali ya ulevi ni kuvunja sheria sana. Unaweza kupoteza leseni yako ya gari, kulipa faini kubwa au kufugwa.**

***Fikiri kuhusu usalama barabarani uliyofanya kwa mazoezi, na marekebisho unaweza kuhitaji ili uwe salama zaidi Marekani.***

- ❒ Jinsi gani ilifanya mazoezi ya usalama barabarani?
- ❒ Jinsi gani ulibaki salama njiani?
- ❒ Unafikiri nini itakuwa tofauti kuhusu usalama barabarani Marekani? Kwa nini?

***Kama hujuwi mahali unapoenda, simama na uulize njia. Fanya mazoezi ya kuuliza na mwengine. Hapa kuna baadhi ya maswali unaweza kuuliza:***

- ❒ Jinsi gani naenda sokoni kutoka hapa?
- ❒ Kituo cha basi cha karibu zaidi kiko wapi?
- ❒ Hii basi inaenda sokoni?
- ❒ Kunako ofisi ya posta karibu?

***Towa maswali yako mwenyewe!***

## KUWA NA GARI NA KUENDESHA GARI



Unaweza kuanza kuendesha gari hapo hapo unapofika Marekani, lakini kuna majukumu na malipo kwa kuwa na gari. Jaribu kutumia usafiri wa umma mpaka upate kazi na pesa ya kununua gari.

---

Henri anatembeza gari tangu miaka mingi kabla yakuasili nchini Marekani. Miezi michache baada ya kuasili, alinunua gari ya zamani. Siku moja gari lingine liligonga gari lake kutoka nyuma. Ajali haikukuwa kosa ya Henri, lakini alikuwa na matatizo mengi kwani alikuwa akitembeza gari bila leseni au bima. Ilikuwa muhimu Henri akumbuke nini kuhusu kutembeza gari Marekani?

---

## LESENI YA KUTEMBEZA



Utakapo kuwa tayari kuanza kuendesha gari, jambo la kwanza utahitaji ni leseni ya mji. Kabla ya kupata leseni yako, lazima upimwe macho, ufanye mtihani wa kuandika, na mtihani wa kuendesha gari. Ukikamatwa ukitembeza bila leseni inayo faa, unaweza kulipa faini, na inaweza kuwa vigumu kwako kupata leseni siku za karibuni. Kisha kupata leseni yako, lazima uheshimu sheria za kuendesha. Ukivunja sheria, unaweza kupoteza leseni yako. Kwa mfano, ukikamatwa unaendesha gari ukiwa katika hali ya ulevi, unaweza kupoteza leseni yako, unaweza pia kulipa faini kubwa, au kupelekwa jela.

## BEI YA KUWA NA GARI



Kuna bei nyingi kwa kuwa na gari. Mbele ya yote, taifa nyigi zinalazimisha mtu awe na bima ya gari. Na bima ya gari, unalipa mara kwa mara kwa kampuni ya bima. Kama una ajali na mtu anaumia au mali inaharibiwa, kampuni ya bima inalipa malipo ya matibabu au ya kutengenezesha gari. Bima ni kwa kawaida bei ghali zaidi kwa watu wasiokuwa na rekodi ya kuendesha gari nchini Marekani. Aina ya gari, umri wako, na idadi ya watu ambao watakuwa wakitembeza gari yako pia itasababisha beyi ya bima. Kuna malipo nyingine wakati una gari na kuiendesha—petroli au mafuta, maegesho, kodi, karatasi za gari, na matengenezo ya gari.

***Fikiri kuhusu tofauti kati ya kutumia usafiri wa umma na kuwa na gari Marekani.***

- ❒ Faida ya kutumia usafiri wa umma badala ya kuwa na gari ni gani?
- ❒ Namna gani haki na majukumu za kuwa na gari na kuendesha gari Marekani zinatofautiyana na haki na majukumu nchini mwako au nchi yako ya ukimbizi?

---

Yin Nyo amechoka na kupoteza pesa nyingi kwa kuchukua basi kwa kwenda na kutoka kazini kila siku. Anahitaji kununua gari. Ni wazo nzuri? Nini unaweza kuenleza Yin Nyo kuhusu tofauti kati ya kutumia usafiri wa umma na kuwa na gari nchini Marekani?

---

## KAMILISHA*

***Chagua jibu bora zaidi kwa maswali hapa chini ukifanya chaguo bora.***
***Hii ni mfano:***

*Lugha gani ndio inazungumzwa na watu wengi zaidi Marekani?*

a. Kichina.

(b.) Kiingereza.

c. Kiugerumani.

***Watu wengi Marekani wanazungumza kiingereza. Kwa hiyo jibu ni b. Kiingereza.***

1. Gani ya aina zifwatazo ni aina ya usafiri wa umma?

   a. Mabasi ya mji.

   b. Magari ya moshi.

   c. Gari ya rafiki yako.

   d. Treni ya abiria.

   e. Chaguo a, b, na d.

2. Nchini Marekani, unahitaji leseni ya dereva kwa kuendesha gari.

   a. Ndiyo.

   b. Hapana.

---

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 221.

3. Kama unakamatwa ukitembeza gari katika hali ya ulezi, nini kati ya zifuatazo inaweza kutokea?

    a. Utapoteza leseni yako ya kutembeza kwa muda fulani.

    b. Utalipa faini kubwa.

    c. Utaenda katika jela.

    d. Moja au yote hapa juu.

4. Nchi nyingi zinalazimisha gari kuwa na bima.

    a. Ndiyo.

    b. Hapana.

5. Katika malipo ya kuwa na gari kuna gani zifuatazo?

    a. Biama ya gari.

    b. Karatasi za gari.

    c. Petroli.

    d. Matengezo ya gari.

    e. Yote hapa juu.



8

# Sura Ya Nane
## HUDUMA ZA AFYA

Mfumo wa huduma za afya nchini Marekani ni ngumu na mara nyingi bei ghali. Inaweza kuwa vigumu mara ya kwanza kuelewa mfumo wa huduma za afya ya Marekani, lakini kwa uvumilivu na muda utaanza kujifunza kuhusu hayo. Kumbuka yakuwa wafanyakazi wa shirika lako la makazi mapya wanaweza kukusaidia kujibu maswali yako na kukutolea maelezo zaidi kama unayahitaji.

### Sura Hii Itajadili

- Uchunguzi wa afya yako wa awali
- Watoa huduma za afya
- Kulipa huduma za afya
- Mafikiri kuhusu afya Marekani

**Mfumo wa huduma za afya nchini Marekani ni ngumu na mara nyingi bei ghali.**

## MANENO MUHIMU YA KIINGEREZA

Maneno ya Kiingereza yafuatayo hutumiwa wakati wa kuzungumza kuhusu huduma wa afya nchini Marekani. Maneno haya itakuwa na mafaa kwako kuyajifunza.

***Sema neno au msemo katika kiingereza. Andika neno katika lugha yako ya asili. Kisha chapa picha ya neno ama msemo, andika maana yake, au uitimiye katika msemo. La kwanza limefanyika kwa ajili yako.***


| Katika Lugha yako | Katika Kiingereza | Chapa picha ya neno, andika maana yayo, au uitumiye katika msemo. |
|---|---|---|
| *daktari wa meno* | dentist | *Daktari wa meno ni daktari ambaye anatunza matatizo ya meno na kinywa.* |
| | doctor | |
| | doctor's office | |
| | health | |
| | hospital | |
| | immunization | |
| | insurance | |
| | interpreter | |
| | medicine | |
| | nurse | |
| | sick | |

**Umjulishe daktari kama una matatizo yoyote ya afya ili uweze kutunzwa haraka.**

**Kuna aina mbalimbali ya watoa huduma za afya nchini Marekani.**

## UCHUNGUZI WA AFYA WA AWALI

Kukutana kwako na huduma za afya za Marekani mara ya kwanza labda itakuwa mara ya kwanza ya uchunguzi wa afya yako. Shirika lako la makazi mapya litakupangia uchunguzi huu mara baada ya kufika Marekani. Uchunguzi utatambua na kutibu matatizo yoyote ya kiafya ambayo yanaweza kuingilia shuguli za makazi yako mapya, kama vile uwezo wako wa kufanya kazi au uwezo wa watoto wako kuandikwa kwenye shule. Watoto wako watapata chanjo ya kukinga wakati wa ukaguzi kwa sababu watoto wote wanaojiandikisha kwenye shule za umma lazima waonyeshe ushahidi wa kuchanjwa.



Ni muhimu sana kumweleza daktari kama una matatizo yoyote ya afya au ugonjwa ili uweze kutunzwa kwa haraka mara moja. Huduma ya afya kubwa inaweza kutopatikana katika wiki zako za kwanza za kufika kwako, isipokuwa unahitaji huduma ya haraka.



***Fikiri kuhusu masuala yoyote ya afya ambayo unaweza kuhitaji kumueleza daktari wako.***

# SURA YA NANE 8

Kisha ukaguzi wa kwanza wa afya, utahitaji kuelewa namna gani mtapata huduma za afya wewe na ndugu katika jamaa yako mtakapoihitaji. Wafanyakazi wa shirika la makazi mapya watakusaidia kutokana na maoni yako.

***Fikiri kuhusu namna gani ulishughulika na matatizo ya afya katika siku zilizo pita.***

- ❒ Wakati ulijisikia mgonjwa, ulifanya nini?
- ❒ Wakati ulijiumiza, ulifanya nini?
- ❒ Wakati gani ulienda kwa daktari?

## WATOAJI HUDUMA ZA AFYA

Marekani kuna aina mbalimbali za watoaji huduma za afya. Hapa kuna baadhi ya watoa huduma za afya za kawaida:




**IDARA YA AFYA YA UMMA.** Idara za afya ya jamii zinatoa chanjo za kukinga magonjwa na zinatoa huduma nyingi za afya za kuepuka magonjwa, zikiwemo kufanya ukaguzi na kutunza magonjwa ya kifua kikuu. Huduma za ukingo wa afya ni huduma ambazo zinazo kinga na magonjwa kabla ya kutokea. Kwa wakimbizi, huduma hizi ni bure au si bei ghali sana. Miadi ni muhimu kwa kawaida. (ujifunze zaidi kuhusu bima ya afya katika sura hii, katika sehemu iitwayo "Bima ya Afya.")



**KLINIKI ZA JAMII NA VITUO VYA AFYA.** Kliniki za jamii na vituo vya hutoa huduma za afya za lazima na pia hutoa ushauri wa afya. Pia Kliniki zingine hutoa huduma za meno na ukaguzi wa macho. Kliniki zingine katika miji zina tunza aina fulani za magojwa, kama wanawake waja wazito au watu wenye ukimwi. Unaweza kuhitaji au kutohitaji miadi katika kliniki ya jamii au kituo cha afya. Kliniki zinakubali bima binafsi na msaada wa serikali wa afya "Medicaid", (bima ya serikali kwa watu wenye pato ndogo) na kliniki nyingi zinalipisha kulingana na uwezo wa kulipa wa mgonjwa.



**MADAKTARI BINAFSI.** Kuna aina mbili kuu za madaktari nchini Marekani: madaktari wa magonjwa mbalimbali, na madaktari wataalamu. Madaktari wa magonjwa mbalimbali wanatoa huduma za matibabu ya magonjwa mbalimbali, zikiwemo ukaguzi wa kila mwaka. Wataalamu wanatunza katika eneo moja la magonjwa. Baadhi ya wataalamu wanatunza makundi fulani, kama vile wanawake au watoto. Wengine wanajitaalamu katika sehemu moja ya mwili, kama vile moyo, macho, au miguu. Unahitaji miadi kuona daktari binafsi. Kabla ya kuona daktari binafsi, kwa kawaida, lazima uoneshe ya kwamba unaweza kulipa kwa ajili ya huduma au kwamba una bima.

**Vyumba vya matunzo ya haraka ni kwa matatizo makubwa ya afya, yanayotokea kwa rafla.**




**HOSPITALI**. Madaktari na kliniki zinawapeleka wagonjwa wenye matatizo maalum kwenye hospitali kwa ajili ya vipimo na upasuaji. Huduma kutoka hospitali ni bei ghali, na hospitali inahitaji ushahidi wa bima au uwezo wa kulipa huduma hizo au una bima.




**VYUMBA VYA MATUNZO YA HARAKA**. Maeneo haya katika hospitali au kwingineko yamewekwa kwa matatizo makubwa ya afya na yanayotokea kwa rafla. Si lazima kufanya miadi kwenda kwenye eneo la hali ya haraka, lakini sehemu hizi ni sehemu zenye shuguli nyingi na utahitaji kusubiri kwa muda mrefu kama hali yako si mbaya sana. Huduma ya vyumba vya hali ya haraka ni ghali sana. Kama tatizo lako si la hali ya haraka, ni bora ufanye miadi ya kwenda kwenye kliniki au ofisi ya daktari.

---

Lubna alijikata kidole chake alipokuwa akikata mboga. Mume wake Emaad aliita texi na wakaenda kwenye chumba cha matunzo ya haraka cha hospitali ya karibu. Lubna na Emaad hawakuweza kuzungumza au kuandika Kiingereza, na hawakuweza kujaza makaratasi.  Ungejisikia je ungelikuwa Lubna au Emaad? Lubna na Emaad walipaswa kufanya nini?

---




**KLINIKI ZA UTUNZAJI WA HARAKA**. Katika jamii zingine, kliniki za matunzo ya haraka zinapatikana. Kliniki hizi ni kwa ajili ya ugonjwa au kidonda ambayo ina mahitaji ya huduma ya mara moja, lakini si kubwa zaidi ili kwenda kwenye chumba cha matunzo ya haraka. Hauitaji miadi.

# SURA YA NANE 8

***Fikiri kuhusu uzoefu wako uliopita kuhusu huduma ya afya.***

- ❒ Namna gani uliamua chakufanya?
- ❒ Ulikuwa na uchaguzi wa huduma ya afya?
- ❒ Uzowefu wako na watoa huduma za afya ulikuwa nzuri au mbaya?

***Patanisha wasiwasi ya afya upande wa kushoto na yale unapashwa kufanya kwa kuume.**** 

1. Unahoma kwa muda wa siku 3.
2. Una baridi na mafua.
3. Ulikuwa ukijisikia na wasiwasi na huzuni kwa muda wa miezi 2.
4. Unasikia mchoko.
5. Unafikiri una mfupa ya kuvunjika.
6. Una maumivu kali ya tumbo.



a. Uijitunze peke yako.



b. Uende kwa daktari.




c. Uende kwa chumba cha matunzo ya haraka.

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 221.

**Wamerikani wengi wanategemea mipango ya bima ya afya kwa sababu bei ya huduma ya afya ni juu sana.**

***Fikiri kuhusu kama hali za afya kwa ukarasa wa 95 ni madogo (nand yataboreka pekeyayo ama na matunzo za msingi nyumbani), inaweza kuhitaji matunzo, au ni kutisha maisha. Patanisha kila hali ya hizi ma picha sahihi hapa chini.*[*]**

| Kama unakitu ambacho: | Unapashwa: |
|---|---|
| 1. Ni kidogo |  a. Uende kwa chumba cha matunzo ya haraka. |
| 2. Yanaweza kuhitaji matibabu |  b. Uijitunze yumbani. |
| 3. Ni ya ghafla na kubwa |  c. Umwone daktari. |

***Wakati una shaka, pigia rafiki yako simu au maneja wa kesi yako kwa shauri.***

---

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 221.

*Hapa chini kuna zingine ishara ya kawaida nchini Marekani ambayo yanahusiana na afya. Patanisha ishara katika mstari wa juu na maana sahihi chini.** 

1.



2.




3.




4.



5.



6.




a. Hospitali

b. Duka la dawa

c. Sumu

d. Chumba cha matunzo ya haraka

e. Matunzo ya kwanza

f. Hatari


## KULIPA KWA AJILI YA HUDUMA ZA AFYA

*Fikiri kuhusu maswali yafuatayo kuhusu huduma za afya nchini mwako au nchi yako ya ukimbizi.*

- ❒ Namna gani huduma za afya zinalipwa?
- ❒ Ilikuwa bei ghali?

Huduma za afya nchini Marekani ni bei ghali, na mara nyingi watu wachache tu wanaweza kulipa deni za matunzo yao. Programu za serikali zinalipa deni za matunzo ya watu wa kipato cha chini ambao wana kubaliwa kwa program. Watu wengine wanategemea bima ya afya ya kulipa kwa afya yao.

### BIMA YA AFYA



Watu ambao wana bima ya afya wanalipa mara kwa mara kwa kampuni ya bima, na kishakampuni ya bima inalipa deni zao za matunzo, waajiri wengi wanatoa waajira wengi wanawapa wafanyakazi wao program za bima, na mara nyingi wanalipa sehemu ya beyi ya kila mwezi. Bei iliyobaki inakatwa kutoka kundi lako la malipo pamoja na kodi zako za mapato. Kwa kawaida, wafanyakazi wapya wanasubiri kwa muda kabla wakubaliwe kwa bima. Inawezekana kununua bima ya afya yako mwenyewe, lakini ni bei ghali kwa kawaida.

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 221.

**Kwa watu wenye umri wa kufanya kazi wenye kipato cha chini, serikali inatoa programu ambazo zinalipa kwa ajili ya matunzo kwa muda mfupi.**

**Nchini Marekani, una haki ya huduma za mkalimani na siri.**


Maria anafanya kazi ya muda maalumu, kwa dola 9 saa moja, na anapata faida ya huduma ya afya kwa ajiili ya jamaa. Mume wake Luis anafanya kazi ya kudumu, lakini hana faida. Maria anapewa kazi ya kudumu ambayo inalipwa dola 13 saa moja, lakini hatapewa faida ya huduma za afya. Ungelifanya nini ungelikuwa Maria? Kwa sababu gani faida za huduma za afya ni muhimu?

## MSAADA WA HUDUMA ZA AFYA KWA WAKIMBIZI (RMA), MSAADA WA AFYA KWA WATU WENYI KIPATO CHA CHINI (MEDICAID). NA MSAADA WA AFYA KWA WAZEE (MEDICARE)

Wakimbizi wanaweza kuomba msaada wa huduma za afya kutoka Shirika la Wakimbizi la Msaada wa Afya (Refugee Medical Assistance, RMA) au Msaada wa Afya (Medicaid). Programu zote mbili zinawalipia deni za huduma za afya kwa watu wenye umri wa kufanya kazi ambao wanapata malipo ya chini, lakini programu hizi zinaweza kutumiwa tu mpaka utakapopata bima kutoka kwa mwajiri wako au utapoweza kununua bima ya afya mwenyewe. Wakimbizi wenye umri zaidi ya miaka 65 wanaweza kupata msaada wa afya wa Medicare. Hii ni programu ya serikali inayosaidia watu ambao wana umri zaidi ya miaka 65 kulipa deni zao za huduma za afya.

***Patanisha aina ya bima ya afya na watu inayowasaidia. Fumbuo: Moja ya majibu inatumiwa kwa aina mbili za bima.****

1. Bima kwa wazee
2. Msaada wa huduma za afya kwa wakimbizi.
3. Msaada wa huduma za afya kwa watu wa umri wa miaka juu ya 65.



a. Aina hii ya bima ni kwa ajili ya watu wenye umri wa kufanya kazi wenye kipato kidogo ambao hawawezi kupata bima kupitia kazi zao. Wakimbizi wanakubaliwa kwa hii.



b. Aina hii ya bima ya afya inasaidia watu zaidi ya umri wa miaka 65 na deni zao za matunzo. Wakimbizi wanakubaliwa kwa hii.

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 221.

## HAKI ZAKO ZA KUPATA HUDUMA ZA AFYA



Nchini Marekani, una haki mbili muhimu za huduma za afya.Una haki ya kupata huduma za mkalimani na una haki ya siri.Haki ya siri inamaana kwamba daktari au muuguzi wako hawezi kumwambia mtu yeyote kitu chochote kuhusu afya yako bila ruhusa yako.

### HUDUMA ZA UKALIMANI

Inabidi uwe na uwezo wa kumuelewa daktari wako ili uweze kupata matunzo mema. Kama unahitaji msaada wa lugha kwa kuwasiliana na daktari wako, una haki ya kupata mkalimani akusaidie. Shirika lako la makazi mapya linaweza kukusaidia kupata mkalimani.

---

Paw Mu ana miadi ya daktari juma ijayo. Anaongea Kiingereza kidogo, lakini mara ya mwisho aliona daktari wake hakuelewa mambo mengi aliyosema. Kama ungekuwa Paw Mu, ungejisikia je? Paw Mu angepashwa kufanya nini?

---

***Fanya mazoezi ya kuomba mkalimani na mwengine. Hapa kuna mifano miwili ambazo unaweza kutumia kwa kufanya ombi:***

- ❒ I don't understand English. Can I please have an interpreter?
- ❒ I speak Swahili. I would like to talk to someone in that language.

### HALI YA SIRI

Kwa sheria, kila kinachotokea kati yako na mtoa huduma ya afya yako ni siri. Mtoa huduma wa afya yako hawezi kuwaambiya jamaa zako, rafiki zako, au mwajiri wako kuhusu hali yako ya afya bila kupata ruhusa yako.


---

Umma ana matatizo ya kupata mimba. Mume wake hataki Umma azungumze na daktari kuhusu hayo. Halafu daktari akimweleza mtu mwengine? Ungejisikia je ungelikuwa katika hali hii? Ni nini lazima Umma na mume wake wajuwe kuhusu madaktari nchini Marekani?

---

**Wamerikani wengi wanakwenda kwa daktari mara moja kwa mwaka kwa uchunguzi wa afya zao, ili waweze kujua kuhusu matatizo yoyote ya afya kaabla yakuwa mabaya.**

*Zungumza na mwenzako kuhusu kwa nini siri na daktari wako ni muhimu.*




**Usafi binafsi inaweza kuwa muhimu hasa kwa kupata na kuchunga kazi.**

## MAFIKIRI ZA WAMEREKANI JUU YA AFYA

*Chapa picha katika duara zilizo hapa chini kuonesha nini unafikiri kuhusu tabia za afya.*

Wamerikani wanaamini kwamba watu wanaweza kuepuka magonjwa kwa kuwa na usafi, kuwa na lishe nzuri, kufanya mazoezi, na kupata usingizi wa kutosha. Wamerikani wanavaa nguo zinazowafanya wapate joto wakati wa baridi na nguo zinazowasaidia kupunguza hali ya joto wakati wa majira ya joto. Wanakwenda kwa daktari au kliniki mara moja kwa mwaka, ili waweze kujua wana matatizo gani ya kiafya kabla matatizo hayo kuwa makubwa. Wanakwenda kumwona daktari wa meno ili meno yao yasafishwe mara mbili kila mwaka kwa kuhepuka matatizo makubwa kwa meno yao.



Madaktari nchini Marekani wanaweza kutokuwa wa uzowefu wa kutunza mangonjwa kutoka nchi nyingine. Unaweza kulazimishwa kumweleza daktari wako namna gani wewe na watoto wako mmepata matunzo mbele, na umweleze matumizi na madawa za nchi yako ambazo mmetumia. Lazima kujuwa ya kwamba madaktari na wauguzi nchini Marekani wanaweza kufikiri yakuwa baadhi ya dawa na matumizi kutoka nchi nyingine si salama. Baadhi ya dawa hizi na matumizi zinaweza hata kuwa kinyume na sharia nchini Marekani.

---

Soe Naing ana maumivu ya tumbo, hivyo anatumia baadhi ya mimea kutoka nchi yake. Baada ya muda, Soe Naing bado hajisikii vizuri na kumwona daktari. Daktari anashangaa wakati Soe Naing anamuambia kuhusu majani alizozitumia. Anamwambia ya kuwa lazima aache kutumia majani hizo. Kwa nini daktari anamwambia kuacha kutumia majani hayo? Ungelikuwa Soe Naing, ungeli itika shauri ya daktari na kuacha kuchukua majani? Lazima Soe Naing akumbuke nini kuhusu dawa za kiasili nchini Marekani?

---

## USAFI NA USAFI BINAFSI



Wamarekani wengi wanaoga kila siku, wana wosha meno yao mara mbili kila siku, wanatumiya shampuu kwa nywele zao mara nyingi, wana weka marashi mara moja kwa siku, na wana fua mavazi yao mara kwa mara. Maduka yanauzisha aina nyingi za bidhaa kwa kusaidia watu kutoonekana wachafu au kuwa na harufu yoyote ya jasho. Usafi binafsi inaweza kuwa muhimu hasa kwa ajili ya kupata na kulinda kazi.

---

Msimamizi mpya wa kazi wa Mathieu anamwambia Mathieu ya kuwa lazima aoge kila siku na kuweka marashi. Namna gani ungelijisikia ungelikuwa Mathieu? Namna gani Mathieu angelihepuka haya?

---

## LISHA BORA

Lisha shihi inamaana ya kula chakula kizuri kwa kutunza afya ya mwili.  Ni pia kupima kiwango cha vyakula ambavyo vinavyoweza kusababisha tatizo za afya na magonjwa makubwa kama yanakuliwa mara nyingi na kwa kiasi kikubwa. Kati ya vyakula hivyo kuna ambavyo vina sukari nyingi, chunvi, au mafuta (kwa mfano, vyakula vya kukaanga, vya sukari, na soda).

***Zungusha picha zilizo hapa chini ambazo zinaonesha chakula cha afya. Vuta picha ambayo inaonesha chakula isiyo ya afya.****



a. Vya sukari



b. Kuku



c. Tunda



d. Viazi karanga



e. Maziwa



f. Mafuta



g. Mchele



h. Chakula yenyi chunvi




i. Soda



j. Mboga



k. Maji

***Je, unaweza kufikiri kuhusu vyakula vingine ambavyo ni vya afya au si vya afya? Chapa baadhi hapa chini.***

| Chakula cha afya | Chakula isiyo ya afya |
|---|---|
| | |

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 221.


CAL COR Cultural Orientation Resource Center

***Saani hii ya chakula inatoa wazo ya vyakula ambavyo lazima kula ili kuwa na afya bora.***




***Kumbuka kwamba juu ya kula chakula cha afya, chakula bora, mazoezi ya mara kwa mara kama kutembea kwa dakika 20 kila siku ni muhimu kwa afya ya mwili na akili.***

## UTUNZAJI WA AFYA YA AKILI

Afya ya akili ni kuhusu jinsi unajisikia, unafikiri, na unaishi ukikubaliana na maisha. Inahusu pia na namna gani unashugulika na msongo wa maisha.



***Fikiri kuhusu namna gani afya ya akili ilishughulikiwa nchini mwako au nchi yako ya ukimbizi.***

- ❒ Watu walizungumza kuhusu afya ya akili?
- ❒ Pamoja na nani watu walizungumza afya ya akili?
- ❒ Namna gani watu walishugulika na msongo wa maisha?
- ❒ Njia gani ilikuwa ya kawaida kwa kushughulika na msongo wa maisha?

**Wamarekani wanaamini kwamba afya ya akili ni muhimu kama afya ya kimwili.**

Wamarekani wanaamini kwamba afya ya akili ni muhimu kama afya ya mwili, na kwamba huduma za afya nzuri pamoja na matunzo ya wataalamu wa afya ya akili wakati inahitajika. Wakimbizi na wageni wengine wanahitaji kuzingatia vizuri afya yao ya akili kwa sababu mara nyingi wanapata hali ya msukosuko wakati wa na ishi na hali ya kufadhaika wakati wa kujirekebisha na maisha ya Marekani. Kama unajisikia hali yako inakushinda na huwezi kuendelea na shughuli zako za kila siku, ni lazima utafute huduma za afya ya akili. Shirika lako la makazi mapya linaweza kukusaidia kupata huduma hizi na kuweka habari zako siri.

---

Kisha myezi 6 nchini Marekani, Namina alianza kukumbuka nyumbani. Alijuwa hii ni ya kawaida, lakini baada ya muda alianza kujisikia huzuni sana, na alitoka nyumbani mwake kwa kuenda kazini tu. Nini lazima Namina afanye? kwa sababu gani ni muhimu Namina afanye angalisho kwa jinsi anajisikia?

---



***Fikiri kuhusu ambacho unakifanya unapojisikia mwenyi wasiwasi na wa msongo.***

- ❒ Jinsi gani unakabiliana?
- ❒ Vitu gani vingine ungeliweza kufanya?
- ❒ Unazungumza na nani?



***Cheza mfano hii na mwengine njia moja ya kuomba msaada.***

- ❒ Mtu 1: Hujambo? Habari za leo?
- ❒ Mtu 2: Mimi sijisikii vizuri siku ziliopita.
- ❒ Mtu 1: Nini mbaya?
- ❒ Mtu 2: Sijisjikii kama mimi mwenyewe.
- ❒ Mtu 1: Unataka kusema au unamaanisha nini?
- ❒ Mtu 2: Sina furaha sana. Na sijui nifanye nini kuhusu hilo. Unaweza kunisaidia?

***Fikiri kuhusu njia zingine kwa kuomba msaada kwa mwengine.***

***Kama una matatizo ya kueleza unavyojisikia, angaliya picha zilizo kwenye kiambatisho C: nyuso za mhemuko kwa ukarasa 226 kwa uongozi mwingine.***

## KAMILISHA*

***Chagua jibu bora zaidi kwa maswali hapa chini ukifanya chaguo bora.***
***Hii ni mfano:***

*Lugha gani ndio inazungumzwa na watu wengi zaidi Marekani?*

a. Kichina.

(b.) Kiingereza.

c. Kiugerumani.

***Watu wengi Marekani wanazungumza kiingereza. Kwa hiyo jibu ni b. Kiingereza.***

1. Utakuwa na uchunguzi wa afya baada ya kufika nchini Marekani?

   a. Ndiyo.

   b. Hapana.

2. Ni kwa njia zingine watu wanalipa huduma ya afya nchini Marekani?

   a. Bima ya afya (Mara nyingi inatolewa kwa njia ya mwajiri wao).

   b. Programu za serikali ambazo zinalipa kwa huduma za afya kwa watu ambao wana pato ya chini, kwa muda mfupi tu.

   c. Kwa mapato yao wenyewe.

   d. Programu za serikali ambazo zinalipa deni zote za matunzo kwa watu wote.

   e. Chaguo a, b, na c.

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 221.

3. Lazima mtu aende kwenye chumba cha matunzo ya haraka (Emergency Room "ER") wakati tu anakabiliwa na matatizo makubwa ya afya.

    a. Kweli.

    b. Uongo.

4. Vitu gani vifwatavyo ndivyo Wamarekani wanaamini yanaweza kusaidia kuzuia magonjwa?

    a. Kufanya mazoezi mara kwa mara.

    b. Kula vyakula vyenyi sukari nyingi na chunvi.

    c. Usingizi wakutosha usiki.

    d. Kuwa safi.

    e. Chaguo a, c, na d.

5. Kama unamweleza daktari wako kitu chochote, daktari wako anahitajika kuwaambiya jamaa, marafiki, na mwajiri wako.

    a. Hii ni kweli.

    b. Hii ni uongo.



# Sura Ya Kenda
## MATUMIZI YA FEDHA

Gharama za maisha nchini Marekani ni juu kabisa. Hii ndiyo sababu kupata kazi Marekani haraka iwezekanavyo ni muhimu sana kwa watu wazima wote ambao wanaweza kufanya kazi. Lazima uwe mwangalifu na pesa yako, ili usije kutumia zaidi ya uwezo wako. Wafanyakazi wa shirika lako la makazi mapya watakusaidia kufanya bajeti yako. Bajeti itakusaidia kujuwa pesa ngapi unayo, ngapi unaweza kutumia, na ngapi unaweza weka akiba.

---

### Sura Hii Itajadili

» Kufanya mipango ya matumizi
» Wapi unaweza kununua vitu
» Kulipa kodi, Huduma za benki, na Historia ya mkopo.

**Kuweka bajeti itakusaidia kujua pesa ngapi unayo, ngapi unaweza kutumia, na ngapi unaweza weka akiba.**

## MANENO MUHIMO YA KIINGEREZA

Maneno ya Kiingereza yafuatayo hutumiwa wakati wa kuzungumza kuhusu makazi mapya nchini Marekani. Maneno haya yatakuwa na mafaa kwako kuyaijifunza.

***Sema neno katika Kiingereza, andika lugha yako ya asili. Kisha, chapa picha ya neno, andika maana yake, au uitumiye katika msemo. La kwanza limefanyika kwa ajili yako.***

| Katika lugha yako | Katika kiingereza | Chapa picha ya neno, andika maana yayo, au uitumiye katika. |
|---|---|---|
| *Kuwa na uwezo wa kununua* | afford | *Lilith na Abdul wanaangalia kwenye akaunti yao ya benki iliwajuwe kama wanaweza kununua gari.* |
| | budget | |
| | change | |
| | cheap | |
| | coins | |
| | dollar | |
| | expensive | |
| | money | |
| | sales tax | |
| | wallet | |
| | How much does it cost? | |

**Kila mwezi utahitaji kulipa kwa gharama za maisha na gharama nyingine.**

**Kama una malengo ya muda mrefu kama vile elimu au kununua nyumba, unaweza kutaka kuweka kiasi fulani katika akaunti yako ya akiba kila mwezi.**

## KUFANYA MIPANGO YA MATUMIZI

Kila mwezi utahitaji kulipa kwa gharama za maisha na gharama nyingine.



***Gharama zako za mara kwa mara zilikuwa gani nchini mwako au nchi yako ya ukimbizi?***

Haya yatakuwa gharama zako kubwa za maisha chini Marekani:



**KODI YA KUPANGA.** Hii, pengine itakuwa gharama yako kubwa ya kila mwezi.

---

Hani alijua ya kwamba gharama za kupanga zinaweza kuwa ghali nchi Marekani, lakini alishangaa kupokea bili yake ya kwanza ya umeme. Gharama za maisha gani zingine Hani anaweza kupata?

---



**UMEME NA GHARAMA NYINGINE.** Hii ni pamoja na umeme, gesi au mafuta, maji, na ukusanyaji wa takataka. Baadhi ya gharama hizi zinaweza kuwa kwenye kodi yako ya kupanga, lakini unaweza lazimishwa ulipe gharama nyingine wewe mwenyewe. Katika sehemu nyingi za Marekani, bili zako za umeme na gesi au mafuta zitakuwa kubwa katika myezi za majira ya baridi na myezi ya joto wakati unahitaji joto au hali ya hewa zaidi.



**CHAKULA.** Unaweza kuweka hakiba kwenye chakula kwa kutafuta maduka na biashara zenye bei za chili kabisa na kununua biashara ya bei iliyo pungunziwa.

**ULINZI WA WATOTO.** (Angalia Sura 12 kwa maelezo zaidi kuhusu ulinzi wa watoto.)



**USAFIRI.** Kati ya hii kuna bai ya kwenda na kutoka kazini, dukani, na kwenye miadi.




**SIMU.** Utahitaji kulipa simu yako kila mwezi. Kumbuka ya kwamba kuita nje ya Marekani inaweza kuwa bei ghali. Zungumza na watu katika jamii jayo ili ujifunze kuhusu njia bora ya kuita nje ya Marekani.



**MKOPO WA SAFARI.** Karibu myezi 6 kisha kufika Marekani, utahitaji kuanza kulipa deni yako ya mkopo wa safari kila mwezi mpaka unalipa yote.



**HUDUNA ZA AFYA.** Utakapopata kazi ya kudumu, unawezakupata aina fulani ya bima ya afya. Lakini kazi nyingi za kiwango cha kwanza hazitoi bima miezi ya kwanza ya ajira. Inaweza kukubidi ununue bima yako mwenyewe.



**AKIBA NA MSAHADA KWA JAMAA LAKO NJE YA MAREKANI.** Kama una malengo ya muda mrefu kama elimu au kununua nyumba, itakubidi uweke kiasi fulani kwenye akaunti ya akiba ya benki kila mwezi. Unaweza pia kutaka kutuma pesa kwa watu wa jamaa yako amawo wangali nchini mwako. Utakapo kuwa na kazi na kujua ngapi unatumia kila mwezi, unaweza kuamua pesa ngapi unaweza weka hakiba au kutuma nyumbani kila mwezi.



***Zunguusha malipo makubwa ya maisha yaliyotajwa kwenye ukarasa 110 na 111 ulizozilipa zamani.***

***Hapa kuna mifano ya malipo unaweza kufikiria wakati wa kuunda bajeti***

*nchini Marekani.*

| Aina ya malipo | Maelezo na vitu muhimo | Bei nchini Marekani | |
|---|---|---|---|
| | | Mtu 1 | Jamaa ya watu 5 |
| **Kodi ya kupanga** | | | |
| **Umeme na gharama nyingine (gesi, umeme, ....)** | Malipo ya kila mwezi | | |
| **Chakula** | Chakula kilicho andaliwa nyumbani dhidi ya kula nje. | | |
| **Ulinzi watoto** | Malipo kwa kila mtoto | | |
| **Usafiri** | Usafiri wa umma dhidi ya kuwa na gari | | |
| **Simu** | Ya karibu, ya mbali, ya nje ya nchi | | |
| **Mkopo wa safari** | Inapashwa kulipwa katika kipindi cha myezi 36 | | |
| **Bima za afya** | Kwa njia ya kazi dhidi ya kuinunua mwenyewe, dhidi ya kutokuwa na bima ya afya | | |
| **Malipo mengine** | Hakiba na msaada kwa jamaa iliyo nje ya Marekani, mavazi, vifaa vya nyumbani, vifaa vya vyoo, na vifaa vya shule | | |

*Gharama zingine unaweza kufikiria:*

| Aina ya malipo | Maelezo na vitu muhimo | Bei nchini Marekani | |
|---|---|---|---|
| | | Mtu 1 | Jamaa ya watu 5 |
| **Kutoka** | | | |
| **Jambo la kupitishia muda** | | | |
| **Televisheni/ Interneti/ simu ya mkononi** | | | |
| **Shuguli za zaidi** | | | |

Saw Tun alifanya kazi mbili iliasaidie watoto wake watatu na kutuma fedha kwa jamaa yake nje ya Marekani. Alijisikia akichoka sana wakati wa muda kidogo yeye alikuwa nayo kwa kuwa na watoto wake. Kama ungelikuwa Saw Tun, ungelifikiria kufanya nini? Ungelizungumza na nani kuhusu changamoto hizi?

**Maduka makubwa ni maduka kawaida ya chakula.**

***Kuna vitu vingi ambavyo wewe au watu wa jamaa yako mnaweza hitaji kununua Marekani. Kwa ajili ya bajeti, itakuwa muhimu kutambua nini jamaa yako inataka dhidi ya nini jamaa yako inahitaji. Baadhi ya vitu vinavyo takiwa vinaweza kuwa bei ghali na visivyo vya lazima, na unaweza kuvitoa katika mahitaji ya jamaa yako. Chapa dhuara kwa vitu vilivyo hapa chini ambavyo jamaa yako inaweza kuhitaji. Uvute vitu ambavyo jamaa yako haihitaji, lakini inaweza kutaka.**** 



a. Kazi



b. Mavazi sahihi



c. Gari



d. Mbegu



e. Vitu vya usafi



f. Nyumba kubwa



g. Fleti ama Nyumba



h. Mazoezi ya mara kwa mara



i. Televisheni



j. Shahada ya chuo kikuu



k. Mboga



l. Maji

*Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 221.

## WAPI UNAWEZA KUNUNUA MAHITAJI YAKO

Maduka na masoko ya Marekani yanatoa aina nyingi za biashara na huduma mbalimbali.



***Fikiri kuhusu ambapo ulinunua vitu nchini mwako au nchi yako ya ukimbizi.***

- ❒ Wapi ulinunulia chakula?
- ❒ Wapi ulinunulia dawa?
- ❒ Wapi ungeweza nunulia mahitaji mengine ya nyumbani?
- ❒ Wapi ulinunulia nguo na viatu?

---

Sumitra alijifunza kuhusu maeneo mbalimbali ya maduka katika jamii yake mpya. Alijua ana bajeti, hivyo, alitumia muda mwingi kwenda maduka mbalimbali ili apate bei nzuri. Lakini ilichukua muda mwingi, na kisha kupata kazi, Sumitra hakupata tena muda wa kuenda kwa maduka hizo mbalimbali. Vitu ngani Sumitra angeweza kufanya?

---

Hapa kuna nafasi kawaida ya kununulia vitu Marekani:




**MADUKA YA SUPAMAKETI.** Haya ni aina ya maduka ya kawaida yanayo uzisha chakula. Maduka mengi ya aina hii yanauzisha pia bishara za kusafisha, biashara za uzuri, magazeti, biashara za nyumbani, na dawa zisizohitaji maandishi ya daktari.




**MADUKA ZA MADAWA.** Maduka hayo yana maduka ya dawa kwa kawaida ambapo dawa zinaweza kununuliwa. Mengi pia yanauzisha madawa yasiyo lazimisha maandishi ya daktari, kama vile mafuta ya mwili, magazeti, na chakula. Vyakula ni mara nyingi bei ghali na vichache kuliko vitu vingine vinavyo uzishwa katika maduka ya supamaketi.



**MADUKA MAKUU YA BIASHARA MBALI MBALI.** Maduka haya yanauzisha nguo, viatu, funicha, vifaa, na vitu vingine ambavyo si chakula.



**MADUKA ZA KUBORESHA NYUMBA.** Maduka haya yana uzisha biashara ili kutengeneza au kudumuisha nyumba, kama vile zana, vifaa, mbao, na mimea.

**Unaweza kupata vyakula vya nchini mwako katika maduka ya vyakula vya asili.**

**Kodi nchini Marekani zinalipa kwa ajili ya huduma nyingi ambayo kila mtu anatumia.**

**MADUKA YA BEI CHINI.** Maduka haya yanauzisha biashara kwa bei ya chini zaidi kuliko yale yanayo patikana katika maduka ya kawaida. Zaidi ya mavazi na vitu vya nyumbani, maduka mengi ya bei ya chini yana uzisha vitu vya elektroniki na vyakula.




**MADUKA YA BIASHARA ZILIZOTUMIWA.** Maduka haya yanauzisha vitu vilivyo tumiwa, kama vile funicha, sahani, na nguo, kwa beyi ya chini. Ni ya kawaida kwa Wamarekani kununua vitu vya zamani.



**MADUKA YA VYAKULA VYA ASILI.** Maduka haya ni ya wahamiaji au wakimbizi. Unaweza kupata vyakula kutoka nchi yako kwenye duka la vyakula vya asili.




---

Fariba alikuwa na shida ya kupata vyakula ambavyo alifurahi kupika nchini mwake katika maduka ya sepemaketi ya Marekani. Wapi anaweza kwenda ili apate vyakula hivi? Lazima Fariba amuombe nani msaada?

---

**UUZISHAJI YANAYOFANYWA NYUMBANI.** Kwenye uuzishaji haya, watu wanauzisha vitu kutoka nyumba zao kwa bei za nchini. Ni sehemu nzuri sana za kununua vitu vya nyumbani, fanicha, na nguo. Uuzishaji wa nyumbani yanatangazwa kwenye magazeti au kwenye matangazo ya mtaani.



Kabla ya kuishi Marekani, Basma alikuwa bado haja kuwa fanicha iliyo tumikishwa. Anataka kubadilisha fanicha za zamani ambazo alipewa na shirika lake la makazi mapya, lakini hana pesa ya kununua vitu vipya. Ungelikuwa Basma ungelijisikia namna gani? Basma anaweza kufanya nini?

## KULIPA KODI

Kodi nchini Marekani zinalipa huduma nyingi zinazotumiwa na wakazi wote wakiwemo wakimbinzi. Kodi za mapato zinalipia elimu ua umma, uangaliaji wa njia na barabara kuu, polisi, huduma za kuzima moto na hali ya dharura, na programu za huduma za jamii. Watu wanaoishi Marekani wanalipa aina tatu za kodi za mapato:

Peter Htoo hakuwahi kulipa kodi kabla sasa, na hakuelewa ni kwa maana gani. Alikasirika sana kulingana na pesa iliyokamatwa katika mshahara yake kila wiki. Nini unaweza kumueleza Peter Htoo kuhusu kodi?

**KODI ZA MAPATO.** Kila mfanya kazi analipa kodi za mapato ya serikali ya nchi, na makazi wa baadhi ya majimbo wanalipa kodi ya mapato ya jimbo. Kodi hizi zinatolewa na mwajiri wako kutoka kwenye mshahara wako. Kama una pato ya chini, serikali itakurudishia baadhi ya hayo uliyoyalipa.




**KODI ZA MALI BINAFSI.** Serikali za jamii zinakusanya kodi za mapato za nyumba, kiwanja, majengo unazo. Mwenye nyumba yako analipa kodi hizi kwa nyumba unayo panga. Sehemu nyingine wanalipisha kodi kwa magari.



**KODI ZA MAUZO.** Wanunuzi kwenye majimbo mengi watu wanalipa kodi kwa vitu wanavyo nunua. Kodi ya mauzo inaongezeka kwa vitu mbalimbali kama vile chakula au madawa. Kwa vitu vingine kama vile sigara na pombe ni zaiidi.



**Wamarekani wengi wanaweka fedha zao katika benki kwa sababu ina hakiba kutoka serikali ya Marekani. Hii ina maanisha kwamba kama fedha inapoteya au kuibiwa katika benki, serikali la Marekani litakuilipa fedha yako.**

***Zunguusha vitu vilivyo hapa chini ambavyo kodi ya Marekani inaweza kulipa kwa ajili yavyo. Vuta vitu kodi haiwezi kulipa nchini Marekani.****



a. Elimu ya umma



b. Barabara



c. Matengenezo ya nyumbani



d. Gari binafsi




e. Huduma za dharura



f. Pombe au sigara



g. Bishara ya kufula




h. Mipango ya huduma za jamii

***Wapi uliweka fedha yako nchini mwako au nchi yako ya ukimbizi?***

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 221.

# SURA YA KENDA 9


## HUDUMA ZA BENKI

Wamarekani wanaweka fedha yao kwa kawaida kwenyi benki kuliko nyumbani. Fedha ambayo unaweka kwenye benki ina bima ya serikali ya Marekani. Hii ina maana kwamba kama fedha inapoteya au kuibiwa katika benki, serikali la Marekani litakulipa fedha yako. Benki zina aina mbalimbali za akaunti kwa lengo mbalimbali. Kuna aina mbili kuu za akaunti za benki:

**AKAUNTI ZA AKIBA.** Hizi ni za kuweka akiba. Benki zinakulipa asilimia fulani ya fedha kwa kuweka fedha zako kwenye akaunti na kuzitumia fedha zako.

**AKAUNTI YA CHEKI.** Hizi ni kwa malipo. Benki inakupa cheki unazoweza kuzijaza kwa kulipa kodi ya nyumba na madeni mengine. Lazima ufanye angalisho usiandike cheki za pesa zaidi kuliko ulizo nazo kwenye akaunti yako. Ukiyafanya, benki itakulipisha pesa.

Mfano wa cheki:


**Your full name**
Your street address
Your city, state, zip code

Check number

Date

Pay to the order of

$

Dollars

**Name of bank**

For

Bank and state routing numbers; your account number



***Fikiri maswali yafwatayo:***

- ❒ Faida ya kuweka pensa kwenye benki ni gani?
- ❒ Kwa nini kuweka fesa katika benki nchi Marekani ni zoezi ya kawaida?
- ❒ Kwa nini kuweka fesa katika benki inaonekana kuwa salama?

---

Katika nchi yake, Malyun aliweka pesa yake katika mahali pa kuficha nyumbani. Sasa, kwa kuwa iko nchni Marekani, hajisikii vizuri kuweka pesa yake katika benki, ingawa anajuwa kwamba watu wengi nchini Marekani wanatumia benki kwa kuweka hakiba. Nini unaweza kumueleza Malyun? Kwa nini benki ni mahali salama kuweka fedha yako?

---

**Wakati unatumia mpango ya mkopo au kadi ya mkopo, unakopa fedha na utalipishwa faida juu ya kiasi ya deni unayo.**

**Kwa kuwa na historia nzuri ya mkopo, ulipe kwa wakati kila mwezi.**

## MKOPO NA HISTORIA YA MKOPO




Wamarekani wanatumia kadi za mkopo kwa kawaida, na mipango ya mkopo kwa manunuzi makubwa kama gari na fanicha. Kadi na mipango zinawaruhusu kulipa kidogo mara nyingi kwa muda fulani badala ya kufanya malipo yote wakati wa ununuzi.

Unapotumia kadi ya mkopo, unakopa pesa. Benki au kampuni ambayo inatoa kadi ya mkopo inatoza riba juu ya idadi ya pesa ulizokopa, na lazima ulipe kila mwezi. Ukikosa kulipa, kampuni ya kadi ya mkopo inaweza kuchukua pesa unayo kwa deni. Ukikosa kulipa mara nyingi, duka inaweza kuchukua biashara uliyo nunua.

Ukiamua kupata kadi ya mkopo, itabidi uitumie kwa uangalifu. Ni rahisi kupata deni kubwa kwa kutumia kadi za mkopo. Kabla ya kununua kitu kwa kutumia kadi ya mkopo hakikisha kwamba utaweza kufanya malipo ya kila mwezi zaidi ya malipo nyengine

---

Kampuni ya kadi ya mkopo ilimtolea U Myint tiketi ya safari ya ngede ya bure akichukua kadi ya mkopo mara ya kwanza. Alitumia kadi yake kwa kununua vitu ambavyo hakuwa na uwezo wa kukilipa. Kisha mwezi moja alipata bili yake. U Myint hakujua ya kwamba angelipaswa lipa deni yake haraka hivyo au kulipa faida nyingi. Namna gani U Myint angelihepuka deni hizi kumueleza? Nini unaweza U Myint kuhusu matumizi ya kadi za mkopo hizi?

---

*Kwenye kiwango kilicho hapa chini, chapa kwa kuhakikisha au andika kuhusu mazuri na mabaya ya kuwa na kadi ya mkopo.*

| MAZURI | MABAYA |
| --- | --- |
| | |

*Jadili kuhusu mazuri na mabaya na mwengine.*

## HISTORIA NZURI YA MKOPO

Wakati una mikopo au kutumiya mikopo, unaweza kuanzisha historia ya mkopo. Mashirika binafsi yanayotoa maelezo ya mkopo yanafanya ripoti ya mkopo inayoonyesha historia ya mkopo, na benki yanaangalia ripoti unapoomba mkopo au kadi ya mkopo.




**HISTORIA MBAYA YA MKOPO.** Kama unalipa kwa wakati kila mwezi, historia yako ya mkopo itakuwa nzuri na benki zitakubali kukukopesha fedha na kukupa kadi za mkopo.


**HISTORIA MBAYA YA MKOPO.** Kama unakosa kulipa au ukitumia kadi yako ya mkopo kuzidi uwezo wako wa kulipa, utakuwa na historia mbaya ya mkopo na hautaweza kupata mikopo au kadi ya mkopo baadaye.

# 9 MATUMIZI YA FEDHA

**Kulipa kila mwezi mkopo yako ya safari ni bahati yako ya kwanza kwa kujenga historia nzuri ya mkopo nchini Marekani.**

***Kama haukulipa bili yako kwa wakati katika nchi yako au nchi yako ya ukimbizi, nini ingetokea?***

## MKOPO YA KUSAFIRI




Lazima kuweka pesa pembeni kwa kulipa mkopo yako ya safari kila mwezi. Hii ni bahati yako ya kwanza ya kujenga historia nzuri ya mkopo nchini Marekani. Kumbuka ya kuwa kukosa kulipa inaweza sababisha uwe na historia mbaya ya mkopo. Kama una shida kwa kulipa eleza shirika lako la makazi mapya mara moja.

---

Jasmin alipata bili yake ya kwanza ya mkopo ya safari. Alikuwa na kazi ya sehemu ya muda, na alijisikia hana pesa ya kutosha kwa kulipa. Kwa sababu gani ni muhimu Jasmin alipe, hata kama ni kisasi kidogo?

---

## KULIPA BILI



Lazima pia ulipe kodi yako ya kupanga na gharama za umeme na gesi au mafuta kwa wakati kila mwezi. Ukichelewa kulipa, unavunja agano na unaweza kuwa na shida na sharia. Shida hii inaweza kuoneka kwenye ripoti yako ya mkopo.

# SURA YA KENDA 9

Naw Gay na mume  wake hawawezi kusoma kiingereza. Siku moja walipata barua. Ndani kuna kipande cha karatasi yenyi miandiko. Mwezi iliyo fwata, walipata barua ingine. Kisha posho chache hawakukuwa na umeme. Naw Gay alimuita maneja wake wa kesi, ambaye alikuja na akatambua barua. Naw Gay hakulipa bili ya umeme, kwa hiyo umeme ulikatwa. Nini ya lazima Naw Gay na mme wake wangeli fanya? Shauri gani unaweza kuwaptia?

***Jaza misemwa yafwatayo kuhusu kulipa bili na malipo nyingine Marekani:***




- ❒ Malipo ambayo nayajuwa ni …
- ❒ Bili ambazo ni mapya kwangu ni…
- ❒ Najitumainia zaidi kuhusu…
- ❒ Vitu vinavyo nipa wasiwasi ni …

***Fikiri pamoja na mwengine kuhusu malipo Marekani.***

## KAMILISHA*

***Chagua jibu bora zaidi kwa maswali hapa chini ukifanya chaguo bora.***
***Hii ni mfano:***

*Lugha gani ndio inazungumzwa na watu wengi zaidi Marekani?*

a. Kichina.

(b.) Kiingereza

c. Kiugerumani.

***Watu wengi Marekani wanazungumza kiingereza. Kwa hiyo jibu ni b. Kiingereza.***

1. Gani ya yafwatayo inachukuliwa kama ya lazima?

   a. Umeme.

   b. Gesi.

   c. Ukusanyaji wa takataka.

   d. Yote ya juu.

2. Ni bei nchini kununulia vyakula kwenye maduka ya vyakula pahali pa kwenye supamaketi.

   a. Kweli.

   b. Uwongo.

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 221.

3. Gani ya yafwatayo ni kodi ambayo watu wanao ishi Marekani wanalipa?

   a. Kodi za mapato.

   b. Kodi za mali binafsi

   c. Kodi za mauzo.

   d. Watu hawalazimishwi kulipa kodi yoyote Marekani.

   e. Chaguo a, b, na c.

4. Wapi Wamarekani wengi wanaweka pesa yao?

   a. Nyumbani nchi ya kitanda

   b. Kwenye benki au mikopo ya muungano.

   c. Katika nafasi salama nyumbani mwao.

   d. Kwa marafiki wao ama wandugu wanaowatumainia.

5. Rafiki yako ameanza kazi yake ya kwanza na kisha mwezi moja akapata kadi ya mkopo. Ameanza kununua fanicha mpya, mavazi, na vitu vingine na kadi yake ya mkopo. Anapokea yakutosha kwa kulipa nyumba, chakula, lakini hana yakutosha kwa kulipa kwa ajili ya vitu alivyo vinunua na kadi yake ya mkopo. Kwa hivyo hawezi kulipa kadi yake ya mkopo. Yeye atakuwa na aina gani ya historia ya mkopo?

   a. Historia mbaya ya mkopo.

   b. Historia nzuri ya mkopo.



# Sura Ya Kumi
## KUJIREKEBISHA KIUTAMADUNI NA KABADILISHA NAFASI

Kama wengine ambao walioondoka kwao na kuhamishwa katika nchi ya kigeni, pengine utajisikia na wasiwasi na kuchanganyikiwa wakati unajaribu kuzowea nchi yako mpya. Nikawaida kujisikia hivyo, yanakwenda kisha masiku. Unaweza kuhitaji miaka 2 hadi 5 kwa kuzowea kabisa masiha katika jamii yako mpya. Marekebisho yako itakuwa rahisi kama unashirikiana na wale ambao wanakusaidia na kama uko mvumilivu na wazi na mwaminifu kwao. Pia kujifunza kwa haraka iwezekanavyo itakusaidia kuzowea. Kujifunza kuishi katika utamaduni mpya si rahisi, lakini, inaweza pia kuwa uzowefu mzuri unapojifunza mambo mapya na kupata ujuzi mpya.

---

### Sura Hii Itajadili

» Kujirekebisha ki utamaduni
» Kukabiliana na mshituko wa utamaduni na msongo
» Kubadili nafasi katika jamaa

**Kujifunza kuishi katika nchi mpya inachukuwa wakati. Marekebisho yako itakuwa rahisi kama unashirikiana na wale wanaokusaidia na kujifunza kusema kiingereza haraka iwezekanavyo.**

## MANENO MUHIMU YA KIINGEREZA

Maneno ya kiingereza yafuatayo yanatumiwa wakati wa kuzungumza kuhusu kujirekebisha kiutamaduni na kubadilisha nafasi ambayo inatokea wakati wakuhamia Marekani. Maneno haya na misemwa haya yatakuwa na mafaa kwako kuyajifunza.

***Sema neno katika Kiingereza, andika lugha yako ya asili. Kisha, chapa picha ya neno, andika maana yake, au uitumiye katika msemo. La kwanza limefanyika kwa ajili yako.***

| Katika lugha yako | Katika kiingereza | Chapa picha ya neno, andika maana yayo, au uitumiye katika msemo. |
|---|---|---|
| *ulezi wa watoto* | child care | *Ulezi wa watoto ni huduma ya watoto wa watu wengine na huduma ya chekechea, yaya, au mlezi wa muda.* |
| | culture | |
| | culture shock | |
| | diversity | |
| | retirement | |
| | traditions | |
| | values | |

**Wakimbizi wengi wanajikaza kubaki na mila na madili yao na wakati huo huo wanajifunza matabia mapya ya Marekani.**

## KUJIREKEBISHA KIUTAMADUNI

Kama mgeni, unahitaji kujifunza kuhusu mila na madili za Marekani. Lakinisi si kusema ya kwamba unapashwa kuacha utamaduni wako wote. Wakimbizi wengi wanajikaza kubaki na milaa na madili yao na wakati huo huo wanjifunza matabia mapya ya Wamerikani. (Angalia Sura ya 2 kwa maelezo zaidi kuhusu maadili ya Marekani). Unaweza pia kupata nafasi za kushiriki utamaduni wako na wanachama wa jamii yako.



Sabah ajisikia kuwa yeye ni watu wawili tofauti. Kazini anapana maonyi yake mara nyingi na anafanya kazi na wanaume. Nyumbani, yeye ni mama wa asili na mama wa nyumbani. Anapika chakula, na kusafisha, anatunza watoto, na anakubaliana na mme wake. Kama ungekuwa Sabah, ungelijisikia namna gani? Ungelibaki katika hali hizo mbili mbali mbali ungelijaribu kupata usawa kati ya hayo mbili?


CAL COR Cultural Orientation Resource Center

# SURA YA KUMI 10

***Fikiri kuhusu maadili ambayo yanaweza kuwa ya faida kwako. Kati hii, inaweza kuwa ku andikisha watoto wako shuleni, kuishi katika jamii salama, kuwa na uwezo wa kusema huru na kuwa na haki ya kidini.***

***Andika au chapa maadili mbalimbali ambazo ni za lazima kwako katika duara zilizo hapa chini. Kwa mfano, kati ya hii kunaweza kuwa jamaa yako, afya, na utulivu wa kifeza.***

Baadhi ya maadalili nchini Marekani yanaweza kuwa tofauti na maadili unayo fikiri ni ya lazima sana. Lazima upate usawa katika ya makundi mawili ya maadili.

---

Myo Myint na Yin Nwe ni bibi na bwana. Walipofika mara ya kwanza Marekani, walijaribu sana kuanza maisha yao kama waliyokuwa nayo nchini mwao, lakini Yin Nwe aliweza kupata kazi yake ya kwanza, kwa hiyo, Myo Myint alibaki nyumbani kwakujali watoto na nyumba. Kisha masiku, Myo Myint alipata kazi ya muda, lakini Yin Nwe' alikuwa na mshahara ya zaidi. Namna gani ungelijisikia ungelikuwa katika hali hii?


---

# 10 KUJIREKEBISHA KIUTAMADUNI NA KABADILISHA NAFASI

**Mshtuko wa ukamaduni na msongo ni kawaida. Mtu yeyote anayeshi katika mahali mapya anaweza kuyaona.**

## MPINDO-U WA MAREKEBISHO YA KITAMADUNI

Mchoro iliyo hapa chini inaonesha hatua za kawaida za marekebisho ya kiutamaduni ambazo watu wengi wanaona wakati wanahamia ao kutembelea mahali mapya.




| KIPINDI CHA FURAHA | KIPINDI CHA MSHTUKO WA KIUTAMADUNI | KIPINDI CHA MAREKEBISHO | KIPINDI CHA UJUZI |
|---|---|---|---|
| Kujisikia msisimko na furaha, wakati kila kitu kipya na ya kusisimua na kizuri. Hii inatokea mara nyingi kisha kufika mahali mapya. | Kujisikia na wasiwasi na kuchanganyikiwa wakati mgeni anajaribu kuzowea katika mazingira ambayo ni tofauti na isiyo ya kawaida. | Kujisikia wakupoa wakati mgeni anatoka katika mshtuko wa utamaduni na anaanza kujisikia vizuri zaidi na kujiamini katika mahali mapya. | Kujisikia vizuri na maisha mapya na utamaduni upya, ingawa kuna vipindi ambavyo ni bado vigumu wakati mwingine. |

Yote yalianza vizuri kwa Tara. Alipata kazi haraka, watoto wake walikuwa na furaha shuleni, na Kiingereza yake iliboreka alipokuwa akizungumza na marafiki yake mapya. Lakini, kisha karibu myezi 6 kisha kufika Marekani, Tara alianza kukumbuka nchi yake. Mtoto wake wa kiume alianzakupata shida shuleni, na hakuweza kujuwa namna gani anaweza kumusaidia. Kulingana na mpindo-U ya marekebisho ya kitamaduni, nini inaweza kutokea kisha? Muda gani unafikiri itachukua kabla Tara aanze kujisikia vizuri? Ungelifanya nini ungelikuwa Tara? Ungelizungumza na nani?

## KUKABILIANA NA MSHTUKO WA UTAMADUNI NA MSONGO

Unapokuwa katika hali ya mshtuko wa utamaduni, unajisikia mara nyingi mnyonge na wakuchanganyikiwa kwa kuishi katika nchi usiyoelewa. Mshtuko wa utamaduni ni kawaida. Mtu yeyote anayeishi katika mahali mapya anaweza kuyaona.



***Kama unaona mshtuko wa utamaduni, haya ni baadhi ya ngisi unaweza kujisikia:***

- ❒ Wakuchanganyikiwa kwa sababu huwezi kufanya mambo rahisi kama kwenda sokoni au kuchukua usafiri umma.
- ❒ Wakuchoka wakati wa mchana au hauwezi kulala usiku.
- ❒ Wa hasira.
- ❒ Asiyekuwa na nia ya kitu chochote au wauzuni
- ❒ Wa huzuni bila kujua sababu.
- ❒ Asiyekuwa na hamu ya kula chochote.

Mary Paw ni wakufurahi kwa kawaida na mwenyi nguvu. Lakini kisha karibu myezi 4 nchini Marekani, aligeuka mpole na wauzuni. Ana matatizo ya kuamka asubuhi na kufanya shuguli zake za kila siku, kama vile kulipa deni zake, kwenda sokoni, na kufanya kazi. Mary Paw anaanza kuzungumza kuhusu kurudi nchini mwake na hanahamu ya chakula. Lazima Mary Paw afanye nini? Anapashwa zungumza na nani? Ungelimjua Mary Paw, ungelimsaidia namna gani?

**Njia za kukabiliana na mshtuko wa utamaduni inawezakuwa kukutana na marafiki, kucheza michezo, au kuwasiliana na kundi za kidini au za kiroho.**

***Fikiri kuhusu jinsi hizi za kujisikia.***

- ❒ Jinsi gani kati ya hizi ulijisikia zamani?
- ❒ Wakati alijisikia hivyo, nini ilikusaidia kujisikia bora?

***Shiriki baadhi ya mawazo haya na mwengine. Uliza mwengine kuhusu mawazo mengine.***

Kujisikia hivi ni ya kawaida na mara nyingi, kujisikia hivi inaisha na wakati. Wageni wengi Marekani walijisikia hivi na walikuwa na nguvu zaidi na uwezo wa kushugulikiwa na hayo.

---

Furaha ya Grace kuhusu maisha yake mapya inafifia kama mambo yanakuwa magumu na msongo inapoanza. Anageuka mtu wa woga, na anaanza kuweka hasira yake kwa jamaa lake. Anazungumza na msimamizi wa kesi yake kuhusu hayo, na Grace anapata mshauri wa kuzungumza naye. Anakutana na mshauri mara moja kila juma. Mkutano yao inakawiya, lakini Grace anaanza kujisikia vizuri. Kisha akaanza kujisikia wakujiamini zaidi katika mazingira yake mapya. Mambo yanaendelea!
Grace alifanya nini alipojisikia kuwa na woga? Vitu gani vingine Grace angelifanya kwa kukabiliana na marekebisho yake ya kiutamaduni? Kwa nini ilikuwa muhimu Grace apate msaada?

---

Wakati mwingine msongo ya mshtuko ya utamaduni unaweza kusababisha matatizo katika jamaa na hata vurugu nyumbani. Lazima utambuwe msongo unayo sikia, utambuwe inatokea wapi, na uendeleshe namna za kiafya za kukabiliana nayo.

***Tambua msongo yako ili uweze kuendelesha namna za kiafya za kukabiliana nayo. Na ukumbuke vitu viwili. Kwanza, mshtuko kiutamaduni ni ya kawaida. Wengine wengi wanajisikia jinsi unavyojisikia. Kitu cha pili, mambo yote yatakuwa mazuri!***

***Baadhi ya vitu gani ni ambavyo ulivifanya nchini mwako au katika nchi yako ya ukimbizi ulipojisikia wakusikitika?***



Utamaduni mbalimbali na watu mbalimbali wanakubaliana na mshtuko wa utamaduni katika njia tofauti. Labda umewahi kuwa na namna zako za kukabiliana na maisha kama vile:

- ❐ Kula vizuri, kufanya mazoezi, na kulala masaa zakutosha.
- ❐ Kukutana na marafiki au kuhudhuria mikutano ya jamii au ya utamaduni.
- ❐ Kuwa na malengo binafsi.
- ❐ Kuwasiliana na huduma za kidini.
- ❐ Kujisikia vizuri kwa kufurahia jambo wanalolipenda au kusikiliza muziki wanayopenda.
- ❐ Kujiunga na makundi za watu walitoka nchini mwako au kabila lako.

---

Ahmed alishangaa na jinsi ya haraka alijisikia na mushtuko wa utamaduni kisha kufika Marekani. Aliwakumbuka jamaa na marafiki yake, na kila kitu kilionekana kuwa kipya na hakukizowea. Hakuweza kulala vizuri, na alijisikia wakuchoka na asiyekuwa na furaha wakati wote. Kisha posho chache, Ahmed maneja wa kesi yake, na alimsaidia kupata mshauri wa kuzungumza naye. Ahmed alikuwa na woga ya kuzungumza juu ya jinsi alivyojisikia na mtu asiyemjua, lakini kisha siku chache alijisikia vizuri zaidi na mshauri na mambo yalikuwa bora. Nini ilikuwa ya muhimu kuhusu namna gani Ahmed aliishi jambo hii? Vitu gani vingine Ahmed angelifanya kwa kujisaidia?

---

***Chapa au andika kuhusu njia ambazo unaweza kutumia kwa kukabiliana na mshtuko utamaduni na mshtuko utamaduni.***

***Zungumza hii na mwenzako.***

**Mabadiliko ya nafasi ni moja ya jambo za msongo katika uhamiazi ya makao mapya.**

Poe Kyaw mtoto wa May Htoo alijiandikisha kwenye shule ya kati walipofika. Poe Kyaw alijuwa Kiingereza mbiyo zaidi kuliko mama yake. Poe Kyaw aliweza kutembea na May Htoo kwa kumsaidia kwa Kiingereza, na angeli tafsiri maelezo kutoka shule kwa May Htoo. Namna gani unafikiri May Htoo alijisikia kuhusu mabo hii? Halafu Poe Kyaw? Jambo hii ingelibadilisha uhusiano kati yao? Namna gani? Ungelifanya nini katika jambo hii?

## KUBADILI NAFASI KATIKA FAMILIA

Kwa wakimbizi wengi, moja ya changamoto kubwa Marekani ni mabadiliko ya nafasi. Baba, mama, vijana, watoto wadogo, na wazee, wote wanatambua kwamba maisha katika Marekani yanaweza kubadilisha uhusiano kati yao. Hii ni jambo la kawaida katika makazi mapya, lakini inaweza kusababisha matatizo mwanzoni.



Pradeep alikuja Marekani pamoja na binti yake mkubwa, mme wake, na watoto wao wadogo watatu. Pradeep alikuwa na shida kwa kujifunza lugha, hivyo hakutoka nyumbani sana. Pradeep alijisikia wakusikitika kwa sababu wajukuu wake hawakutaka kuzungumza lugha yao ya asili au kukaa naye na kusikiliza hadisi zake kuhusu maisha nchini mwao. Mara kwa mara walikosea hata wazazi wao adabu. Pradeep alipitia katika kipindi gani? Majukumu iko namna gani katika jamaa yao? Ungelikuwa Pradeep, ungelifanya nini?

***Katika chati ilio hapa chini chapa picha au andika majina ya watu ambao wataishi pamoja katika jamaa yako (peke yako pia) nchini Marekani. Kisha fikiri kuhusu majukumu yao ya zamani naya sasa katika jamaa. Fikiri jinsi majukumu ya jamaa inaweza kubadilika tena wakati mtaishi Marekani.***

| **Watu wa jamaa yako:** | **Majuukumu za watu hapa yalikuwa gani nchini mwako** | **Majukumu yao yalikuwa gani katika nchi ya ukimbizi?** | **Namna gani majukumu yanaweza kubadilika Marekani?** |
|---|---|---|---|
| *Kwa mfano: mzazi, mtoto, ndugu* | *Kwa mfano: mwanafunzi, mfanyakazi katika Jamaa, dada mkubwa, kaka* | *Kwa mfano: kupika, mkalimani, kaka mkubwa au dada mkubwa* | *Kwa mfano: mtoto ana kazi, mke anaenda kwenye shule ya kiingereza* |
| Mimi | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

**Wamerikani wanaamini kwamba kuna usawa wa jinsia kati ya wanawake na wanaume na wanaheshimu uwezo wa kuwa na uhuru kwa wote wawili, wanawake na wanaume.**

## WANAUME NA WANAWAKE



Wote wawili, mume na mke wanaweza kuwana matatizo kwa kujirekebisha katika kuchukua wajibu tofauti wanaume na wanawake nchini Marekani.

Wamarekani wanaamini kwamba kuna usawa kati ya wanawake na wanaume na wanaheshimu uwezo wa kujitegemea na uwezo wa kuwa na uhuru kwa wote wanawake na wanaume. Katika jamaa nyingi, mume na mke, wote wawili wanafanya kazi, na wanashirikiana katika majukumu ya kulea watoto.

Katika jamaa mbalimbali, mke anaweza kupata nshahara kubwa zaidi kuliko mumewe. Katika jamaa zingine, mke anaweza kupata kazi na mumewe asipate. Katika jamaa kama hii, mume anatarajiwa kulea watoto wakati hawako shuleni. Katika hali kama hizi, wakimbizi wamoja wanaweza kujisikia wamepoteza nafasi zao za uongozi katika jamaa. Wakimbizi wamoja wa kike wanaweza kujisikia kuwa na msongo wanapochukua majukumu mapya, kama vile, kupata mshahara kubwa ambayo jamaa inahitaji. Kuonesha msaada kwa mtu mwengine, pamoja na mawasiliano ya wazi na uaminifu, inaweza kusaidia kujenga maelewano zaidi na kupunguza msongo kati ya wazazi.

---

Adam na mkewe Fatima wanafanya kazi. Lakini kazi ya Fatima ina mshahara kubwa na inalipia jamaa bima ya afya. Wakati wa majira ya joto, Adam analazimishwa kuenda kazini kwa masaa madogo ili achunge watoto nyumbani. Ungelikuwa Adam, ungejisikia namna gani? Ungelichukua jambo hii namna gani? Ungejisikia kuchanganyikiwa, ungefanya nini?

---

## MAWAZO KUTOKA KWA WAKIMBIZI

“Ilikuwa lengo langu kuja Marekani, hivyo nilikuwa na furaha kweli kufika hapa.”

“Sisemi kamwe ‘hapa kila kitu ni kamilifu, kila kitu ni rahisi’ hapana. Maisha siyo rahisi, lakini angalau unajisikia salama. Unaweza enda kazini na kurudi salama. Baraka kubwa.”

***“Wakati ninafikiri jinsi maisha yangekuwa Marekani, nilikuwa na wasiwasi…Lakini nimekuwa nikiishi hapa kwa muda mrefu nimeanza kukabiliana na maisha ya hapa.”***

”Hapa, kama tunapata kazi na kuzungumza lugha, maisha itakuwa rahisi.”

“[Tu] lifikiri kwamba maisha itakuwa bora Marekani. Tulifikiri itakuwa bora, si kwa ajili yetu tu, lakini kwa watoto wetu pia. Kila kitu kimekuwa sawa hadi sasa.”

“Unajuwa, nchini mwetu, tunafanya vitu kwa kundi. Tunakula kwa kundi, tunafanya kazi…kwa kundi, na pia tunazungumza katika lugha ya asili. Pia ninakosewa na hayo.nakosewa na binamu yango, marafiki yangu. Kwangu mimi, si rahisi kuishi Marekani, lakini ni vizuri kwa jamaa yangu..

**Makazi mapya inawezakuwa vigumu kwa vijana wanapojirekebisha kwa maisha katika utamadunina mpya na kwa wakati huo huo wanatarajiwa kuendelea na maisha yao ya asili nyumbani na katika jamii zao.**

**Wakimbizi wazee wanaweza kujisikia wametengwa au kuwa peke yao wanapo pambana na shida za kujifunza lugha mpya na utamaduni mpya.**

## VIJANA



Makazi mapya inawezakuwa vigumu kwa vijana, hasa wanaokuwa kati ya miaka 13 na 20. Ni lazima wajirekebishe kwa maisha mapya katika utamaduni mpya, na wakati huo huo wanatarajiwa kuendelea na maisha yao ya asili nyumbani na katika jamii zao. Na inabidi wafanye hivi wakati wana mabadiliko ya umri kutoka hali ya kuwa kijana kwenda kuwa watu wazima.

Kwa sababu wanajifunza Kiingereza haraka zaidi kuliko wazazi wao, vijana wanaweza kuombwa kuwa watafsiri wa wazazi wao na wachukue majukumu mengine mapya. Mara kwa mara ni lazima waende shuleni na pia wafanye kazi. Wazazi wao wanaweza kujisikia kwamba hawana uwezo wa kuwasaidia watoto wao kwa sababu ya kutofahamu vizuri mfumo wa elimu ya Marekani.

***Jaribu ku kuelewa yale watoto wako wanapitilia ndani ili uweze kuwasaidia!***



Kwa kawaida vijana wajisikia hawawezi kueleza wazazi wao kuhusu wasiwasi katika maisha yao. Wakati wasiwasi hii inakuwa kubwa, vijana wamoja wanafanya mabo ambayo inaweza kuwaletea shida au wengine. Wanaweza kuanza kukosa shule, kujiunga na magengi, au kutumia madawa ya kulevya.  Uwahimize watoto wako kuzungumza na wewe kuhusu yale wanafanya na jinsi wanajikia. Pia, uwahimize kujiunga na shuguli za shule, kama vile michezo, au shuguli za jamii ambazo wanaweza kuwa na watu wengine wa umri wao. Hii inaweza kuwasaidia kuzoea bora mazingira yao mapya.

Bhim mtoto wa Balaram alikuwa kwenye shule la sekondari. Bhim alikuwa na marafiki na alikuwa akitumika vizuri shuleni. Alionekana kuwa na furaha. Lakini basi siku moja, jirani ya Balaram ambaye ni Mmerekani, Colleen, alimuambia Balaram kwamba aliona Bhim akirafikiana na watoto ambao wanaleta shida mara nyingi. Colleen alimushauria Balaram azungumze na Bhim kabla hayaanza kupata shida, pia. Ungekuwa Balaram, ungefanya nini?

***Uwahimize watoto wako kuzungumza na wewe. Utawaelewa zaidi!***



## WAZEE

Kubadilisha wajibu ni pia shida kwa wazee, ambao wanaweza kufikiri kwamba wamepoteza hali yao ya zamani ya kuwa watu wenye ujizi na uzoefu katika jamaa na jamii zao. Matatizo ya kujifunza lugha mpya na utamaduni mpya, pia changamoto ya kimwili yanaweza kusababisha wazee kujisikia wanatengwa na kuwa peke yao. Wazee wanaweza kuona kwamba hawana tena nafasi ya heshima katika jamii.

Wazee wanaweza pia kukabiliana na changamoto za kiuchumi. Baadhi ya wakmbizi wazee ambao walitarajia kuacha kazi na kupata pensheni wanaweza wakajikuta kwamba wanahitaji kazi, hasa kama wana umri chini ya miaka 65. Wakimbizi wenye umri zaidi ya miaka 65 wanaweza kutambua kwamba malipo kwa wale walioacha kazi hayalingani na matarajio yao, na kwamba faida ya walemavu hayawezi kugharamia malipo ya daktari, naya kwamba jamaa yao haiwezi kuwahudumia kama wanavyohudumiwa nchini mwao.

Alaso alikuwa na umri wa miaka 61 na alikuwa ameachakazi tangu myaka mingi wakati alijiunga na watoto wake waliyo kuwa watu wazima Marekani. Alaso alijua ya kwamba jamaa ya mtoto wake wa kiume haikukuwa na pesa ya kutosha. Walipata kwa shida pesa ya kulipa malipo yao. Pia alishangaa ya kwamba hangeweza kupata msaada ya serikali. Je, serikali ilijuwa ya kwamba amekwisha kuacha kazi? Ungejisikia namna gani ungekuwa Alaso? Ungefanya nini?

Matatizo haya yote ya uchumi yanaweza kusababisha unyonge na mambo mengine ya afya ya akili kwa mzee. Watiye moyo wazee kushiriki katika shuguli na kuzoweyana na wengine, kwa mfano, kwa kuhudhuria darasa la Kiingereza, itawasaidia kuwa na nguvu na kushiriki.

***Wakimbizi wazee wengi wanaishi maisha ya furaha sana nchini Marekani na wanafanya urafiki na kubaki katika ushiriki katika shuguli za jamaa na jamii.***

**Kama wewe au mmoja wa jamaa yako hajawahi kujisikia hawezi kukabiliana na matatizo ya maisha yenu mpya Marekani, tafuta msaada mara moja.**

***Rudilia chati kuhusu jamaa kwa ukarasa wa 135. Kulingana na na habari zilizoelezwa, unaweza kutambua jukumu nyingine au tofauti yoyote ambayo wewe au mwengine wa jamaa yako anaweza kuipata Marekani? Rudilia chati kama inavyo hitajika.***

***Namna gani jamaa yako inaweza kusaidiana kupitia mchakato wa makazi mapya?***

## KUTAFUTA MSAADA



Kama wewe au mtu mwingine wa jamaa yako mnajisikia hamwezi kukabiliana na matatizo ya maisha yenu mpya Marekani, tafuteni msaada mara moja. Zungumza kuhusu maswala ya majukumu mapya ya jamaa kwenye madarasa ya kujirekebisha kiutamaduni au pamoja na mtumishi wa kesi yako nchini Marekani. Shirika lako la makazi mapya yanaweza kutafuta huduma ambazo zitakusaidia kupata ujuzi wa kukabiliana na shida hizi na kukupatia uwezo wa kukabiliana na hali za matatizo nyumbani.

***Fikiri kuhusu jinsi gani unaweza kuomba msaada unapojisikia kuchanganyikiwa au una woga Katika jukumu ya kucheza na mwengine, eleza jinsi unajisikia na uombe msaada.***

- ❒ Mtu 1: Jambo! Habari za leo?
- ❒ Mtu 2: Sijisikii vizuri leo.
- ❒ Mtu 1: Nini haiendeki?
- ❒ Mtu 2: Nasikia huzuni.
- ❒ Mtu 1: Nasikitika kusikia hayo. Nini inakusikitisha?
- ❒ Mtu 2: Nakumbuka jamaa yangu.

***Kama unamatatizo yakuonyesha jinsi unajisikia, angalia kiambatisho C sura za mhemuko kwa ukarasa wa 226 kwa uongozi mbali mbali mbalimbali.***

## KAMILISHA*

***Chagua jibu bora zaidi kwa maswali hapa chini ukifanya chaguo bora.***
***Hii ni mfano***:

*Lugha gani ndio inazungumzwa na watu wengi zaidi Marekani?*

a. Kichina.

(b.) Kiingereza.

c. Kiugerumani.

***Watu wengi Marekani wanazungumza kiingereza. Kwa hiyo jibu ni b. Kiingereza.***

1. Kujirekebisha kikamilifu kwa jamii yako mpya inaweza kuchukua miaka 2 hadi 5.

   a. Kweli.

   b. Uwongo.

2. Gani ya yafuatayo ni njia unaweza kukabiliana na msongo na mshtuko utamaduni?

   a. Kuchangia chakula na marafiki.

   b. Kuhudhuria ibada ya kidini.

   c. Kusikiliza mziki waku furahisha.

   d. Kujifungia katika chumba chako kwa siku tatu.

   e. Chaguo a, b, na d/au c inaweza kuwa njia ya afya ya kukabiliana na msongo na mshtuko utamaduni.

3. Mazungumzo ya wazi na uaminifu kati ya watu wa jamaa moja itaweza kusaidia mchakato wa kujirekebisha kuwa rahisi.

   a. Kweli.

   b. Uwongo.

---

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 221.

4. Kama mshtuko utamaduni, jinsi gani unaweza kujisikia?

    a. Hasira.

    b. Kusikitika?

    c. Furaha.

    d. Kutosikia hamu ya kula.

    e. Chaguo a, b, na/au d.

5. Nani anaweza kupata mabadiliko ya majukumu katika jamaa nchini Marekani?

    a. Wanaume na wanawake.

    b. Vijana.

    c. Wazee.

    d. Yote ya juu?

11




# Sura Ya Kumi Na Moja
## HAKI NA MAJUKUMU CHINI YA SHERIA NCHINI MAREKANI

Sheria ya Marekani zinawekwa kwa kuhifadhi haki za watu, na inabidi ujue haki zako za kisheria na majukumu yako.

---

### Sura Hii Itajadili

» Haki zako na Majukumu yako.
» Sheria za Marekani ambazo inabidi uzijuwe
» Hali yako ya kisheria na Uraia wako.


**Sheria za Marekani zinawekwa kwa kulinda haki za watu Marekani.**



## MANENO MUHIMU YA KIINGEREZA

Maneno ya kiingereza yafuatayo yanatumiwa wakati wa kuzungumza kuhusu haki na majukumu chini ya sheria ya Marekani. Maneno haya na misemwa haya yatakuwa na mafaa kwako kuyajifunza.

***Sema neno katika Kiingereza, andika lugha yako ya asili. Kisha, chapa picha ya neno, andika maana yake, au uitumiye katika msemo. La kwanza limefanyika kwa ajili yako.***

| Katika lugha yako | Katika Kiingereza | Chapa picha ya neno, andika maana yayo, au uitumiye katika msemo. |
|---|---|---|
| *mahakama* | court |  |
| | judge | |
| | jury | |
| | law | |
| | law office | |
| | lawyer or attorney | |
| | legal clinic | |
| | responsibilities | |
| | rights | |
| | U.S. Constitution | |

**Kama mkimbizi, una haki sawa na mtu yeyote mwengine anayeishi Marekani.**

**Nchini Marekani, unaweza kuazibiwa kama unavunja sheria, hata kama haukujua kuhusu sheria unayoivunja.**

*Ulikuwa na haki gani nchini mwako au katika nchi yako ya ukimbizi? Majukumu yako yalikuwa gani? Zungumza na mwengine kuhusu sheria na majukuku hizi.*

## HAKI ZAKO



Kama mkimbizi, una haki sawa na mtu yeyote mwengine anayeishi Marekani. Haki hizi ni pamoja na uhuru wa kutoa maoni yako, uhuru wa dini, uhuru wa kuhudhuria mikutano. Wakazi wote wa kisheria wa Marekani, wakiwemo wakimbizi, wanahaki sawa na wengine kwenye mambo ya ajira, nyumba, elimu na kupata huduma za serikali.

### ULINZI KINYUME CHA UBAGUZI

Sheria ya Marekani hairuhusu ubaguzi kwa kuangalia asili ya mtu, dini yake, au kabila lake. Kama unabaguliwa au unaimwa haki zako kwa sababu ya namna unavyo onekana ama kwa sababu ya lugha unayo zungumza, una haki ya kupata ulinzi wa kisheria.

Patricia ni tayari kuhama kwenye nyumba kubwa na amezungumza na jirani mwenye nyumba kuhusu nyumba. Mwenye nyumba anamwambia Patricia ya kwamba hawezi kuishi katika fleti hiyo kwa sababu hawapangishi wakimbizi. Patricia anauliza, kwa sababu gani, na mwenye nyumba anamueleza ya kwamba alipata shida na jamaa ya wakimbizi miaka michache iliyopita. Kwa nini huu ubaguzi? Patricia anaweza kufanya nini?

## ASIYEKUWA NA KOSA MPAKA KUTHIBITISHWA KUWA ALIYEFANYA KOSA

Kama unashtakiwa na kosa nchini Marekani, unaendelea kuishi kama mtu asiyekuwa na kosa mpaka idibitishwe ya kwamba ulifanya kosa. Una haki ya kupata mwanasheria ambaye atakuwakilisha mahakamani. Kama hauna uwezo wakupata mwanasheria, mahakama italipa moja wa kukuwakilisha.



***Fikiri kuhusu haki na majukumu nchini Marekani badala ya nchini mwako au nchi yako ya ukimbizi.***

- ❒ Namna gani sheria za Marekani zinafanana na hizo za nchi yako?
- ❒ Tofauti ni gani?
- ❒ Namna gani majukumu yanafanana?
- ❒ Tofauti ni gani?

***Zungumza kuhusu kufanana na tofauti pamoja na mwenzako.***

# MAJUKUMU YAKO



Nchini Marekani, unaweza kuazibiwa kama unavunja sharia, hata kama haukujua kuhusu sheria unayoivunja. Hukumu ya baaddhi ya makosa ni kurudishwa nchini mwako. Kwa sababu hii ni vema sana kujifunza na kuheshima sheria.

Kuna aina tatu za sheria nchini Marekani:

**SHERIA ZA SERIKALI,** kama vile sheria kinyume na uuzaji wa dawa za kulevya ambazo zinahukumu kila mtu anayeishi Marekani.

**SHERIA ZA MAJIMBO** zinatofautiana kutokana na jimbo moja hadi jimbo lingine. Kwa mfano, kwenye baadhi ya majimbo unaweza kupata leseni ya kuendesha gari ukiwa na umri wa miaka 16, kwenye majimbo mengine lazima uwe na umri wa miaka 18.

**SHERIA ZA MAHALI UNAPOKAA** ni sheria zinatumiwa katika mji au mkoa fulani.

# 11 HAKI NA MAJUKUMU CHINI YA SHERIA NCHINI MAREKANI

**Marekani, watu wanaweza kuto kunywa au kununua pombe mpaka watimize umri wa miaka 21.**

**Ni kinyume cha sheriya kuwaacha watoto bila ukingo.**



***Utahitaji kuelewa sheria za Marekani kwa sababu mengi zao ni tofauti na sheria katika nchi yako, hapa chini kuna mambo muhimu unapaswa kujua kuhusu sheria za Marekani.***

| Sheria kuhusu: | Maelezo kuhusu sheria: | Kulikuwa sheria yenye kufanana kati ya nchi yako au nchi yako ya ukimbizi? |
|---|---|---|
|  Madawa ya kulevya | Ni kinyume cha sheria kununua, kuuzisha, au kutumia aina mbalimbali ya madawa ya kulevya kama vile heroini, na kokeini. Ukivunja sheria hii unaweza rudishwa nchini mwako. | |
|  Kuvuta sigara | Katika majimbo mengine, ni kinyume cha sheria kuvuta sigara kwenye maeneo ya umma kama vile majengo ya sinema au afisi, na pia katika migahawa. Kama unavuta sigara, uliza shirika lako la makazi mapya kuhusu sharia hizi katika eneo lako. | |
|  Pombe | Marekani, watu wanaweza kuto kunywa au kununua pombe wanapofika umri wa miaka 21. Mahali pengi, hairuhusiwe pia kunywa pombe kwenye njia au nje, kutosha kwenye mahali sahihi kama vile baa au migahawa. Pia, kuendesha gari wakati mtu analewa (DUI) unaweza kunyanganywa leseni yako, na/au kuwekwa jela. | |
|  Kutembeza gari | Ni kinyume cha sheria kutembeza gari kama hauna leseni ya Marekani au kama umekunywa pombe. Pia, majimbo mengi yana sheria kuhusu utumiaji wa mikanda ya viti kwenye gari. Wazazi wanatakiwa wawafunge watoto wao mikanda na watumie viti maalum vya usalama. Kuna sheria za mikanda kwa watu wazima pia. | |

| Sheria kuhusu: | Maelezo kuhusu sheria: | Kulikuwa sheria yenye kufanana kati ya nchi yako au nchi yako ya ukimbizi? |
|---|---|---|
|  Kuwa na wa bibi wengi | Kuowa zaidi ya mpenzi mmoja (polygamy) hairuhusiwi na sheria. | |
|  Kutesa kimwili | Ni kinyume cha sheria kumtesa mtu kimwili (kupiga mtu) mke wako au watoto wako. Shirika la ulinzi wa watoto linaweza kumchukua mtoto wako na kumtoa nyumbani mwako. | |
|  Ulinzi wa watoto | Ni kinyume cha sheria pia kuacha watoto wako bila ukingo. Ingawa majimbo machache sana yanaweka umri wa kisheria kuwa mtoto anaweza kuachiwa nyumbani peke yake, watoto wa karibu umri wa miaka 12 hawapaswi achiwa nyumbani peke yao. Katika nchi mbalimbali, watoto wakubwa wanawa linda watoto wadogo, lakini nchini Marekani, watoto wadogo lazima wasimamiwe na mtu mzima. Kuacha mtoto peke yake inachukuliwa kama upuuzi na inaweza kusababisha kuondolewa kwa mtoto na shirika la ulinzi wa watoto. | |
| Mapenzi na watoto & unyanyasaji wa kijinsia | Mapenzi na watoto (wowote chini ya umri wa miaka 18) katika majimbo mengi ni kinyume cha sheria. Unyanyasaji wa kijinsia na mtoto inaweza kusababisha hukumu wa kufungwa na kuridishwa nchini mwako. | |

| Sheria kuhusu: | Maelezo kuhusu sheria: | Kulikuwa sheria yenye kufanana kati ya nchi yako au nchi yako ya ukimbizi? |
|---|---|---|
|  Unyanyasaji wa kijinsia | Maoni ya kushambulia au matendo ya aina ya kijinsia katika eneo la kazi (unyanyasaji wa kijinsia) ni kinyume cha sheria. | |
|  Silaha | Kuna sheria ambazo zinadhibiti kununua, kuuzisha, na matumizi ya silaha za moto. Sheria hizi ni tofauti kulingana na majimbo. | |
|  Kuwinda wanyama na kuvua samaki | Katika maeneo mengi, ni kinyume cha sheria ku winda wanyama au kuvua samaki bila leseni. | |
|  Mazingira na mbuga ya asili | Kuna sheria za kulinda mazingira na mbuga ya asili. Kwa mfano, katika baadhi ya mbuga, ni kinyume na sheria ku washa moto wala kuvuta sigara. Katika mbuga zote, lazima wafanya kambi wachukuwe uchafu wao wakati wanaondoka. | |
|  Ukali kwa wanyama | Majimbo mengine yana sheria ya kulinda wanyama na tiba kali. Uliza shirika lako la makazi mapya kuhusu sheria katika eneo lako. | |

# SURA YA KUMI NA MOJA 11

***Jadiliana na mwengine kuhusu sheria za Marekani zilizo jadiliwa kwenye ukarasa uliopita..***

- ❒ Gani inaweza kuwa rahisi kwako kufwata?
- ❒ Gani inaweza kuwa vigumu zaidi?

***Fikiri kuhusu matukio yafuatayo:***

---

Othman anafunga bangi katika mfuko yake kabla ya kusafiri Marekani. Wakati alifika kwa bandari ya kuingia, bangi ilikamatwa na Othman alipelekwa katika chumba cha kuulizwa maswali. Othman alijua ya kwamba hangeweza kuleta dawa za kulevya Marekani, lakini hakujua kwamba bangi ilikuwa kinyume cha sheria Marekani. Nini Othman angefanya kabla yakuja Marekani?

---

Nway Meh ana watoto vijana watatu. Kuna majirani pembeni, alafu, Nway Meh anawaacha watoto wake katika maegesho karibu na nyumba yake ili wacheze wakati anaenda kwenye duka. Siku moja anarudi nyumbani anakuta polisi hapo. Anamuuliza Nway Meh kwa sababu gani watoto waliachwa bila ulinzi. Nway Meh haelewi. Kuna majirani wengi pembeni. Shida ni gani hapa? Lazima Nway Meh afanye nini ili aheshimu sheria za Marekani kuhusu ulinzi wa watoto na upuuzi?

---

Ebaid amenunua mbuzi kwa wakulima, na kuileta katika nyumba yake. Anaichinjia katika kiwanja chake na anawakaribisha majirani zake kuchangia nyama ya mbuzi. Lakini polisi inakuja na kuomba Ebaid aondoe mbuzi kutoka kiwanja. Tatizo ni gani? Nini Ebaid alifanya vibaya?

---

Naw Baw alikuwa akiloa katika ziwa karibu na nyumba yake. Polisi alimueleza ya kwamba hairuhusiwi kuloa hapo. Alitupa samaki alizoziloa na akampa faini. Naw Baw alisema hatafanya hayo tena, na alimuomba askari osimpe faini kwa sababu hakukuwa na jua ya kwamba hawezi kuvua katika ziwa hiyo. Unafikiri polisi alimujibu namna gani?

---

**Mwaka wako wa kwanza Marekani, utakuwa na hali ya kuwa mkimbizi.**

**Wakati una hali ya mkimbizi, huwezi kusafiri nje ya Marekani bila ruhusa.**

## HALI YAKO YA KISHERIA NA URAIA WAKO

### HALI YA KUWA MKIMBIZI

Mwaka wako wa kwanza Marekani, utakuwa na hali ya kuwa mkimbizi. Wakati huu ni lazima uchukue nakala ya kadiyako ya I-94 na kadi ya EAD wakati wote kama ushahidi wa hali yako halali ya kuwa Marekani. Kama mkimbizi, unaweza kufanya mambo yafuatayo:



- ❒ Kusafiri popote nchini Marekani. (kumbuka ya kwamba, ukihama, lazima ujulishe huduma za uraia na uhamiaji wa Marekani ndani ya siku 10 kisha kubadilisha anwani yako).
- ❒ Kununua nyumba.
- ❒ Kufanya kazi
- ❒ Kwenda kwenye shule.
- ❒ Kufadhili mume au mke wako, na watoto wako ambao wana umri chini ya miaka 21. Ukitaka mke au mume wako au watoto wako waje kukaa pamoja nawe Marekani, shirika lako la makazi mapya litakueleza mambo na taratibu zinazotakiwa.

***Fikiri kuhusu haki hizi. Namna gani ni tofauti na haki ulizokuwa nazo kabla ya kufika Marekani? Chapa dhuara kwa hizo zitakazo kuwa za mafaa kwako na kwa jamaa yako.***

## MAMBO HUWEZI KUFANYA WAKATI UKO MKIMBIZI

Wakati uko mkimbizi, hauwezi kupata pasipoti ya Marekani, kujiunga na jeshi, kupiga kura wakati wa uchaguzi, au kuajiriwa kwenye kazi za serikali zinazohitaji raia wa Marekani. Wakati una hali ya kuwa mkimbizi, hauwezi kusafiri nje ya Marekani bila ruhusa kutoka huduma za uraia na uhamiaji wa Marekani. Kama ni lazima usafiri nje ya Marekani, shirika lako la makazi mapya litakueleza namna gani utapata ruhusa hiyo. Ukirudia katika nchi yako ya asili, unaweza kutoruhusiwa kuingia tena Marekani.

---

Kwa mkutano wa kwanza wa Saw Eh Do na mshauri wa ajira, mshauri anamuuliza Saw Eh Do aina gani ya kazi angetaka kuomba. Saw Eh Do anasema anataka kuwa askari kama baba yake na mjomba wake walipokuwa nchini mwao. Nini mshauri wa ajira anamuambia Saw Eh Do? Je, Saw Eh Do anaweza kujiunga na askari jeshi la Marekani? Kwa sababu gani anaweza au hawezi? Ataweza kujiunga na askari jeshi ya Marekani siku moja?

---

## HUDUMA YA CHAGUO



Wanaume wote nchini Marekani wenye umri kati ya 18 na 25 lazima wajiandikishe na shirika la serikali linalowachagua watu kwa huduma za kiaskari, kwa kawaida wakati wa vita. Hii pia inafanyika kwa wakimbizi wanaume. Kwa wakati huu, wanajeshi wote wa jeshi la Marekani ni watu wanaojitolea. Watu wasiojiandikisha wanaweza kuwa na shida ya kupata hali ya ukazi wa kudumu na kupata uraia.

---

Wakati Leonce, mtoto wa Thom alitimiza umri wa miaka 18, alikuwa na msisimko ya kuwa sasa mtu mzima. Leonce anamuambiya Thom kuhusu haki zake za kuwa mtu mzima nchini Marekani. Ungelikuwa Thom, nini ungemwambia Leonce kuhusu majukumu zake?

---

**Kisha mwaka moja nchini Marekani, lazima uombe kuwa mkaji wa kudumu (LPR).**

## MAKAZI YA KUDUMU





Kisha mwaka moja nchini Marekani, lazima uombe kuwa mkaji wa kudumu (LPR), au mwenye kadi ya kijani. Wakazi wa kudumu wanaweza kusafiri nje ya Marekani (hata kama si vizuri kubaki nje ya nchi kwa muda wa zaidi ya mwaka moja) na wanaweza kujiunga kwenye jeshi la Marekani, lakini hawawezi kupiga kura wakati wa uchaguzi wa Marekani au kuwa na kazi za serikali ya Marekani ambazo zinahitaji wafanyakazi walio waraia. Shirika lako la makazi mapya litakueleza namna gani unaweza kuwa mkazi wa kudumu.

---

Leyla amekuwa Marekani kwa miezi 9, na anajua ya kwamba itamubidi kuomba makazi ya kudumu hivi karibuni. Lakini yeye hajui namna gani kuyafanya. Lazima Leyla azungumze na nani kwa kupata habari zaidi kuhusu kuomba makazi ya kudumu?

---

## URAIA




Kisha kukaa Marekani muda wa miaka 4 na miezi 9, unaweza kuomba kuwa raia. USCIS au shirika lako la makazi mapya linaweza kukueleza mambo yanayotakiwa kwa kuwa raia. Pamoja na mambo mengine, lazima uoneshe unatabia nzuri na unaujuzi wa kimsingi wa lugha ya Kiingereza pamoja na historia ya serikali ya Marekani. Wahamiaji na wakimbizi wanaopata uraia haki na bahati kama raia waliozaliwa nchini Marekani.

***Andika au chapa katika dhuara zilizo hapa chini kwa ukarasa ufwatayo kwa kuonesha haki mbalimbali ambazo utakuwanazo nchini Marekani wewe kama mkimbizi. Andika au chapa katika mraba pembeni ya dhuara kwa kuonesha majukumu mbalimbali utakuwa nazo.***

### HAKI:

***Kama vile ulinzi kutoka ubaguzi au kusafiri popote Marekani.***

### MAJUKUMU:

***Kama vile kujifunza na kuheshimu sheria au kuhakikisha ya kwamba watoto wana ulinzi.***

## KAHI NA MAJUKUMU KULINGANA NA HALI YA UHAMIAJI*

***Katika chati iliyo hapa chini na kwa ukarasa ufwatayo, onesha haki na majukumu za mtu kulingana na hali mbalimbali unazo za uhamiaji nchini Marekani.***

| | **Mkimbizi** | **Mkaji wa kudumu (LPR)** | **Raia** |
|---|---|---|---|
| Kuitikiwa | Kisha kufika Marekani | Kisha kuomba, kisha mwaka 1 | Kisha kuomba, kisha miaka 4 na miezi 9 |
| Nyaraka | I-94 | I-551 au kadi ya kijani | Pasipoti ya Marekani |
| **HAKI** | | | |
| Kuomba muungano wa jamaa | | | |
| Kuomba msaada wa umma | | | |
| Kwenda shuleni na kufanya kazi | | | |
| Kusafiri kwa uhuru ndani ya Marekani | | | |
| Kusafiri nje ya Marekani bila ruhusa | | | |
| Kupiga kura | | | |

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 222.

| | **Mkimbizi** | **Mkaji wa kudumu (LPR)** | **Raia** |
|---|---|---|---|
| **MAJUKUMU** | | | |
| Kujua kutii sheria | | | |
| Kulipa kodi | | | |
| Kujiandikisha kwa ajili ya uchaguzi kama raia mwanaume kati ya umri wa miaka 18 na 25 | | | |
| Kuheshimu haki za wengine | | | |
| Kuwa muamuzi katika mahakama | | | |
| Kushugulikia na kulinda watoto wako | | | |

## KAMILISHA*

Kweli au uongo? Kwa kiasi gani unafikiri unajua kuhusu makazi mapya nchini Marekani? Pima ufahamu wako na maswali zilizo hapa chini. Soma maswali hii na chapa dhuara kwa neno **Kweli** ikiwa unafikiri ni kweli na chapa dhuara kwa neno **Uongo** ikiwa inafikiri si kweli.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Kama mkimbizi, una haki sawa na mtu yeyote mwengine anayeishi Marekani. | **Kweli** | **Uongo** |
| 2. | Nchini Marekani, unaweza kuazibiwa kama unavunja sheria, hata kama haukujua kuhusu sheria unayoivunja. | **Kweli** | **Uongo** |
| 3. | Kuvuta sigara inaruhusiwa kwenye maeneo ya umma. | **Kweli** | **Uongo** |
| 4. | Katika maeneo mengi, ni kinyume cha sheria ku winda wanyama au kuvua samaki bila leseni. | **Kweli** | **Uongo** |
| 5. | Kuowa zaidi ya mpenzi mmoja wakati moja inaruhusiwa Marekani. | **Kweli** | **Uongo** |
| 6. | Kisha mwaka moja nchini Marekani, mkimbizi ambaye anachagua kubaki nchini lazima aombe kuwa mkaaji wa muda. | **Kweli** | **Uongo** |
| 7. | Wanaume wa umri kati ya 18 na 25 wasio jiandikisha na huduma za kujitolea wanaweza kuwa na shida ya kupata hali ya ukazi wa kudumu na/au kupata uraia. | **Kweli** | **Uongo** |
| 8. | Unaweza kuomba uraia kisha miaka 2 nchini Marekani. | **Kweli** | **Uongo** |

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 222.



12

# Sura Ya Kumi Na Mbili
## KAZI

Kutafuta kazi itakuwa moja katika mambo muhimu utakayofanya baada ya kuwasili nchini Marekani. Wamarekani wanaamini kwamba lazima watu wazima wafanye kazi utakayofanya na kutegemea jamaa yao, na wasitegemee msaada wa fedha kutoka kwa serikali. Kwasababu msaada wa serikali ni wa muda na wa kiasi ya pesa ndogo, kupata kazi haraka iwezekananvyo ni muhimu sana

---

### Sura Hii Itajadili

» Kupata kazi
» Mshahara
» Mafanikio kazini

**Lazima kupata kazi haraka iwezekanavyo kwa sababu msaada wa serikali ni wa muda.**

## MANENO MUHIMU YA KIINGEREZA

Maneno ya kiingereza yafuatayo yanatumiwa wakati wa kuzungumza kuhusu kazi nchini Marekani. Maneno haya na misemwa haya yatakuwa na mafaa kwako kuyajifunza.

***Sema neno katika Kiingereza, andika lugha yako ya asili. Kisha, chapa picha ya neno, andika maana yake, au uitumiye katika msemo. La kwanza limefanyika kwa ajili yako.***

| Katika lugha yako | Katika Kiingereza | Chapa picha ya neno, andika maana yayo, au uitumiye katika msemo. |
|---|---|---|
| *Karatasi ya kuomba kazi* | application | *Yi Yi anajaza karatasi ya kuomba kazi katika benki.* |
| | career | |
| | employee | |
| | employer | |
| | employment | |
| | full-time job | |
| | job | |
| | part-time job | |
| | résumé | |
| | salary | |
| | volunteer | |

**Kupata kazi yako ya kwanza inaweza chukua majuma au miezi, kwa hivyo ni vizuri kuitika kazi ya kwanza inayo tolewa kwako.**

**Kujifunza Kiingereza inakusaidia kupata kazi.**

**Wakimbizi wanaanza kazi ya kiwango cha kwanza.**

## KUPATA KAZI

Wakati unatafuta kazi, kumbuka haya yafwatayo:



- ❐ Kupata kazi yako ya kwanza inaweza chukua siku kidogo au muda mrefu kama miezi mingi. Kwa sababu ya hii, lazima uanze kutafuta kazi mara moja.
- ❐ Utategemewa kufanya kazi yoyote ya kwanza utakayopata, hata kama haina mshahara kubwa au kama si sawa na kazi yako ya zamani uliyokuwa nayo.
- ❐ Kuna watu wengi wenyi kuomba kazi moja kwa wakati moja, kwa hivyo ni muhimu kuwa tayari kukubali kazi katika utaalamu upya.
- ❐ Serikali au shirika lako la makazi mapya hawawezi kuhakikisha kwamba utapata kazi.
- ❐ Huduma za kuajiriwa za wakimbizi zitakusaidia katika juhudi zako za kutafuta kazi, lakini huwezi kupata kazi kama wewe mwenyewe hauna juhudi.
- ❐ Wakimbizi ambao wanaacha kazi wanaweza kupoteza msaada wa serikali.
- ❐ Kujifunza kiingereza inaweza kukusaidia kupata kazi. Waajiri wengi wanatafuta watu ambao wanaweza kuzungumza, kusoma, na kuandika katika lugha ya kiingereza.

---

Gori Maya anachukua kazi ya kwanza anayotolewa. Haipendi kazi yake, lakini anajifunza kiingereza na anamarafiki wazuri. Anapo omba kazi mpya kisha miaka miwili, Gori Maya anaweza kujibu kwa Kiingereza, na sasa anawatu anaowajua. Namna gani kuitika kazi ya kwanza imesaidia Gori Maya?

---

# SURA YA KUMI NA MBILI 12


## AINA ZA KAZI

***Fikiri kuhusu kazi uliyokuwa nayo zamani.***

- ❒ Ilikuwa aina gani ya kazi?
- ❒ Ujuzi gani ulihitaji kwa kuchaguliwa kwa kazi hiyo?

Nchini Marekani, kuna aina tatu kubwa za kazi: kazi za kiwango cha kwanza, kazi za ufundi, na kazi za taalimu au ubingwa.

***Patanisha picha ya mfano ya aina ya kazi iliyo kushoto na maelezo sahihi zaidi yaliyo kuume.***



1. Kazi za kiwango cha kwanza

a. Hizi zinahitaji kwa kawaida diploma ya chuo kikuu, kujuwa Kiingereza zaidi, na kiwango cha juu cha ujuzi. Kazi hizi zinalazimisha kwa kawaida kuwa na leseni au cheti. Mengi ya kazi hizi zinalipa mshahara kwa mwaka au kwa mwezi badala ya mshahara kwa saa.



2. Kazi za ufundi

b. Kazi hizi zinahitaji mafunzo kidogo au uzoefu ndogo. Kazi hizi zinalipa mshahara kwa masaa na hazihitaji kiwango cha juu cha ujuzi wa lugha ya kiingereza. Wakimbizi wengi wanafanya kazi hizi wakisoma Kiingereza au wakijifunza ujuzi wengine.



3. Kazi za taalimu au ubingwa

c. Hizi zinahitaji mafunzo, kiwango cha juu cha ujuzi wa lugha ya Kiingereza, na kiwango fulani cha ujuzi wa kazi hiyo. Kazi hizi zinalipa mshahara, kwa masaa au kwa wiki, ambao ni kubwa kuliko mshahara wa kazi za kiwango cha kwanza, na ni kubwa hata kuliko kazi za taalimu au ubingwa.

**Wanaume na wanawake wanafanya kazi pamoja mahali pa kazi nchini Marekani na mara kwa mara wanawake wanawasimamia wanaume kazini.**

***Fikiri kuhusu maswali yafwatayo:***

- ❐ Jinsi gani unaweza kujisikia kuhusu kufanya kazi katika aina mbalimbali za kazi?
- ❐ Aina gani ya kazi itakuwa rahisi kwako kupata?
- ❐ Ni gani itakuwa ngumu?
- ❐ Jinsi gani unajisikia kuhusu ya kwamba kazi ya kwanza wakimbizi wanapata ni kazi ya kiwango cha chini?
- ❐ Unaweza zungumza na nani kama kazi yako inakuwa ngumu? Utaweza kufanya nini?

---

Baada ya kufika Marekani, Mohammed alikutana na Claire, mshauri wa ajira, Claire alimuonyesha Mohamed ya kwamba aombe kazi kama zamu. Mohamed hanawazo ya kuomba kazi ya aina hii na anakatala. Kisha miezi tatu Mohamed anamtembelea Claire kwasababu hawezi kupata kazi. Kazi ya zamu ilisha chukuliwa na mutu mwingine, lakini Claire anamuambia atamujulisha Mohammed kama anasikia kuna nafasi ingine. Kwa nini ni muhimu kuitika kazi ya kwanza inayo patikana ni vizuri? Kwa nini ni vizuri kuwa tayari kuitika kazi yoyote?

---

## WANAWAKE NA WANAUME KAZINI



Marekani, wanawake na wanaume, wote wanafanya kazi. Nusu ya wafanyakazi ni wanawake, na wanafanya kazi sawa na wanaume na kwenye viwango vya kazi, mara kwa mara wanasimamia wafanyakazi wa wanaume.

---

Khin Myint anajisikia kwamba majibu yake kwa kazi yalikuwa mazuri, na anafurahi anapopokea simu yakumujulisha kama alipata kazi. Lakini hakutambua ya kwamba mkubwa wake wa kazi atakuwa mwanamke. Zamani, alifanya kazi na wanaume tu. Ungelikuwa Khin Myint, ungelijisikia namna gani? Lazima Khin Myint afanye nini?

---

***Fikiri kuhusu mawazo ya wanaume na wanawake kutumika pamoja.***

- ❒ Katika nchi yako au nchi yako ya ukimbizi, ilikuwa ya kawaida wanaume na wanawake kufanya kazi pamoja?
- ❒ Unafikiri unaweza kujisikia namna gani kama unafanya kazi ambapo wanaume na wanawake wanafanya kazi pamoja? Inaweza kuwa vigumu kuyazoweya?
- ❒ Kama ni vigumu kuzowea, atazungumza na nani kuhusu hayo?

---

Aisha hajawahi kufanya kazi pengine kuliko nyumbani. Anaitika kazi ya kuweka biashara katika mifuko dukani, na anatambua ya kwamba anapashwa kufanya kazi pamoja na wanaume wengi kila siku. Haya yanasababisha Aisha kujisikia na wasiwasi sana. Ungelikuwa Aisha, ungelifanya nini? Ungelijisikia namna gani kuhusu kufanya kazi na mtu wa jinsia tofauti?

---

## WATOTO KAZINI



Nchini Marekani, watoto wa umri karibu 14 wanaweza fanya kazi za muda, lakini wanaweza kulazimishwa kufanya kazi kwa masaa madogo. Vijana wengi nchini Marekani, wanafanya kazi za muda jioni baada ya shule, siku za wikendi, na wakati wa mafungo.

***Fikiri kuhusu itakuwa je kwa watu wafwatao wa jamaa yako kama wanafanya kazi Marekani.***

| Watu wa jamaa yako: | Jinsi gani majukumu ya jamaa yatabadilika kama mtu huyu anafanya kazi? |
|---|---|
| Wewe | |
| Mpenzi wako | |
| Watoto wako | |
| Baba na Mama mkwe wako | |
| Ndugu zako | |

**Mahali za kuchunga watoto wadogo wakati wazazi wote wawili wanafanya kazi, au jamaa ya mzazi mmoja anafanya kazi.**

Mwalimu wa Dinesh anafikiri ya kwamba lazima achukue madarasa ya mafungo ili aweze kuelewa zaidi, lakini, Dinesh anataka kufanya kazi ya magungo ili aweze kusaidia jamaa yake. Jinsi gani ungeweza kushugulika na hali hii? Ungelikuwa mzazi wa Dinesh ungelimuambia nini? Nini ni ya lazima Dinesh afanye? Kazi au kuendelesha zaidi shule? Kwa nini?



***Fikiri kuhusu marekebisho gani unaweza kulazimishwa kufanya.***

- ❒ Nani katika jamaa yako atapata shida na mabadiliko hii?
- ❒ Jinsi gani majukumu ya jamaa yatabadilika?
- ❒ Nani ataweza kujikaza kuwasiliana zaidi?
- ❒ Jinsi gani jamaa yako itakamilisha hii?

## KUCHUNGA WATOTO



Katika jamaa nyingi Marekani, wazazi wote wawili na watoto wadogo wanaenda kufanya kazi. Wazazi hawa wanahitaji mtu wakuchunga watoto wao wanapokuwa kazini. Vituo vya kuchunga watoto ni mahali ambapo wanafanya hayo. Kwa kawaida, huduma za kuchunga watoto si bure. Watu wanaweza pia toa huduma za kuchunga watoto nyumbani mwao.

Ubah na mume wake Abdullah wana mtoto mchanga na mtoto wa umri wa miaka 2. Ubah anafanya kazi usiku kama kazi ya kudumu ambayo inampa huduma za afya kwa jamaa yake. Abdullah  anafanya kazi ya muda maalumu mchana. Abdullah anaweza kupata kazi ya muda maalumu ingine jioni. Akichukua kazi hii, jamaa itapata fedha zaidi, lakini watalazimishwa kulipa kwa kuchunga watoto. Nini Ubah na Abdullah wanahitaji kufanya wanapoamua? Nini unaweza kuwashauria?

***Chapa au andika kuhusu kuchunga watoto nchini mwako au nchi yako ya ukimbizi.***

***Fikiri kuhusu namna gani unaweza kujisikia kama watoto wako au wajukuu wako wanachungiwa na mtu mwengine asiye kuwa wa jamaa yako ambaye haisihi nanyi, kama:***

| | **Faida ya chaguo hii ni gani?** | **Ubaya ya chaguo hii ni gani?** |
|---|---|---|
| Ndugu anayeishi karibu | | |
| Kituo cha kuchunga watoto | | |
| Kunchunga watoto nyumbani | | |
| Mtu mmoja anaye chunga watoto nyumbani mwako | | |
| Shule kabla ya kuanza shule kwa watoto wa umri wa miaka 3 na zaidi | | |

- ❐ Gani itakuwa chaguo yako bora kwa huduma za kuchunga watoto?
- ❐ Huduma gani ya kuchunga watoto itakuwa bei chini?
- ❐ Huduma gani ya kuchunga watoto itakuwa ya kweli zaidi kwako utakapoanza kufanya kazi Marekani?

**Shirika lako la makazi mapya litakusaidia kupata huduma za kazi.**

**Ni muhimu kuwa kwa wakati siku za maulizo zako za kazi.**

**Wakati wa maulizo ya kazi, angalia mutu anayekuuliza maswali kwa macho, cheka, na umpe mkono.**

## NAMNA GANI KUTAFUTA KAZI

***Fikiri kuhusu namna gani watu wanatafuta kazi nchini mwako au nchi yako ya ukimbizi.***

- ❒ Ungeli tafutia wapi?
- ❒ Hatua gani ungeweza kuchukua?

Mtu bora wa kukusaidia kupata kazi ni wewe mwenyewe. Lakini kuna wengine ambao wanaweza kukusaidia katika juhudi zako:


❒ **MASHIRIKA YA MAKAZI MAPYA NA HUDUMA ZA KUAJIRI WAKIMBIZI.** Wafanya kazi wa mashirika ya makazi mapya na huduma za kuajiri wakimbizi wanaweza kusaidia wakimbizi wengi kupata kazi zao za kwanza Marekani. Sikiliza mashauri ya wafanyakazi wa shirika lako la makazi mapya. Wao wanauzoefu katika kusaidia wakimbizi kupata kazi.



❒ **NDUGU NA MARAFIKI.** Uliza marafiki na ndugu zako ambao wana kazi wakujulishe kama kuna kazi yoyote katika kampuni zao, au kampuni zingine katika eneo.



❒ **MAGAZETI, INTERNETI, NA MASHIRIKA YA KAZI YA UMMA.** Makampuni mengi yanatangaza makazi wanazo katika magazeti na kwenye interneti. Makampuni memgi yanakwenda kwa njia ya mashirika ya kazi ya umma kwa kuajira watu. Ufanye angalisho na huduma za kazi zinazokuomba kulipa fedha na kukuahidi kupata kazi.



***Chapa duara kwa namna zingine zilizo tajwa kwa ukarasa 168 ambazo ulitumia zamani ulipokuwa ukitafuta kazi.***

***Fikiri kuhusu maswali yafwatayo:***

- ❒ Kama unapata shida ya kupata kazi Marekani, nani utajisikia vizuri kuomba msaada?
- ❒ Kwa nini unajisikia vizuri kuuliza mtu huyu?
- ❒ Nani unaweza kuomba msaada zaidi?

---

Alberto alipata taarifa ya kazi katika gazeti ambayo aliifurahiya. Alimletea maneja wa kesi yake hiyo taarifa, na maneja wa kesi huu alimsaidia Alberto kujaza makartasi. Alipokuwa akila, kisha siku chache, Alberto alimjulisha rafiki yake kuhusu kazi hiyo. Rafiki ya Alberto alimwambia ya kwamba anamjua mtu ambaye anafanya kazi katika kampuni hiyo, na ya kwamba mtu huyo anaweza kumsaidia Aklberto. Vitu gani mbalimbali Alberto alifanya kwa kujisaidia mwenyewe kupata kazi ? Nani unaweza kujisikia vizuri kuomba msaada kwa kupata kazi ?

---

## MASHAURI ILI UPATE MAFANIKIO KWENYE MAULIZO YA KAZI



Katika maulizo ya kazi, mtu wa kampuni atakueleza kuhusu kazi. Atazungumza nawe na kukuuliza maswali kuhusu uzoefu wako wa kazi yako ya zamani kwa kutambua kama unastahili kwa kazi hiyo katika kampuni yao. Maulizo ya kazi ni muhimu sana. Kama unafanya hisia nzuri, una bahati nzuri ya kupata kazi. Hapa chini kuna vitu ambavyo unaweza kufanya kwa kuwa na hisia nzuri:



- ❒ **KUFIKA KWA WAKATI.** Wakati ni muhimu sana kwa Wamarekani. Ukichelewa kwa maulizo, mkuu wa kazi atafikiri kwamba utachelewa kila siku kufika kazini pia.
- ❒ **KUWA MSAFI NA KUVAA MAVAZI YANAYOKUBALIKA KIKAZI.** Mshauri wako wa kazi anaweza kukusaidia kuhusu aina ya mavazi unayoweza kuvaa.
- ❒ **MTAZAME ANAYEKUULIZA MACHONI, CHEKA, NA MSHIKE MKONO.** Wamarekani wanaamini kwamba kumtazama mtu machoni kunaonesha uaminifu, na kucheka na kumshika mtu mkono inaonesha tabia nzuri ya kazi.

**Nikawaida kwenda kwa maulizo kadhaa kabla ya kupata kazi.**

- ❐ **ULIZA MASWALI KUHUSU YALE UTAKAYO FANYA KAZINI.** Hii inamwonesha mtu anayekuuliza maswali kwamba unapenda kazi.
- ❐ **SEMA BAADHI YA KIINGEREZA, KAMA UNAIJUA.** Hata kama unajuwa Kiingereza kidogo tu, kuisema inaonesha mkuu wa kazi ya kwamba unajitumainia. Pia, inaonesha ya kwamba unania ya kujifunza Kiingereza, ambayo inaweza ku ongeza bahati yako kwa ajili ya kazi bora.
- ❐ **JARIBU KUONDOA WASI WASI.** Kila mtu ana wasi wasi wakati wa maulizo ya kazi. Juwa ya kumbwa hauko peke yako katika hali hii.



*Fanya mazoezi na mwenzako:*

- ❐ Kuangaliana usoni.
- ❐ Kucheka.
- ❐ Kushikana mkono.
- ❐ Kusema Kiingereza (hata kama ni kusema tu, "Hello").
- ❐ Kuondowa wasiwasi.



***Pamoja na mwengine, cheza mfano kwa kujibu maswali kutoka kwa mkuu wa kazi, kama vile:***

- ❒ Je, unaweza kunieleza kuhusu wewe mwenyewe?
- ❒ Kwa nini unataka kazi hii?
- ❒ Uzoefu wako gani wa zamani utakusaidia na kazi hii?
- ❒ Wakati gani unaweza kuwa tayari kwa kuanza kufanya kazi?

***Sasa mfanye mazoezi ya kumuuliza mwengine maswali, kama vile:***

- ❒ Hii ni kazi ya muda au ni kazi ya kudumu?
- ❒ Wakati gani kazi inaanza?
- ❒ Ni aina ya kazi gani nitafanya?
- ❒ Nani atakuwa mkuu wangu wa kazi?
- ❒ Mtu atakaye itikiwa ataanza kazi wakati gani?

Unaweza kulazimishwa kwenda kwa maulizo za kazi kadhaa kabla ya kupata kazi. Hii ni kawaida kwa mtu yeyote anaye tafuta kazi Marekani. Unaweza kujisikia kutaka kutoendelea kama haupati kazi baada ya maulizo yako ya kazi ya kwanza, lakini jaribu kuwa na subira. Uliza jamaa na mshauri wako wa kazi kwa kupata moyo zaidi kama unayahitaji.

***Uwe na tumaini! Tafuta faraja kwa jamaa yako na mshauri wako wa kazi.***

---

Kwa kujitayarisha kwa maulizo ya kazi, Ganga alivaa mavazi safi na akaoga. Alitumia Kiingereza kidogo aliyo juwa, alimshika mkuu wa kazi mkono, na alimutazama usoni. Ganga alijisikia ya kwamba maulizo ya kazi ilipitika vizuri, lakini hakupokea simu. Unafikiri hii ilitokea kwa sababu gani? Unafikiri Ganga anajisikia namna gani? Nini ungelifanya ili ubaki mwenye tumaini unapotafuta kazi?

---

## SIFA ZAKO NZURI



*Wakubwa wengi wa kazi wanauliza kuhusu sifa zako nzuri kwenye maulizo ya kazi. Hapa kuna orodha ya maneno yanayohusika na kazi ambayo yanaweza kueleza nzuri kuhusu mtu. Angalia na utambulishe sifa nzuri kubwa unazo.*

| Sifa | Katika lugha yako | Chapa picha au andika kuhusu maana ya hayo kwako: |
|---|---|---|
| Honest | | |
| Dependable | | |
| Flexible | | |
| Hard worker | | |
| Good work ethic | | |
| Cooperative | | |
| Motivated | | |

| Sifa | Katika lugha yako | Chapa picha au andika kuhusu maana ya hayo kwako: |
|---|---|---|
| Fast learner | | |
| Reliable | | |
| Positive attitude | | |
| Good listener | | |
| Punctual | | |

*Fanya mazowezi kwa ajili ya maulizo ya kazi ya baadaye ukimwambiye mwenzako kuhusu sifa zako nzuri katika Kiingereza.*

**Lazima ubaki kwa kazi yako ya kwanza kwa miezi 6 au zaidi.**

***Kama hauwezi kupata kazi kwa wakati, fikiri juu ya nini unaweza kufanya ili ubaki na mafikiri mazuri unapotafuta kazi. Chapa duara kwa baadhi ya mambo inaweza kukusaidia kujisikia vizuri kuhusu wewe mwenyewe.***



Kuhudhuria sherehe za kijamii au kitamaduni



Kufanya mazoezi



Kujihusisha katika shule ya watoto



Kusikiliza muziki unaoizowea



Fanya mazoezi ya Kiingereza




Chukuwa mafunzo ya ujuzi



Zungumza na kiongozi wa dini au kiroho katika jamii yako



Zungumza na marafiki na ndugu kuhusu jinsi unajisikia



Ujitoleye katika jamii yako

***Vitu gani vingine unafanya kwa kubaki na mafikiri mazuri katika utafiti wako wa kazi?***

# SURA YA KUMI NA MBILI 12

## HISTORIA YA KAZI

***Fikiri kuhusu kazi yako ya sasa au kazi uliyokuwa nayo zamani.***

- ❐ ***Ulifanya kazi nyumbani au nje?***
- ❐ ***Makazi gani ulikuwa nazo?***
- ❐ ***Ujuzi gani unahitaji kwa kazi unayo? Ujuzi gani ulihitaji kwa kazi yako nyumbani?***

***Chapa au andika hapa chini kuhusu baadhi ya kazi ulizofanya zamani.***

---

Poe Hser aliitwa kwa maulizo ya kazi kisha kuomba kazi ya kusafisha nyumba. Hajawahi kufanya kazi pengine kuliko nyumbani mwake, lakini aliweza kuzungumza kuhusu uzoefu wake kusafisha nyumba na kufulia jamaa yake. Kisha posho moja, Poe Hser alitolewa kazi hiyo. Namna gani uzoefu wa Poe Hser wa zamani ulimusaidia kupata kazi? Namna gani baadhi ya ujuzi wako unaweza kukusaidia?

---

Kazi yako ya kwanza itakuwa hatua muhimu ya kwanza ya kujiwekea historia ya kazi Marekani. Jaribu kubaki kwenye kazi yako ya kwanza kwa muda wa miezi 6 au zaidi, hata kama kazii si kweli hayo unayotaka kufanya. Wakubwa wa kazi wa baadaye wataangalia utendaji wako wa kazi kwenye kazi yako hii ya kwanza wanapotaka kukupatia.

---

Masood na Ali wanaomba kazi moja. Katika mwaka iliyo pita, Masood alikuwa na kazi moja wakati Ali alikuwa na kazi nne mbalimbali nani unafikiri mkubwa wa kazi atapatia kazi? Kwa sababu gani? Kubaki kwa kazi moja ina maana gani kwa mtu?

---

**Kuboresha Kiingereza chako ni moja katika namna ya kufikia kwa kazi bora, yenyi kulipa vizuri.**

**Kama hauelewi kuhusu kitu chochote, uliza kuhusu hayo.**

## MALENGO ZA KAZI



*Inabidi ujiwekee malengo ya kazi na utambue mambo utabidi kufanya ili ufanikiwe kupata malengo hayo.*

*Fikiri kuhusu malengo zako za kazi. Chapa au andika kuhusu malengo zako za kazi katika duara hapa chini. Jaribu kuwa kweli!*

**Lengo lako la kazi katika mwezi 1:**

**Lengo lako la kazi katika miezi 6:**

**Lengo yako ya kazi katika mwaka 1:**

**Lengo yako ya kazi katika miaka 5:**

Kupata kazi bora zaidi yenye malipo makubwa zaidi itabidi uimarishe uwezo wako wa lugha ya Kiingereza na inaweza kukubidi kujifunza ujuzi mpya. Kama ulifanya kazi fulani katika nchi yako, utaweza kufanya kazi katika eneo lile nchini Marekani, lakini unaweza kulazimishwa kuenda shuleni na kupata cheti. Kufikia malengo yako inaweza kuchukua muda, na unahitaji kuwa na uvumilivu. Zaidi ya yote, kumbuka kwamba Marekani inajulikana kuwa nchi ya bahati ya kazi kwa wale ambao wanfanya kazi kwa bidii.

Kisha miezi 8 nchini Marekani, Arzu alifikiri kuhusu malengo zake za kazi. Alisikitika kwamba mabo hayakuenda kulingana na njisi alikuwa amepanga. Ungelikuwa Arzu, ungelijisikia namna gani? Ungelifanya nini? Namna gani Arzu anaweza kubaki mwenyi mafikiri mazuri kuhusu uzoefu wake Marekani?

## MALIPO, MASAA, NA MAFAO

Unapopewa kazi, mkuu wa kazi atakuambiya kuhusu malipo, masaa, mafao. Hapa kuna baadi ya vitu utaambiwa:



- ❒ Pesa ngapi utalipiwa.
- ❒ Kama utalipiwa mshahara kwa saa au mshahara kila mwaka.
- ❒ Mara ngapi utalipiwa.
- ❒ Utatumika masaa ngapi kwa posho.
- ❒ Mipango ya kazi itakuwa je.
- ❒ Mafao gani yanatolewa.

Kama hauelewi kuhusu kitu chochote, uliza kuhusu hayo.

***Pamoja na mwengine, fanya mazoezi ya kuuliza kila mmoja kuhusu vitu ukamili na mahitaji ya kazi, kama vile::***

- ❒ Kazi itakuwa kwa ma saa ngapi kwa posho?
- ❒ Wakati gani kazi inaanza?
- ❒ Italipwa mara ngapi?
- ❒ Mafao gani yanatolewa?

***Towa maswali yako mwenyewe!***

Utakapo pokea malipo yako kufwatana na mpango iliyowekwa ambayo ladba ni mara moja kwa posho, mara moja kila posho mbili, au mara moja kwa mwezi. Utakapopokea mshahara yako kama  hundi la malipo pamoja na karatasi ya maelezo ya malipo. Karatasi ya maelezo ya malipo itakuwezesha kuwa na historia ya malipo yako, uichunge karatasi hii unapopata fedha kutoka hundi lako au unapoziweka katika benki.

**Ni muhimu kulipa kodi yako nchini Marekani.**

**Hepuka mazungumzo binafsi na jamaa, marafiki, na wenzako wa kazi na usipige simu binafsi unapofanya kazi.**

**Usiache kazi kamwe kabla ya kupata ingine mpya.**

## KAZI ZINAZOLIPA KWA FEDHA MKONONI



Kufanya kazi na kulipiwa mkononi ni kinyume cha sheria Marekani kama haulipe kodi ya mshahara kwa serikali. Kama mkuu wa kazi anakulipa fedha mkononi na hakupatiye karatasi yenye maelezo ya malipo ambayo inaonesha malipo ya ujumla, fedha zilizokatwa, na malipo halisi, nyinyi wote wawili, muna vuja sheria. Kama unavunja sheria, unaweza kulazimishwa kulipa faini au kufungwa katika jela.

---

Claudia alipata kazi ya kusafisha nyumba. Alilipiwa kwa pesa mkononi kwa kazi yake, na mara nyingi alipata pesa ya kidokezo. Nini unaweza kumueleza Claudia kuhusu kulipa kodi? Kodi ya Claudia inalipa kwa ajili ya nini? Kwa nini lazima alipe kodi?

---



***Fikiri kuhusu maswali yafuatayo kuhusu kodi:***

- ❒ Kwa nini ni muhimu kulipa kodi yako Marekani?
- ❒ Nini inaweza kutokea kama hulipi kodi yako?

## MAMBO YA KUZINGATIA ILI UFANYIKIWE KATIKA KAZI

- ❒ **FIKA KWA WAKATI KAZINI.** Wakubwa wa kazi wanatumaini wafanyakazi wafike kazini kwa wakati, na utakuwa na sifa nzuri ikiwa unafika daima kazini bila kuchelewa. Kama unachelewa kazini, mshahara wako unaweza kupunguzwa. Kama unatabia ya kuchelewa unaweza kupoteza kazi yako.
- ❒ **CHUKUA MAPUMZIKO YA MAGONJWA KAMA UNAGONJWA KWELI.** Pia, unaweza hitaji kukamata siku bila kazi kama ndugu wa karibu (bibi au mtoto) ni mgonjwa na unalazimishwa kumpeleka mtu yule kwa daktari. Kama hayo yanatokea, umjulishe mkuu wako wa kazi mbele ya wakati.



- ❒ **PIGA SIMU IKIWA HAUWEZI KWENDA KAZINI.** Umpigiye simu mkuu wako wa kazi kila mara utachelewa kufika kazini au hautaweza kufika kazini kwa sababu yoyote. Ikiwa unajuwa ya kwamba hautaweza kufika kazini kwa sababu ya mpango fulani, zungumza na mkuu wako wa kazi mbele ya wakati ili upate ruhusa ya kutokuja kazini au kuchelewa.
- ❒ **KUWA WA KIRAFIKI.** Wakati wa chakula cha mchana na muda wa mapumziko unaweza kupata jinsi ya kukutana na wafanyakazi wenzako. Mada za kawaida za mazungumzo kazini ni hali ya hewa, shuguli za wikendi, chakula, na michezo. Utaweza pia kuwa na bahati ya kuzungumza kuhusu utamaduni wako hasa wakati wa likizo za kitamaduni.
- ❒ **CHAPA KAZI UKIWA KAZINI.** Hepuka mazungumzo binafsi na jamaa, marafiki, na wenzako wa kazi na usipige simu binafsi unapofanya kazi..
- ❒ **ULIZA MASWALI.** Kama kuna kitu ambacho hauelewi, uliza. Utafanya kazi vizuri zaidi na mkuu wa kazi atakuheshimu kwa kujaribu kujifunza na kujiendeleza.
- ❒ **JIFUNZE UJUZI MPYA NA MAJUKUMU MAPYA KILA MARA IWEZEKANAPO.** Unaweza kupata kazi bora zaidi ukionyesha kwamba uko tayari kuchukua majukumu zaidi.
- ❒ **JULISHA KABLA YA KUACHA KAZI.** Wakati unaacha kazi moja ili uchukuwe nyingine, mjulishe mkuu wako wa kazi ya zamani mbele ya posho 2. Usiache kazi kamwe kabla ya kupata kazi nyingine mpya.

***Chapa duara kwa mabo ya kufanyikiwa kazini ambayo ni tofauti na hizo za ujuzi wako wa zamani.***

***Fikiri kuhusu maswali ya fwatayo:***

- ❒ Gani ya mambo ya fwatayo yanaweza kuwa rahisi kwako kuyafwata?
- ❒ Mambo gani yanaweza kuwa magumu kwako kufwata?
- ❒ Nini utafanya ili uweze kuwa na mafanyikio kazini?

---

Sanaa alifanya kazi kwa bidii kwa kazi yake mpya, lakini mara kwa mara hakuelewa nini alitakiwa kufanya. Sana hakujuwa Kiingereza kabisa, kwa hiyo hakuweza kumweleza mkuu wake wa kazi ya kwamba hakuelewa vitu vingine ambavyo aliombwa kufanya. Namna gani Sanaa anaweza kuelewa vizuri? Ungelikuwa Sanaa, namna gani ungeshugulika na hali hii?

---

# 12 KAZI

**Unahaki ya kufanya kazi katika eneo salama na yenye afya.**

Boris alianza kazi kisha miezi chache baada ya kufika Marekani. Hakuweza kuzungumza Kiingereza, lakini alikuwa mfanya kazi mwema sana na wa kurafikiana, na mkuu wake wa kazi na wenzake wa kazi walimpenda sana. Kisha miezi 16, Boris aliomba kazi ingine mahali pengine na akaacha kazi yake ya kwanza bila kujulisha mtu yeyote. Alishangaa wakati hakupata kazi hii mpya. Baadaye alitambua ya kwamba mkuu wake wa kazi hakusema vizuri kuhusu yeye kwa kazi mpya hiyo. Nini Boris alifanya vibaya? Boris angelipashwa kufanya nini?

## HAKI ZA MAHALI PA KAZI



Kama mkimbizi, una haki za mahali pa kazi sawa na raia wa Marekani. Mkuu wa kazi hawezi kukubagua kwa sababu ya hali yako ya kuwa mkimbizi na hawezi kukuima kazi wala kuto kukupandisha cheo kwa sababu ya umri wako, ulema ulionao, hali ya kuwa au kutokuwa na ndoa, nchi unayotoka, asili yako, dini, au jinsia, au mwelekeo wa kijinsia. Hata hivyo, badhi ya ajira ni wazi tu kwa wananchi wa Marekani.

Sheria ya kazi pia inalinda wafanya kazi kutokana na hali isiyo ya salama kwenye maeneo ya kazi. Lazima mkuu wa kazi ahakikishe ya kwamba mahali pa kazi ni salama na kwa afya. Sheria inalinda pia wafanya kazi na hali ya unyanyasaji wa kijinsia katika eneo za kazi. Unyanyasaji wa kijinsia ni tabia yoyote ya hali ya mgono ambayo inamfanya mtu kujisikia kutishiwa au wasiwasi.

Sangita ana mkuu wake wa kazi ambaye ni mwanaume ambaye ni mwema, msaidizi, na wa kurafikiana. Lakini mara kwa mara anamugusa kwenye bega anapozungumza naye. Hii inafanya Sangita mwenyi wasiwasi sana. Swala hapa ni gani? Lazima Sangita afanye nini?

***Fikiri kuhusu haki kazini nchini Marekani.***

- ❒ Njisi gani haki hizi zinaweza kuwa sawa na ujuzi wako wa zamani?
- ❒ Namna gani zinaweza kuwa tofauti?
- ❒ Namna gani unaweza zoweya tofauti hizi?

# SURA YA KUMI NA MBILI 12

## KAMILISHA*

Kweli au uongo? Kwa kiasi gani unafikiri kujua kuhusu makazi mapya Marekani? Pima ujuzi wako na maarifa yaliyo hapa chini. Soma maarifa na chapa duara kwa maneno **Kweli** ikiwa unafikiri ni kweli na chapa dhuara kwa neno **Uongo** ikiwa unafikiri si kweli.

1. Kupata kazi yako inaweza kuchukua mda kidogo kama vile siku chache mpaka miezi mingi. **Kweli** **Uongo**
2. Serikali au Shirika lako la makazi mapya linapashwa kukutafutiya kazi. **Kweli** **Uongo**
3. Kujifunza Kiingereza inaweza kusaidia kuongeza bahati yako ya kupata kazi. **Kweli** **Uongo**
4. Wakimbizi wengi wanaanza kufanya kazi kwa kiwango cha kwanza. **Kweli** **Uongo**
5. Mara nyingi wanawake wanasimamiya wanaume kazini nchini Marekani. **Kweli** **Uongo**
6. Kama unachelewa kwa maulizo ya kazi, mkuu wa kazi anaweza kutokupa kazi kwa sababu anaweza kufikiri utachelewa kwa kazi pia. **Kweli** **Uongo**
7. Mtu bora kwa kukusaidia kupata kazi ni wewe mwenyewe. **Kweli** **Uongo**
8. Wakimbizi hawalazimishwi kulipa kodi ya malipo kwa serikali nchini Marekani. **Kweli** **Uongo**

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukar 222.

13



# Sura Ya Kumi Na Tatu
## KUJIFUNZA KIINGEREZA

Kujifunza lugha mpya inachukua wakati na kazi. Wamarekani wanaamini ya kwamba mtu si kamwe mzee sana au mdogo sana kwa kujifunza mambo mapya. Kujifunza Kiingereza itakusaidia kupata kazi, kuwa na mafanyikio kazini, na kuwasiliana na Wamarekani wengine, na kuzowea haraka zaidi maisha yako mapya nchini Marekani.

---

### Sura Hii Itajadili

» Umuhimu wa kujifunza Kiingereza
» Njia za kujifunza Kiingereza
» Namna gani kujifunza lugha mpya inachukua muda na kazi ngumu.

**Kujifunza Kiingereza itakusaidia kupata kazi na kujirekebisha haraka zaidi kwa maisha yako mapya nchini Marekani.**

## MANENO MUHIMU YA KIINGEREZA

Maneno ya kiingereza yafuatayo yanatumiwa wakati wa kuzungumza kuhusu kujifunza Kiingereza nchini Marekani. Maneno haya na misemwa haya yatakuwa na mafaa kwako kuyajiifunza.

***Sema neno katika Kiingereza, andika lugha yako ya asili. Kisha, chapa picha ya neno, andika maana yake, au uitumiye katika msemo. La kwanza limefanyika kwa ajili yako.***

| Katika lugha yako | Katika Kiingereza | Chapa picha ya neno, andika maana yayo, au uitumiye katika msemo |
|---|---|---|
| *Rudilia tena tafadhali* | Please say that again. | *Tafadhali rudilia tena. Sikusikia mara ya kwanza.* |
| | Can you repeat that? | |
| | What does _____ mean? | |
| | Can you speak more slowly? | |
| | I don't speak English. | |
| | I don't understand… | |
| | Can you understand me? | |

**Utajifunza Kiingereza haraka zaidi kama una hamu kubwa ya kujifunza lugha.**

***Fikiri kuhusu kwa nini ni vizuri kuwa na uwezo wa kuwasiliana na wengine.***

***Unazungumza lugha gani? Iandike hapa:***

***Zungumza na mwengine kuhusu wapi unaweza kutumia lugha hizi nchini mwako au nchi yako ya ukimbizi. Orodha yako inaweza kujumuisha nyumbani, sokoni, unapotaka kuchua basi mahali fulani, nk.***

***Fikiri kuhusu maswali yafwatayo:***

- ❒ Amna gani ulijifunza lugha unayo zungumza?
- ❒ Ni baadhi ya njia mbalimbali unaweza kuwasiliana na watu ambao wanazungumza lugha tofauti na wewe? Kwa mfano, ni kwa njia gani unaweza kuwasiliana na Wamarekani kabla ya kujifunza namna ya kuzungmza kiingereza?
- ❒ Kiasi gani ya Kiingereza unajua mpaka sasa?

***Toa kiwango chako cha Kiingereza kwenye kipimo hapa chini. 0 ni ngazi ya anayeanza kujifunza Kiingereza (au asiyesema Kiingereza), na 5 ni ngazi ya anayejuwa Kiingereza.***

0 — 1 — 2 — 3 — 4 — 5

Asiye sema Kiingereza au anayejifunza Kiingereza ⟷ Anaye sema Kiingereza

## MASHINDANO YA KIINGEREZA

Usijali kama huwezi kusema kitu chochote kwa Kiingereza kabla ya kuchukua madarasa ya lugha ya Kiingereza. Kabla ya kuanza masomo, utapewa mashindano. Mashindano ni aina ya mtihani. Madarasa ya Kiingereza ina kiwango mbalimbali, kutoka mwanzo hadi viwango vya ju, na mashindano itaonesha kiwango chako ni gani. Mashindano inaweza kuwa mazungumzo au mtihani wa kuandika.

Madarasa ya Kiingereza inatofautiana katika aina ya Kiingereza inayofundishwa. Madarasa moja yanafundisha Kiingereza rahisi, ya mafaa kwa watu ambayo wanaokuja upya wanahitaji kujuwa kujitembeza mjini, kwa kununua vitu katika duka, kusoma ratiba ya basi, au kutafuta kazi. Wengine wanafundisha Kiingereza inayo hitajika kwa kazi, kwa mfano, kufanya kazi katika hoteli au kufanya kazi katika eneo la matunzo ya wangonjwa. Kuna pia madarasa ya Kiingereza yanayo tayarisha wanafunzi kwa masomo ya chuo kikuu. Madarasa hizi zinatumia muda zaidi juu ya kusoma na kuandika.

## UMUHIMU WA KUJIFUNZA KIINGEREZA

Wakati Nadia alifika Marekani mara ya kwanza, alihitaji mtu wa kutafsiri kila mara alipo hitaji kwenda kwa daktari wake. Hii ilikuwa vigumu sana kwa sababu siku moja tuu ambayo mkalimani wa mwanamke alikuwa na wakati ilikuwa siku ya pili tuu. Sasa, kisha myaka 3, Nadia anapanga mpango na daktari yeye mwenyewe bila mtu wa kutafsiri. Hii inamaana ya kwamba anaweza kwenda kwa daktari siku yoyoyte. Namna gani kujifunza Kiingereza imemsaidia Nadia? Njia gani mbalimbali unaweza kufanya mazoezi ya Kiingereza?

Utajifunza Kiingereza haraka zaidi kama una hamu kubwa ya kujifunza lugha. Hapa kuna baadhi ya sababu ya kujifunza Kiingereza ni muhimu:



- ❒ Kupata kazi.
- ❒ Kuwa na mafanyikio kazini.
- ❒ Kujuwa nini watoto wako na wajukuu wako wanasema.
- ❒ Kuwasiliana na mwalimu wa watoto wako.
- ❒ Kuwa huru: kuchukua basi na kwenda sokoni peke yako kwako mwenyewe na kwa ajili ya jamaa yako.
- ❒ Kuzungumza na majirani.
- ❒ Kujuwa nini inaendelea duniani kupitiya televisheni, magazeti na interneti.
- ❒ Kupita mtihani wa uraia wa Marekani ili uweze kuwa raia wa Marekani.

**Fanya mazoezi ya kusema Kiingereza na wengine ambao wanajifunza lugha au tayari wanasema hiyo lugha.**

Naw Ku alijifunza Kiingereza kwa njia ya kazi lakini mme wake, Soe Thu, alijua Kiingereza kidogo tu. Walipoenda kuhudhuria mkutano ya walimu na wazazi pamoja, Naw Ku alimtafsiria Soe Thu. Hii ilikuwa ya wasiwasi sana kwa Naw Ku na Soe Thu. Sasa, kisha miaka 2, kiingereza ya Soe Thu imekuwa bora zaidi, na yeye na Naw Ku wanaweza kuzungumza kiingereza wote wawili kwa mkutano wa wazazi na walimu kwa shule la watoto. Namna gani kusema Kiingereza ilimsaidia Soe Thu? Jinsi gani mbalimbali Soe Thu angeweza kujifunza Kiingereza?

***Kwa nini kujifunza Kiingereza inaweza kuwa muhimu kwako nchini Marekani? Chapa au andika kuhusu sababu mbalimbali hapa chini.***

Bhampa ni mwanaume mzee ambaye amekuwa na shida ya kujifunza Kiingereza. Mtoto wake na binti mkwe wake wote wanaenda kazini, na mujikuu wake anaenda shuleni. Sasa, yeye anabaki nyumbani peke yake. Lazima Bhampa afanye nini kwa kuboresha Kiingereza yake?

## NJIA ZA KUJIFUNZA KIINGEREZA

Kuna njia nyingi unaweza kujifunza Kiingereza. Hapa chini kuna mifano mbalimbali:



**KUHUDHURIA DARASA ZA LUGHA** (mara nyingi inajulikana kama ESL, au Kiingereza kama lugha ya pili). Katika darasa la ESL, wanaume na wanawake wa umri tofauti, elimu,na asili ya kikabila wanakaa pamoja. Katika kiwango cha mwanzo ya darasa la ESL, wanafunzi wanajifunza kwa kawaida Kiingereza wanayoitaji kwa kufanya kazi katika jamii na katika mahali yao ya kazi. Katika darasa ya kiwango cha juu, wanafunzi wanaangalia zaidi Sarufi, kusoma, na kuandika.

---

Faadumo alianza kujifunza Kiingereza, lakini bado anatatizo ya kuwasiliana na watu kazini. Baadhi ya njia gani Faadumo anaweza kuwasiliana na wengine wakati anaenda kujifunza Kiingereza?

---



**JIFUNZE PAMOJA NA MWALIMU WA KUJITOLEA.** Hii inaweza kuwa pia njia nzuri ya kujifunza kuhusu utamaduni na desturi za Marekani. Omba shirika lako la makazi mapya likuunganishe na mtu aliyejitolea.

**KUANGALIA SINEMA ZA KIINGEREZA,** televisheni, maonyesho, au kusikiliza programu za Kiingereza kwa redio.



**FANYA MAZOEZI YA KUSEMA KIINGEREZA NA WENGINE** ambao wanajifunza lugha au tayari wanazungumza Kiingereza.

**SOMA MAGAZETI ZA KIINGEREZA.** Kiingereza iko pande zote karibu nawe: kwenye masanduku ya vyakula, ishara, matangazo, mabasi, vipeperushi, na magazeti.



**JIFUNZE KIINGEREZA KAZINI.** Wakati unapata kazi, utajifunza misamiati na maneno ambayo ni muhimu kwa ajili ya kazi hiyo. Utalazimishwa kushirikiana na wenzako wa kazi, na labda na wateja au wateja ambao wanasema Kiingereza. Kusema Kiingereza nao itakusaidia kuboresha Kiingereza yako.


**Watu kutoka duniani kote wanajifunza Kiingereza nchini Marekani.**

**Wanafunzi katika darasa la Kiingereza wanaweza kuwa na asili tofauti sana, lakini wote wanataka kitu moja: Kujifunza Kiingereza.**

## TOFAUTI KATIKA DARASA LA ESL


Katika darasa lako la ESL, unaweza tambua ya kwamba kuna wanaume na wanawake kutoka duniani kote ambao wanajifunza Kiingereza pamoja nawe. Inaweza kuwa ya kusisimua kukutana na watu wanaozungumza lugha tofauti na wenye historia tofauti ya kiutamaduni na yako.

*Tazama picha ya ramani ya dunia hapa chini. Chapa duara kwenye nchi yako ya asili.*



# SURA YA KUMI NA TATU 13

***Sasa chapa duara ambapo utahamia nchini Marekani.***




***Fikiri kuhusu maswali yafuatayo:***

- ❒ Unafikiri wahamiaji katika jamii yako mpya watakuwa wa wapi?
- ❒ Mambo gani utataka kujifunza kuhusu wengine katika darasa lako?



Tofauti hii inaweza kuwa changamoto kwa walimu wa wanafunzi wengine. Wanafunzi mbalimbali wanaweza kuwa na asili mbalimbali za elimu na malengo kwa kujifunza Kiingereza. Wanafunzi mbalimbali wanaweza kuwa vijana ambao wana matumaini ya kujinfuza kiingereza kwa kuenda kwenye chuo kikuu, na wengine ni wazee ambao wangependa kujifunza Kiingerea ili waweze kwenda sokoni au kwa daktari wenyewe. Baadhi ya wanafunzi wanaweza kuwa watu wazima wanaokuwa na kazi ya kudumu wanaenda shuleni kwa kuboresha Kiingereza yao kazini au kuzungumza na mwalimu wa mtoto wao. Lakini haijalishi asili yao, wanafunzi wote wanataka kitu moja: Kujifunza Kiingereza.

Wakati Priscilla alifika mara ya kwanza katika darasa lake la Kiingereza, alishangaa kuona watu wenyi asili nyingi tofauti. Alikuwa bado hajakuwa karibu na watu wengi kama wale. Ungelikuwa Priscilla, ungelijisikia namna gani? Unafikiri Priscilla alitambua tofauti gani ingine katika darasa lake wanapoendelea na darasa? Ungelikuwa katika darasa la Priscilla ungelifanya nini kwa kujisikia vizuri?

***Fikiri kuhusu siku yako ya kwanza ya darasa la Kiingereza. Namna gani utajitambulisha kwa wengine?***

❒ I come from ________________________. SOMALIA
*Natoka* ________________.

❒ I speak ____________________________. SOMALI
*Nasema* ________________.

❒ My family has ___________ members. 8
*Jamaa yangu ina watu* _______________.

❒ I have been in the United States since _______________. JUNE
*Nimekuwa Marekani tangu* ________________.

❒ I would like to learn about
_____________________________. BUYING FOOD IN THE UNITED STATES AND TAKING THE BUS
*Ningependa kujifunza kuhusu* __________________________________.


CAL
COR Cultural Orientation Resource Center

## KUTUMIA KIINGEREZA

***Endelea kuandika katika chati  wakati unatumia Kiingereza, wapi unatumia Kiingereza, nini ulisema, na namna gani inatumiwa. Ilikuwa vizuri. Ulipata matatizo? Mbili za kwanza zinajazwa katika mifano?***

| Tarehe; wakati | Mahali/hali | Niliyo sema | Matokeo |
|---|---|---|---|
| *Siku ya kwanza, Tarehe 19 mwezi ya tatu, mwaka wa, 2012, pa saa 10 na dakika 30.* | *Nilizungumza na mwalimu wa hesabu wa mtoto.* | *Ndiyo, ninaweza kuwa shuleni kwa mkutano, siku ya pili, tarehe 20 mwezi wa tatu pa saa 10 na dakika 15.* | *Mwalimu alifikiri nilisema Saa 10 na dakika 50. nililazimishwa kungonja. Haikua tatizo.* |
| *Siku ya pili tarehe 20, Mwezi wa tatu, pa saa 9 na dakika 30.* | *Kusoma ratiba ya basi.* | *Niliona hapo kuna basi ya kwenda shuleni inayo ondoka na saa 9 na dakika 5, na kufika pa saa 9 na dakika 59.* | *Nilichukua basi na nikaenda shuleni kwa wakati.* |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

**Kujifunza lugha mpya inachukua wakati, na kila mtu anajifunza kwa njia tofauti.**

**Fanya mazoezi ya kuzungumza au kusikiliza kiingereza kwa kiasi Fulani ya muda kila siku.**

## KUJIFUNZA LUGHA MPYA INACHUKUA MUDA



Mwanzo, unaweza kuwaza ni vigumu kujifunza Kiingereza na kuchanganyikiwa. Ni kawaida kujisikia hivyo. Kila mtu anajifunza mambo kwa njia tofauti. Watu wamoja wanajifunza haraka zaidi kuliko wengine. Watu wengine wanajifunza kwa kufanya. Wengine wanajifunza kwa kusikia au kwa kusoma. Watu wengine wanaweza kutaka kungoja kidogo kabla ya kusema. Wengine wana penda kujaribu maneno mapya na misemwa mara moja. Lakini kwa kila mtu, kujifunza lugha inachukua wakati na juhudi.

***Kujifunza Kiingereza itakuwa changamoto na inachukua muda, lakini endelea kufanya mazoezi!***

***Fikiri kuhusu njia mbalimbali utajaribu kwa kujifunza Kiingereza. Shiriki hizi na mwengine.***

Ya muhimu kwa kujifunza lugha mpya ni kufanya mazoezi kila siku. Hata kama wewe unasikiliza redio au unatazama televisheni kwa lugha ya Kiingereza kwa dakika kumi tu kila siku, hii itakusaidia. Kisha muda na kwa mazoezi utakuwa bora zaidi kuzungumza Kiingereza.

Muda kidogo kisha kufika Marekani, Reza aliji andikisha kwa darasa la Kiingereza. Darasa ilikuwa kila siku ya pili na siku ya nne magaribi. Darasa iliendelea vizuri na alikuwa akijifunza mengi. Kisha Reza alitolewa kazi. Angepashwa kufanya kazi siku ya kwanza mpaka siku ya posho tangu saa kumi mpaka saa sita ya usiku (minuit). Tatizo ni nini hapa? Unafikiri Reza angepashwa kufanya nini?

# SURA YA KUMI NA TATU 13

***Kama una wasiwasi kuhusu kujifunza Kiingereza, vitu gani vizuri unaweza kufanya kwa kujifunza kiingereza? Chapa duara kwa mambo mbalimbali unaweza kufanya kwa kujifunza lugha? Chapa duara kwa mambo hapa chini ambayo unaweza kufanya.***

- ❒ Fanya mazoezi ya kuzungumza Kiingereza na wengine ambao wana zungumza Kiingereza.
- ❒ Tazama televisheni au sikiliza redio katika Kiingereza.
- ❒ Hudhuria madarasa ya Kiingereza.
- ❒ Fanya mazoezi na watu katika jamii yako.
- ❒ Fanya mazoezi na mtu anayezungumza Kiingereza anaye taka kujifunza lugha yako.
- ❒ Weka malengo ya kweli kwa ajili yako mwenyewe kila juma.
- ❒ Chunga orodha ya maneno mapya unayojifunza.
- ❒ Jaribu kusoma Kiingereza ambayo unaona karibu na wewe, juu ya ishara mitaani, kwenye mabasi, na katika madirisha ya maduka.

***Mambo gani mengine yanaweza kukusaidia kujiamini kwa kujifunza Kiingereza?***

## KAMILISHA*

***Chagua majibu bora zaidi kwa maswali hapa chini ukifanya chaguo bora. Hii ni mfano:***

*Lugha gani ndio inazungumzwa na watu wengi zaidi Marekani?*

a. Kichina.

(b.) Kiingereza.

c. Kijerumani.

***Watu wengi Marekani wanazungumza Kiingereza. Kwa hiyo, Jibu ni b. Kiingereza.***

1. Kujifunza Kiingereza ni mchakato wa haraka na rahisi.

   a. Ndiyo.

   b. Hapana.

2. Kwa nini kujifunza Kiingereza ni muhimu sana?

   a. Ili kupata kazi nzuri.

   b. Ili kupita mtihani ya uraia wa Marekani.

   c. Ili kuwa huru na kujitegemea.

   d. Ili kujua nini wajukuu wanasema wanapozungumza Kiingereza.

   e. Yote yaliyo juu.

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 222.

3. Ya muhimu kwa kujifunza Kiingereza ni kufanya mazoezi mara tatu kila juma.

   a. Kweli.

   b. Uongo.

4. Gani ya yanayofwata ni baadhi ya njia ya kujifunza kiingereza?

   a. Kuhudhuria darasa ya lugha ya Kiingereza.

   b. Kutizama sinema ya Kiingereza na maonyesho ya televisheni.

   c. Kufanya mazoezi ya kuzungumza Kiingereza na wakimbizi wengine wanaojifunza Kiingereza pia.

   d. Yote yaliyo juu.

5. Kwa muda na mazoezi utakuwa vizuri zaidi kwa kuwasiliana katika Kiingereza.

   a. Ndiyo, nitakuwa.

   b. Hapana, sitakuwa.



# Sura Ya Kumi Na Nne
## ELIMU

Marekani, elimu inapatikana kwa wote bila kujali umri wa mtu, asili, dini, pendekezo lake la kijinsia, au nafasi yake katika jamii. Wamarekani wengi wanafikiria elimu kama njia ya kupata kazi bora na kuboresha maisha yao.

### Sura hii itazungumza kuhusu

- Elimu kwa watoto
- Elimu kwa watu wazima



## MANENO MUHIMU YA KIINGEREZA

Maneno ya Kiingereza yafuatayo hutumiwa wakati wa kuzungumza kuhusu huduma za afya nchini Marekani. Maneno haya yatakuwa na mafaa kwako kuyajifunza.

***Sema neno au msemo katika kiingereza. Andika neno katika lugha yako ya asili. Kisha chapa picha ya neno au msemo, andika maana yake, au uitimiye katika msemo. La kwanza limefanyika kwa ajili yako.***

| Katika lugha yako | Katika Kiingereza | Chapa picha ya neno, andika maana yayo, au uitumiye katika msemo. |
|---|---|---|
| *mahudhurio* | attendance | *Mahudhurio ina maana ya kuwa katika mahali fulani kwa sababu Fulani, kama vile shule au mkutano* |
| | book | |
| | certificate | |
| | class | |
| | degree | |
| | diploma | |
| | education | |
| | math | |
| | reading | |
| | school | |
| | science | |
| | teacher | |

# 14 ELIMU

**Elimu ya umma ni bure. Watoto wote wenye umri wa miaka 6 hadi 16 lazima waende shuleni.**


**Umwandikishe mtoto wako kwenyi shule haraka uwezavyo. Shirika lako la makazi mapya litakusaidia kuyafanya.**

***Fikiria kuhusu elimu ya umma ilikuwa katika nchi yako au nchi yako ya ukimbizi.***

- ❒ Kulikuwa malipo?
- ❒ Umbali gani shule ilikuwa na ambapo ulipo ishi? Namna gani watoto wako walifika huko?
- ❒ Nini watoto walipeleka shuleni?
- ❒ Somo gani ilifundishwa?
- ❒ Siku ya shule ilikuwa wa muda gani?
- ❒ Watu wazima aliendа shuleni?

***Chapa au andika kuhusu shule nchini mwako au nchi yako ya ukimbizi.***

***Zungumza na mwenzako kuhusu yale uliandika au kuchapa. Hii ni mazoezi mazuri, na unaweza kutaka kuambia mtu nchini Marekani kuhusu shule katika nchi yako au nchi yako ya ukimbizi!***



## ELIMU KWA WATOTO

Elimu ya umma ni bure. Watoto wote wenye umri wa miaka 6 hadi 16 lazima waende shuleni. Kwa kawaida watoto wenyi umri wa miaka 5 mpaka 18 wanaweza kupata elimu ya umma. Wazazi wanaweza pia kuandikisha watoto kenyi shule binafsi, lakini malipo katika shule hizi inaweza kuwa ghali.

***Fikiri kuhusu maswali ya fwatayo:***

- ❐ Wakati gani mwaka wa shule ulianza na uliisha nchini mwako au nchi yako ya kigeni?
- ❐ Watoto walilazimishwa kuenda shueleni?
- ❐ Kulikuwa elimu ya bure kwa watoto wote?

Katika shule za Marekani, watoto wenyi asili ya rangi tofauti, kikabila na lugha mbalimbali wana soma na kucheza pamoja. Katika shule nyingi wanaume na wanawake wanacheza pamoja. Watoto wenyi ulema wa mwili au wa akili, wana haki ya kusoma kama vile watoto wengine wazima.



---

Arale alikuwa na wasichana wawili na mvulana mmoja. Mvulana alikuwa katika kiti cha walemamavu na alikuwa na ulema wa akili. Nchini mwa Arale watoto walemavu hawakuenda shuleni, hata wasichana hawakuenda shuleni pia. Arale alishangaa sana kujua ya kwamba nchini Marekani lazima watoto wote waende shuleni. Ungelikuwa Arale, namna gani ungejisikia? Ungezungumza na nani kuhusu unavyojisikia?

---

Ni muhimu kumwandikisha mtoto kwenye shule haraka iwezekanavyo. Kwa kawaida watoto wanaenda shuleni karibu na mahali wanaishi. Shule nyingi zinahitaji kuona chanjo za watoto wako na rekodi ya matibabu. Shirika lako la makazi mapya litakusaidia katika mchakato huu. Kama mtoto wako ana rekodi yoyote ya matibabu au ya shule, uilete pamoja nawe Marekani.

# 14 ELIMU


**Wakati wanafunzi hawaendi shuleni, lazima wazazi waandike barua inaeleza sababu.**

Kuna viwango nne ya elimu Marekani:

**SHULE YA CHEKECHEA (WATOTO AMBAO HAWAJA ANZA SHULE)**
Kiwango hiki ni kwa ajili ya watoto wa umri ya miaka 3–5. Hailazimishwi na sheria, na si bure kwa kawaida.



**SHULE YA MAANDALIO AU SHULE YA MSINGI**
Kiwango hiki kinaanza na shule ya chekechea (miaka 5) na inaendelea mpaka somo la 5 au la 6 (miaka 12).




**SHULE YA SEKONDARI AU SHULE YA KATI**
Katika kiwango hiki munamo kwa kawaida somo la 6 mpaka la 8 (miaka 12 mpaka 14).



**SHULE YA JUU ao SHULE YA KUHANI**
Katika kiwango hiki kuna somo la 9 mpaka 12 (miaka 14 mpaka 18). Wanafunzi wanaomaliza shule ya sekondari wanapata diploma ya sekondari.



## MWAKA WA SHULE

Mwaka wa shule huanza katika mwezi wa Nane au wa Kenda na kuisha katika mwezi wa Tano au wa Sita. Watoto wengi wanahudhuria madarasa kwa karibu masaa 6 kwa siku. Siku ya Kwanza mpaka siku ya Tano (Jumatatu hadi Ijumaa). Wanafunzi ambao wanaitaji kufikia waliyo mbele darasani wanaweza kuhudhuria shule ya mwezi ya sita na ya saba.

## KUHUDHURIA SHULE

Kuhudhuria shule ni muhimu sana. Watoto wasipoenda shuleni, lazima wazazi wa andike barua ambayo inaeleza sababu, na lazima wanafunzi wafanye kazi ya shule ambazo walikosa.

---

Binti wa Isabel alikuwa na matatizo shuleni. Siku moja Isabel alibaki naye nyumbani ili aweze kumpumzika. Baadaye asubuhi hiyo, shule ilipigia Isabel simu kumujulisha ya kwamba binti yake haukuenda shuleni siku hiyo. Isabel alichanganyikiwa. Aliiambia shule ya kwamba alibaki na binti yake nyumbani siku hiyo. Kwa sababu gani shule ilimpigia simu? Ilikuwa tazizo kwa Isabel kwa kubaki na binti yake nyumbani? Nini Isabel angelifanya iliaweze kuhepuka hali hii?

---

## MALIPO YANAYOHUSIANA NA SHULE



Hata kama elimu ua umma ni bure, wazazi wanalipa pesa fulani kama vile bei za mahitaji ya shule na pesa kwa shuguli ya pekee. Watoto wanaweza kwenda shuleni na chakula chao cha mchana au wanaweza kununua chakula cha bei chini, kwenye kafeteria ya shule.

---

Sonam binti wa Arjun wa umri wa miaka 10 hakupenda chakula cha mchana Arjun alinfungia kwenda shuleni kwa sababu ilikuwa tofauti na chakula ambayo marafiki wa Sonam walileta kwa chakula cha mchana. Watoto wengine walicheka chakula cha Sonam. Sonam alitaka kununua chakula kwenye cafeteria. Ungelikuwa Arjun, ungelijisikia namna gani? Ungelifanya nini kuhusu tukio hii?

---



***Jamaa zilikua na malipo gani kwa shule za umma katika nchi yako au nchi yako ya ukimbizi?***

**Baadhi ya watoto wanoaishi karibu na shule wanatembea.**

## USAFIRI





Baadhi ya watoto wanaoishi karibu sana na shule wanatembea. Kama shule iko mbali sana na nyumbani kwako kwa mtoto kutembea, mabasi ya shule yanaweza kutoa usafiri bure kwa kwenda shule. Mfumo wa shule utaamua umbali kutoka shule kwa ajili ya usafiri wa bure.

**Shule nyingi zina madarasa maalum ya kusoma Kiingereza kwa wanafunzi wasiojua Kiingereza vizuri.**

## MPANGO

Hakuna mpango wa taifa kwa masomo nchini Marekani. Kila jimbo, kila mfumo ya shule ya kila mtaa, au shule peke yake inaamua nini itafundishwa shuleni. Wengi wa wanafunzi wanajifunza Kiingereza, hesabu, masomo ya jamii, na sayansi. Somo zingine kama vile Sanaa, muziki, elimu ya kimwili, na lugha za kigeni yanaweza kutolewa pia.

## MTINDO WA KUFUNDISHA NCHINI MAREKANI



Nchini Marekani walimu wanawahimiza wanafunzi kujifunza kwa kufikiri na kutambuwa, kwa kuuliza mswali, na kujiunga katika majadiliano na shughuli.

---

Wakati Hanan alisikiliza binti yake na mtoto wake wa kiume wakizungumza kuhusu shule yao mpya, alichanganyikiwa. Watoto wake walipata aina gani ya elimu? Mwalimu hakuzungumza sana, na watoto walitarajiwa kuuliza maswali mengi na kutoa mawazo yao wenyewe. Wangeweza hata kutokubaliana na mwalimu au kitabu! Na badala ya kusikiliza mwalimu, walitumia muda mwingi kufanya kazi na wenzao. Jinsi gani mtindo huu wa mafundisho ni tofauti na namna walimu wanafundisha nchini mwako au nchi yako ya ukimbizi? Jinsi gani ni ina fanana? Unafikiri kwa sababu gani walimu wa Marekani wanatumia mtindo hii yakufundisha? Hanan angeliweza kufanya nini ili aweze kuelewa zaidi yanayo pitika katika madarasa ya watoto wake?

---

## KUJIFUNZA KIINGEREZA




Shule nyingi zina madarasa ya pekee ya kusoma Kiingereza kwa wanafunzi wapya. Shule zingine zinatoa msaada kupitia mwalimu wa pekee au mwalimu msaidizi.

# SURA YA KUMI NA NNE 14

Siku moja shule ilimwita Victoria kumwambia kuwa mtoto wake Joseph alikuwa katika shida kwa kuchelewa mara nyingi. Wakati Joseph alifika nyumbani kutoka shuleni, Victoria alimuuliza namna gani walimuazibu shuleni. Joseph alisema kwamba alilazimishwa kuenda kuzungumza na mkuu wa shule  na kueleza kwa nini alichelewa. Victoria alichanganyikiwa. Alijisikia kwamba mtoto wake hakuadhibiwa kweli. Jinsi gani mwanafunzi angeweza kuandhibiwa nchini mwako au nchi yako ya ukimbizi? Ungelikuwa Victoria, ungelijisikia namna gani kuhusu tukio hii. Jinsi gani ungeweza kushugulika na hayo?

## KUJIREKEBISHA

Wanafunzi wapya wengi wanachukua muda kwa kujirekebisha, hasa katika mwaka wao wa kwanza wa shule. Watoto wanaweza kujisikia peke yao mara ya kwanza, lakini wakati Kiingereza yao inaboreka zaidi, wanaweza kuwa na marafiki na kujisikia vizuri shuleni.

***Fikiri kuhusu maswali yafuatayo kuhusu watoto wako:***

- ❒ Changamoto gani unafikiri watoto wako wanaweza kuwa nayo wanapojirekebisha kwa mazingira ya shule nchini Marekani?
- ❒ Jinsi gani unaweza kuwasaidia watoto wako kukabiliana na changamoto hizi?

## TABIA ISIYO YA KAWAIDA YA WANAFUNZI WA MAREKANI

Wwanafunzi wengi wapya na wazazi wao wanashangaa kuona tabia zisizo za kawaida na mavazi za wanafunzi wa Marekani. Shule za umma za Marekani zinawapa wanafunzi uhuru wa kuchagua kufanya mambo wanayotaka, lakini wanatarajiwa pia kufuata sheria za shule. Wakivunja sheria, wanafunzi wanaweza kulazimishwa kubaki shuleni kisha darasa au kufukuzwa shuleni kwa siku chache. Malipizi ya kimwili hairuhusiwi shuleni nchini Marekani.

***Fikiri kuhusu tabia za watoto shuleni nchini mwako au nchi yako ya ukimbizi.***

- ❒ Walivaa unifomu?
- ❒ Waliuliza maswali, walifanya kazi katika vikundi, au walimsikiliza mwalimu kwa wakati nyingi kwa siku?
- ❒ Wanafunzi wangeweza kuzunguuka mara nyingi, au kubaki wakikaa kwa viti vyao kwa wakati nyingi kwa siku?

**Walimu wanaamini nchini Marekani ya kwamba lazima wazazi washiriki katika elimu ya watoto wao.**

## CHANGAMOTO ZA SHULE

Katika shule mbalimbali, hasa shule kubwa katika miji mikubwa, zina matatizo ya kuwa na vikundi vya vijana na ugonvi katika vinkundi vyenye asili tofauti. Katika maeneo mbalimbali, kumetokea matatizo ya wanafunzi wanaotumia madawa ya kulevya na kuleta silaha shuleni. Mtoto anayejisikia kusumbuliwa na mwengine lazima aepuke mtu yule na kuzungumza na mwalimu, au mshauri wa wanafunzi wa shule.

***Kama unafikiri kwamba watoto wanaweza hitaji msaada kwa tatizo shuleni, zungumza na mtu fulani shuleni kuhusu hayo!***




***Jadili kuhusu picha iliyo hapa juu kuhusu darasa la shule ya msingi ya kawaida nchini Marekani pamoja na mwengine.***

- ❒ Ufanano gani unaona kati ya darasa nchini Marekani na darasa nchini mwako au nchi yako ya ukimbizi?
- ❒ Unaona tofauti gani?
- ❒ Unafikiri ufanano na tofauti inamaanisha nini kuhusu jinsi watoto wako watazoea Marekani?

## USHIRIKI WA WAZAZI KATIKA ELIMU YA WATOTO



Walimu nchini Marekani wanaamini ya kwamba lazima wazazi washiriki katika elimu ya watoto wao kwa sababu hii inasaidia watoto kufanikiwa shuleni.Shule zinajaribu kusaidia wazazi kuelewa elimu ya watoto wao, na taarifa nyingi kwa wazazi wasiozungumza Kiingereza.

***Fikiri kuhusu jukumu la wazazi nchini mwako au nchi ya ukimbizi.***

- ❒ Katika njia gani wazazi waliusika?
- ❒ Wazazi walitembelea shuleni? Walisaidia kwa kazi ya nyumbani?
- ❒ Ilikuwa kawaida kuzungumza na walimu au viongozi? Kuhudhuria mikutano na mwalimu?

## MIKUTANO YA WAZAZI NA WALIMU

Shule zitapanga ili uweze kuzungumza kuhusu maendeleo ya watoto wako na walimu katika mikutano ya wazazi na walimu. Wewe pia unaweza kuomba ukutanane na walimu wa wototo wako wakati wowote unapokuwa na maswali au wasiwasi.




# 14 ELIMU

**Wamarekani wengi wanaiona elimu kama jambo linaloendelea maishani.**

***Chapa duara kwa picha iliyo hapa chini ambayo inaonesha njia unaweza kujihusisha na elimu ya watoto wako.***



Kupeleka na watoto kwa basi au shuleni



Tumika na watoto wako kazi za shule nyumbani



Kusindikiza watoto wako kwa matembezi



Kuhudhuria mikutano ya wazazi na walimu au magaribi ya wazazi shuleni



Kuwasikiliza watoto wakizungumza kuhusu shule na kuuliza maswali



Kujitolea katika madarasa ya watoto wako, au kwa chakula cha mchana au mapumziko



Kuzungumza na mwalimu ao kiogozi wa shule



Kusaidia kwa shuguli za nje ya masomo au timu ya michezo ya shule



Kutoa majadiliano juu ya nchi yako kwa wototo wa darasa la mtoto wako



Kujiunga na kundi la wazazi na walimu (PTA) au kuhudhuria mikutano ya bodi ya shule



Kushiriki katika matukio ya pekee kwa, shuguli au kuchangisha fedha

***Yote yalio hapa juu ni njia nzuri ya kushiriki katika elimu ya watoto wako.***

# SURA YA KUMI NA NNE 14

**_Zungumza na walimu wa watoto wako kuhusu jinsi unaweza kuwa sehemu ya elimu ya watoto wako!_**

**_Fikiri kuhusu yote uliyojifunza kuhusu shule nchini Marekani. Chapa au andika kuhusu tofauti kati ya shule nchini mwako au nchi yako ya ukimbizi na Marekani._**

## ELIMU KWA WATU WAZIMA

Wamarekani wengi wanaiona elimu kama kitu watu wanaweza kufurahia maisha yao yote, na watu wazima wengi wanajiandikisha kwenye masomo wakati fulani. Wanaendelea kufanya kazi zao muda ya kudumu na wanahudhuria madarasa jioni au siku za wikendi.

Wakimbizi, pia, wanaweza kuendelea na masomo yao huku wakifanya kazi. Shirika lako la makazi mapya linaweza kukusaidia kutafuta nafasi za kusoma katika jamii yako, kutoka madarasa ya kiingereza na masomo ya kupata diploma ya shule ya sekondari ya juu hadi madarasa ya mafunzo ya ufundi na utaalamu. Ni vizuri kuwa na baadhi ya mafunzo za juu ya shule ya sekondari, kama vile cheti au diploma.

---

Farah aliweka hakiba ili aweze kuchukua madarasa kwenye chuo kikuu. Lakini madarasa ambayo anataka kuchukua yanatolewa jioni, anapokuwa kazini. Lazima Farah afanye nini?

---

**Elimu ya juu inaweza kuwa bei sana.**

Zifuatazo ni moja za nafasi uwezo chache za kupata elimu kwa watu wazima ambao unaweza kupata katika jamii yako:



**KIINGEREZA NA MADARASA YA KUSOMA NA KUANDIKA.** Madarasa hizi zinakusaidia kujifunza Kiingereza. (Angalia Sura ya 13 kwa kujifunza zaidi kuhusu madarasa ya lugha ya Kiingereza.)

**OTHER ADULT EDUCATION CLASSES.** Mipango za elimu kwa watu wazima zinatoa madarasa mengi tofauti kwa watu wa jamii kwa ujumla. Kati ya hayo kuna masomo ya uwekaji hesabu na akaunti, ujuzi wa kuwa karani, ujuzi wa kompyuta, na lugha za kigeni.

**DIPLOMA YA KUJIENDELEZA KIELIMU (GED) MADARASA YA MATAYARISHO KWA DIPLOMA.** Madarasa hizi yanaruhusu watu wazima ambao hawakumaliza kamwe shule ya sekondari kupata diploma ya shule ya sekondari. Wakimbizi walio watu wazima ambao hawakupata elimu ya shule ya sekondari nchini mwao, au wasiokua na diploma ya shule ya sekondari, wanaweza kujifunza kwa kupata diploma ya GED.

**SHULE ZA UFUNDI NA USTADI.** Shule hizi zinafundisha watu kupata kazi zinazohitaji ujuzi wa pekee, kama fundi wa gari, kufanya mipango za kompyuta, na kuwa msaidizi wa daktari wa memo. Shule hizi zinapana vyeti kwa wanafunzi wao wanao hitimu.

---

Moe Win alikuwa fundi wa gari nchini mwake. Nchini Marekani, alichukua kazi ya kwanza aliyoipata, kupanga kabati katika duka. Moe alipata kujua kuhusu mafunzo kwa fundi wa gari, lakini angelipashwa kufanya kazi ya muda akisoma. Ungelikuwa Moe, vitu gani ndivyo ungelivifikiria kuhusu uamuzi?

---



**VYUO VYA JAMII NA VYUO VIKUU.** Kuna aina mbili kuu za elimu ya juu nchini Marekani: nyuo vya jamii au Community college (inayo tolea mpango ya miaka 2), na vyuo vya miaka nne na vyuo vikuu. Njia ya kuandikiwa inaweza kuwa ngumu, bei ghali, kuchukua muda. Vyuo vya jamii havina bei ghali, lakini vyuo vya miaka 4 vinaweza kuwa bei. Mengi ya vyuo vya jamii na vyuo vikuu vina ya pekee zinazo habari kuhusu msahada wa pesa kwa wanafunzi wanahitaji msaada zaidi. Wengi wa wanafunzi wa vyuo vikuu lazima walipe wenyewe kwa kuishi.


CAL Cultural Orientation Resource Center

***Chapa duara kwa njia za elimu ya watu wazima zinazo tolewa kwa ukarasa uliotangulia ambazo wewe au mtu mwengine katika jamaa yako anaweza kufurahiwa nazo.***

***Jinsi gani njia mbalimbali za elimu nchini Marekani zinaweza kuwa za mafaa kwako au kwa mtu mwengine katika jamaa yako?***

## KAMILISHA*

***Chagua majibu boza zaidi kwa maswali hapa chini ukifanya chaguo bora zaidi. Hii ni mfano:***

*Lugha gani ndio inazungumzwa na watu wengi zaidi Marekani?*

a. Kichina.

(b.) Kiingereza.

c. Kiujerumani.

***Watu wengi Marekani wanazungumza Kiingereza. Kwa hiyo, jibu ni b. Kiingereza.***

1. Elimu ya umma kwa watoto ni bure nchini Marekani?

   a. Ndiyo.

   b. Hapana.

2. Katika mitindo ya kufundisha kwa ujumla nchini Marekani kuna gani ya yafuatayo?

   a. Kuuliza maswali

   b. Majadiliano.

   c. Usomi mrefu.

   d. Chaguo a na b.

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 222.

3. Shule zote za umma nchini Marekani zinalazimisha wanafunzi kuvaa unifomu.

    a. Kweli.

    b. Uongo.

4. Rafiki yako anajisikia kuhusu kwenda kwenye shule ya watoto wake kwa mikutano ya wazazi na walimu kwa sababu hazungumzi Kiingereza. Lazima aende tu kwa mkutano?

    a. Hapana, lazima ajifunze kwanza Kiingereza kabla ya kukutana na walimu wa watoto wake.

    b. Ndiyo, silazima azungumze Kiingereza vizuri sana, kwa sababu mashule mengi yanatoa taarifa kwa wazazi wasiosema Kiingereza.

5. Wamarekani wanafikiri ya kuwa unaweza kujifunza tu ukiwa mtoto.

    a. Kweli.

    b. Uongo. Wamarekani wanaamini ya kwamba huwezi kamwe kuwa mzee kwa kujifunza mambo mapya.

15



# Sura Ya Kumi Na Tano

## SAFARI INAYOENDELEA

Kwa wakimbizi wengi, makazi mapya ni mara nyingi njia ndefu na yenyi changamoto, lakini kwa uvumilivu na tabiya nzuri, unaweza kuwa na maisha mazuri naya kustarehe katika jamii yako mpya. Kuna wakimbizi wengi ambao waliacha vitu vyote nyuma kwa kuanza maisha mapya nchini Marekani. Sasa wanasema Kiingereza, wana nyumba zao wenyewe, na wanafanya bishara. Kumbuka ya kwamba ingawa kutakuwa na changamoto nyingi mbele, vile vile kutakuwa pia na njia nyingi kwako.



# SURA YA KUMI NA TANO 15

***Katika sura ya 1, ulitambua mambo mbalimbali ambayo ulisikia kuhusu maisha nchini Marekani. Gani ni kweli? Na gani si kweli? Unaweza sema nini sasa kuhusu masiha nchini Marekani?***

***Rudi kwa ukarasa wa 8 na ujaze mazoezi.***

Kama unavyoona sasa, kuna vitu vingi vya kufikiria kuhusu na kuzingatia: kutumika na shirika lako la makazi mapya na kutumia huduma zingine za jamii, kujifunza Kiingereza, kutafuta kazi ambayo inaweza kuwasaidia wewe na jamaa yako, kukabiliana na utamaduni mpya, kuendelesha elimu, kuelewa na kutumia mfumo wa huduma za afya, kutembea peke yako mjini, kuishi salama na starehe katika nyumba yako na jamii, kujifunza kuhusu majimbo za Marekani na kutimiza haki na majukumu yako…..orodha inaendelea.

***Kutakuwa njia nyingi mpya na ya kusisimua kwa ajili yako !***

***Katika chati iliyo hapa chini, jaza katika kipande cha kati ukichapa au ukiandika mafikiri yako au majibu zako kwa maswali.***

| | **Leo ni tarehe gani?**<br>________________ | **Miezi 6–12 kisha kuandika katika chati hii mara ya kwaza, leo ni tarehe gani?**<br>________________ |
|---|---|---|
| 1. Malengo yako na vipaumbele vyako ni gani kwa mwezi yako ya kwanza nchini Marekani? | | |
| 2. Malengo na vipaumbele vyako ni gani kwa miezi yako 6 ya kwanza nchini Marekani? | | |
| 3. Malengo na vipaumbele vyako ni gani kwa mwaka yako ya kwanza nchini Marekani? | | |
| 4. Malengo na vipaumbele vyako ni gani kwa miaka miwili yako ya kwanza nchini Marekani? | | |
| 5. Malengo yako ya muda mrefu ni gani? | | |

# SURA YA KUMI NA TANO 15

***Katika kipindi cha miezi 6 au mwaka moja tangu sasa, tizama upya chati hii. Angalia wapi ulipo, na jaza katika mstari wa ngambo ya kuume. Kisha fikiri kuhusu yafuatayo:***

- ❒ Namna gani malengo yako yalibadilika?
- ❒ Ulijisikia namna gani kuhusu makazi yako mapya wakati ulijaza kwa mara ya kwanza chati hii?
- ❒ Unajisikia namna gani sasa?
- ❒ Jinsi gani ya kujisikia kuhusu makazi mapya ilibadilika?

Kuweka ujumbe zifwatazo katika akili yako itakusaidia kuwa na uzoefu bora wa makazi mapya:




- ❒ **UWE MWENYE KUJITEGEMEA.** Kuchukua nafasi kubwa katika makazi mapya yako itakusaidia kuzoea zaidi.
- ❒ **JIFUNZE KIINGEREZA.** Kusema Kiingereza itakusaidia kuzungumza mara moja na watu walio karibu nawe na itakuwezesha kuomba msaada unayohitaji.
- ❒ **ITIKA KAZI YA KWANZA INAYO TOLEWA KWAKO.** Kuwa na kazi, hata kama isiyo katika eneo ya ujuzi wako, itakusaidia kupata na kuweka hakiba ili uweze kujisaidia mwenyewe na jamaa yako haraka iwezekanavyo.
- ❒ **SHIRIKIANA NA SHIRIKA LAKO LA MAKAZI MAPYA.** Shirika lako la makazi mapya iliwasaidia wakimbizi wengi mbele yako kwa kufanyikiwa katika jamii yao mpya. Wana ujuzi na uzoefu wa kutumika na wakimbizi, kwa hiyo sikiliza vema wanayo kuambiya na shiriki nao matatizo yako na matumaini yako.



Kuna watu wengi pembeni nawe ambao wanataka kukuona onafanyikiwa. Kati ya watu hawa kuna jamaa yako, jamii yako, na shirika lako la makazi mapya.

***Una misaada mengi kutoka kwa watu wengi. Wanakutaka ufanyikiwe!***

*Chapa picha ya safari yako ya makazi mapya katika  kipande kilicho hapa chini.*

| | |
|---|---|
| **Kama mtoto nchini mwangu…** | **Kama mtu mzima nchini mwangu…** |
| **Katika nchi yangu ya ukimbizi…** | **Miezi wangu wa kwanza nchini Marekani…** |
| **Mwaka wangu wa kwanza nchini Marekani…** | **Miaka yangu tano ya kwanza nchini Marekani…** |

## KAMILISHA*

***Chagua majibu boza zaidi kwa maswali hapa chini ukifanya chaguo bora zaidi.***
***Hii ni mfano:***

*Lugha gani ndio inazungumzwa na watu wengi zaidi Marekani?*

a. Kichina.

(b.) Kiingereza.

c. Kiujerumani.

***Watu wengi Marekani wanazungumza Kiingereza. Kwa hiyo, jibu ni b. Kiingereza.***

1. Namna gani unaweza kuwa mwenyi kujitegemea?

   a. Kupata kazi

   b. Kuuliza maswali usipo elewa kitu fulani.

   c. Kuchunguza mazingira yako, kama vile maduka makubwa ya eneo au maktaba.

   d. Yoyote au yote yalio juu.

2. Hapa chini kuna baadhi ya njia unaweza kufanya mazoezi yako ya Kiingereza. Gani unafikiri inaweza kuwa rahisi kwa kuifanya?

   a. Kuhudhuria madarasa ya Kiingereza.

   b. Kujifunza na mtu anayejitolea.

   c. Kutizama maonyesho au filamu ya Kiingereza kwenye televisheni.

   d. Kufanya mazoezi ya kusema, kusoma, au kusikiliza katika Kiingereza kwa dakika 10 kila siku.

---

* Majibu sahihi zinatolewa katika kiambatisho A kwenyi ukarasa 222.

3. Kwa nini ni muhimu kukubali kazi ya kwanza inayotolewa kwako?

    a. Toleo nyingine ya kazi inaweza kutotolewa kwako kwa muda fulani.

    b. Ili kusaidia jamaa lako.

    c. Kusaidia kulipa deni zako.

    d. Yoyote au yote yalio juu.

4. Hapa chini kuna njia ambazo unaweza kutumia vizuri na shirika lako la makazi mapya. Gani ndiyo ya muhimu zaidi?

    a. Kufika kwa wakati kwa miadi.

    b. Kuuliza maswali.

    c. Kusikiliza vizuri yale wafanyakazi wa shirika lako la makazi mapya wanakueleza.

    d. Shiriki wasiwasi yako, hofu, na matumaini yako na wafanya kazi wa shirika lako la makazi mapya.

# KIAMBATISHO A

## MAJIBU

### SURA YA 1

» **KAMILISHA kwenye ukarasa wa 12: 1.** Kweli **2.** Kweli **3.** Uongo **4.** Kweli **5.** Kweli **6.** Uongo **7.** Kweli **8.** Uongo **9.** Kweli **10.** Kweli **11.** Kweli **12.** Kweli

### SURA YA 2

» **KAMILISHA kwenye ukarasa wa 23: 1.** b **2.** e **3.** e **4.** c **5.** b

### SURA YA 3

» **MAZOEZI YA KUPATANISHA kwenye ukarasa wa 34: 1.** c **2.** a **3.** b
» **KAMILISHA kwenye ukarasa wa 41: 1.** a **2.** b **3.** e **4.** b **5.** d **6.** b

### SURA YA 4

» **KAMILISHA kwenye ukarasa wa 55: 1.** Kweli **2.** Uongo **3.** Uongo **4.** Kweli **5.** Kweli **6.** Uongo

### SURA YA 5

» **MAZOEZI YA AINA YA MAKAZI kwenye ukarasa wa 59: 1.** b **2.** d **3.** a **4.** c
» **MAZOEZI YA USALAMA NYUMBANI kwenye ukarasa wa 63: 1.** d **2.** c **3.** a **4.** e **5.** b
» **KAMILISHA kwenye ukarasa wa 66: 1.** d **2.** a **3.** d **4.** d **5.** b

### SURA YA 6

» **MAZOEZI YA HUDUMA ZA DHARURA kwenye ukarasa wa 73: 1.** c **2.** a **3.** b
» **MAZOEZI YA HALI ZA DHARURA kwenye ukarasa wa 74: 1.** Ndiyo, ita idara ya kuzima moto. **2.** Hapana. Itakuwa sahihi zaidi kuita wazazi wa msichana au kwenda nyumbani kwao kwa kujadiliana kuhusu jambo hii nao. **3.** Ndiyo, omba ambulansi. **4.** Hapana. Kama huone moto kisha kuangalia vizuri, unaweza kuhitaji betri mpya kwa ajili ya king'ora chako cha moto. **5.** Ndiyo, umba polisi. **6.** Hapana. Kama unaweza kujijali mwenyewe kuhusu usalama wako nyumbani, kama kwa mfano huu, hakuna haja ya kuita 911.
» **KAMILISHA kwenye ukarasa wa 77: 1.** d **2.** b **3.** b **4.** a **5.** a

# KIAMBATISHO A

## SURA YA 7

» MAZOEZI YA KUPATANISHA KUHUSU ALAMA ZA BARABARANI kwenye ukarasa wa 85: **1.** c **2.** e **3.** b **4.** a **5.** d

» KAMILISHA kwenye ukarasa wa 88: **1.** e **2.** a **3.** d **4.** a **5.** e

## SURA YA 8

» MAZOEZI YA 1 YA KUPATANISHA KUHUSU WASIWASI YA AFYA kwenye ukarasa wa 95: **1.** b **2.** a **3.** b **4.** a **5.** c **6.** c

» MAZOEZI YA 2 YA KUPATANISHA KUHUSU WASIWASI YA AFYA kwenye ukarasa wa 96: **1.** b **2.** c **3.** a

» MAZOEZI YA KUPATANISHA KUHUSU WASIWASI YA AFYA kwenye ukarasa wa 97: **1.** f **2.** a **3.** d **4.** b **5.** c **6.** e

» MAZOEZI YA KUPATANISHA KUHUSU BIMA YA AFYA kwenye ukarasa wa 98: **1.** b **2.** a **3.** a

» MAZOEZI YA KUPATANISHA KUHUSU VYAKULA VYA AFYA kwenye ukarasa wa102:
**Vyakula vya afya: (chapa duara):** b c e g j k
**Vyakula visivyo vya afya (vuta):** a d f h i

» KAMILISHA kwenye ukarasa wa 106: **1.** a **2.** e **3.** a **4.** e **5.** b

## SURA YA 9

» MAZOEZI KUHUSU MAHITAJI NA MATAKWA kenye ukarasa wa 114:
**Vitu ambavyo jamaa yako inaweza hitaji (chapa duara):** a b d e g h k l
**Vitu ambavyo jamaa yako haihitaji, lakini inaweza kuvihitaji (vuta ):** c f i j

» MAZOEZI KUHUSU KODI kwenye ukarasa wa118:
**Kodi inaweza kulipwa kwa ajili ya (chapa duara):** a b e h
**Kodi hailipwi kwa ajili ya:** c d f g

» KAMILISHA kwenye ukarasa wa 124: **1.** d **2.** b **3.** e **4.** b **5.** a

## SURA YA 10

» KAMILISHA kwenye ukarasa wa 141: **1.** a **2.** e **3.** a **4.** e **5.** d

# KIAMBATISHO A

## SURA YA 11

- **MAZOEZI KUHUSU HAKI NA MAJUKUMU KULINGANA NA HALI YA UHAMIAJI kwenye ukarasa wa 156**:
  - **HAKI:**

    **Kuomba muungano wa jamaa:** Yote (mkimbizi, mkaji wa kudumu [LPR], raia)

    **Kuomba msaada wa umma:** Yote

    **Kwenda shuleni na kufanya kazi:** Yote

    **Kusfiri kwa uhuru ndani ya Marekani:** Yote

    **Kusafiri nje ya Marekani bila ruhusa:** Mkaji wa kudumu [LPR] & raia

    **Kupiga kura:** Raia
  - **MAJUKUMU:**

    **Kujua na kutii sheria: Yote**

    **Kulipa kodi:** Yote

    **Kujiandikisha kwa ajili ya uchaguzi kama raia mwanaume kati ya umri wa miaka 18 na 25:** Yote

    **Kuheshimu kahi za wengine:** Yote

    **Kuwa muamuzi katika mahakama:** Raia

    **Kushugulikia na kulinda watoto wako:** Yote
- **KAMILISHA kwenye ukarasa wa 158**:

  **1.** Kweli **2.** Kweli **3.** Uongo **4.** Kweli **5.** Uongo **6.** Kweli **7.** Kweli **8.** Uongo

## SURA YA 12

- **MAZOEZI YA KUPATANISHA KUHUSU AINA ZA KAZI kwenye ukarasa wa 163**: **1.** b **2.** c **3.** a
- **KAMILISHA kwenye ukarasa wa 181**:

  **1.** Kweli **2.** Uongo **3.** Kweli **4.** Kweli **5.** Kweli **6.** Kweli **7.** Kweli **8.** Uongo

## SURA YA 13

- **KAMILISHA kwenye ukarasa wa 194**: **1.** b **2.** e **3.** a **4.** d **5.** a

## SURA YA 14

- **KAMILISHA kwenye ukarasa wa 210**: **1.** a **2.** d **3.** b **4.** b **5.** b

## SURA YA 15

- **KAMILISHA kwenye ukarasa wa 217**: **1.** d **2.** Yoyote au yote yalio juu **3.** d **4.** Yoyote au yote yalio juu

# KIAMBATISHO B

## KAMUSI YA MANENO YA KAWAIDA YA MAKAZI MAPYA

Maneno yafuatayo yanusiana na wakimbizi wanaopata makazi mapya nchini Marekani:

**BIMA YA GARI** (CAR INSURANCE): Ni mkataba wa fedha kati ya dereva na kampuni ya bima. Katika mkataba, dereva anakubali kulipa kampuni ya bima kiasi fulani cha pesa kila mwezi, na kampuni ya bima inakubali kulipa bei yoyote ambayo inatokana na ajali ambamo dereva anashiriki amo. Katika miji nyingi ya Marekani madereva wanalazimishwa kununua bima ya gari.

**MENEJA WA KESI AU MFANYAKAZI** (CASE MANAGER OR CASE WORKER): Ni mtu katika shirika la huduma za kijamii ambaye anasaidia wakimbizi kupata huduma wanazohitaji

**MAELEZO YA UTAMADUNI** (CULTURAL ORIENTATION [CO]): Ni mchakato wa kujifunza kuhusu maisha nchini Marekani. Mchakato unaanzia nje na unaendelea nchini Marekani.

**IDARA YA AFYA NA HUDUMA ZA BINADAMU** (DEPARTMENT OF HEALTH AND HUMAN SERVICES [HHS]): Ni shirika la serikali inayotoa fedha kwa afya na huduma za binadamu, hasa kwa wale ambao hawawezi kujisaidia.

**IDARA YAMAMBO YA NJE** (DEPARTMENT OF STATE): Ni shirika la serikali inayo ongoza mipango ya kuitikiwa kama wakimbizi nchini Marekani, ikiwa pamoja na mipango ya kuwapokea na kuwakaribisha vizuri (R&P program).

**KUENDESHA GARI UKIWA KATIKA HALI YA ULEVI** (DRIVING UNDER THE INFLUENCE [DUI])/**KUENDESHA GARI WAKATI** (DRIVING WHILE INTOXICATED [DWI]): Ni tendo la kuendesha gari, au chombo kingine, wakati katika hali ya ulevi wa pombe na/au dawa za kulevya.

**HUDUMA ZA HALI YA DHARURA** (EMERGENCY SERVICES): Huduma ambazo zinawasaidia watu wakati wa dharura, kama vile moto, uhalifu, na matatizo makubwa na ghafla za afya. Aina tatu za kawaida za huduma za dharura ni polisi, idara ya moto, na huduma za ambulansi.

**KADI YA KUKURUHUSU KUFANYA KAZI** (EAD [EMPLOYMENT AUTHORIZATION DOCUMENT] CARD): Ni kadi inayotolewa na serikali amabyo inaruhusu mmiliki kufanya kazi nchini Marekani kwa muda fulani wakati mtu ana hali ya pekee ya uhamiaji. Kadi EAD inaitwa pia kibali cha kufanya kazi.

**KIINGEREZA KAMA LUGHA YA PILI** (ENGLISH AS A SECOND LANGUAGE [ESL] CLASSES): Madarasa ya Kiingereza kwa watu wazima na watoto ambao Kiingireza siyo lugha yao ya kwanza.

**MASHIRIKA ZA KIJAMII ZA KIKABILA** (ETHNIC COMMUNITY-BASED ORGANIZATIONS [ECBOs]): Mashirika ya kikabila yaliundwa na wakimbizi wa zamani na wahamiaji, kwa kutoa huduma ambazo zinawasaidia wageni katika jamii zao.

**STEMPU ZA CHAKULA** (FOOD STAMP PROGRAM): Ni mipango ya serikali ambayo inawasaidia jamaa zenye pato la chini kulipa kwa kununua chakula. Jina layo rasmi ni mipango za msaada ya zaidi kwa chakula (Supplemental Nutrition Assistance Program [SNAP]).

# KIAMBATISHO B

**DIPLOMA YA KUJIELELEZA ELIMU** (GENERAL EDUCATIONAL DEVELOPMENT [GED] DIPLOMA): Ni diploma kwa watu wazima ambayo inakubaliwa kuwa sawa na diploma ya shule ya sekondari ya juu.

**KADI YA KIJANI** (GREEN CARD): Inajulikana pia kama kadi ya makazi ya kudumu, kadi hii inatolewa na USCIS (wende kwa mafasiriyo ya neno USCIS kwenye ukarasa wa 225) kwa wasio waraia kama ushahidi ya kwamba mtu ana hali ya mkazi wakudumu nchini Marekani. Anayekuwa na kadi hii anajulikana kama mkaazi wa kudumu (LPR).

**BIMA YA AFYA** (HEALTH INSURANCE): Ni mkataba ambayo inalipa deni za huduma za afya kutokana na magonjwa au kuumia. Malipo kwa ajili ya bei ya bima ya afya yanalipwa na mkuu wa kazi, mtu binafsi, au wote wawili.

**MHAMIAJI** (IMMIGRANT): Ni mtu ambaye anahamia katika nchi nyingine kwa kuisha huko kwa lote.

**SHIRIKA LA KIMATAIFA LA UHAMIAJI** (INTERNATIONAL ORGANIZATION FOR MIGRATION [IOM]): Ni shirika la kimataifa ambalo linadumuisha harakati za kibinadamu na utaratibu wa watu kuvuka mipaka.

**MSAADA WA AFYA KWA WATU WENYI KIPATO CHA CHINI** (MEDICAID): Ni mpango wa serikali ambayo inatoa bima ya afya kwa watu wenyi pato la chini.

**MSAADA WA AFYA KWA WAZEEE** (MEDICARE): Ni mpango ya serikali ambayo inatoa bima ya afya kwa watu wenyi zaidi ya umri wa miaka 65, na watu chini ya miaka 65 ambao wana ulema mbalimbali.

**OFISI YA KUWAPA WAKIMBIZI MAKAZI MAPYA** (OFFICE OF REFUGEE RESETTLEMENT [ORR]): Ni ofisi ya serikali, chini ya idara ya afya na huduma za binadamu, ambayo ina tolewa kwa wakimbizi na makundi mengine na msaada ya pekee kupitia mipango zake na ruzuku.

**KUWA NA WABIBI WENGI** (POLYGAMY): Kuwa na zaidi ya mwanamke mmoja mara moja. Hairuhusiwi nchini Marekani.

**BANDARI YA KUINGIA** (PORT OF ENTRY): Mahali ambapo mtu anaingilia nchini kwa kisheria.

**WARAKA WA KUAHIDI** (PROMISSORY NOTE): Hati ambayo mtu moja anaahidi kulipa kiasi cha seti ya fedha kwa mwengine. Kwa kawaida waraka wa kuahidi ni kwa malipo ya mkopo.

**MIPANGO YA MAPOKEZI NA KUWAWEKA** (RECEPTION AND PLACEMENT PROGRAM): Ni mipango ya idara ya mambo ya nje ambayo inawatolea wakimbizi wapya wanaoasili na huduma muhimu na msaada wanayohitaji kwa kuanza makazi mapya katika jamii mpya.

**MKIMBIZI** (REFUGEE): Ni mtu ambaye amelazimishwa kuondoka nchini mwake kwa kuhepuka mateso. Ufafanuzi kamili ya mkimbizi na shirika la Umoja wa mataifa (UN) la kuhudumia wakimbizi ni mtu ambaye " kutokana na hofu ya kuteswa kwa sababu ya rangi, dini, utaifa, uwana chama wa kikundu fulani cha kijamii au maoni ya kisiasa, iko nje ya nchi ya utaifa wake, na hana uwezo wa, au kutokana na hofu hiyo, hana nia ya kujitegemea mwenyewe kwa ulinzi kutokana na nchi hiyo.

# KIAMBATISHO B

**MSAADA WA PESA KWA WAKIMBIZI** (REFUGEE CASH ASSISTANCE [RCA]): Ni mpango wa serikali ambayo inatoa msaada wa kifedha kwa muda kwa wakimbizi wasio owa au kuolewa na wakimbizi waliyo owa na hawana watoto wanao wategemea.

**MAKAZI MAPYA** (RESETTLEMENT): Mchakato wa kuhamia kwa lote nchini.

**SHIRIKA LA MAKAZI MAPYA** (RESETTLEMENT AGENCY): Shirika ambalo linatoa mapokezi na makao ya mwanzo ambazo wakimbizi wanapata. Shirika linaweza toa misaada zaidi.

**KITUO CHA MSAADA CHA MAKAZI MAPYA** (RESETTLEMENT SUPPORT CENTER [RSC]): Kituo ambacho kinawasaidia wakimbizi kuomba makazi mapya nchini Marekani. RSCs inasimamia pia shuguli za kabla ya kuondoka, kama vile maelezo ya utamaduni.

**HUDUMA LA CHAGUZI** (SELECTIVE SERVICE): Shirika la serikali ambalo linaweza kuwachagua watu kwa huduma za kiaskari, kwa kawaida wakati wa vita. Wanaume wote wenye umri kati ya 18 na 25 lazima wajiandikishe kwa huduma la chaguzi.

**MTOA HUDUMA** (SERVICE PROVIDER): Wakala au shirika ambayo inatoa huduma, au huduma nyingi, kwa watu.

**UNYANYASAJI WA KIJINSIA** (SEXUAL HARASSMENT): Tabia yoyote isiyotakiwa ya hali ya kijinsia ambayo inafanya mtu ajisikiye mwenyi kutishiwa au mwenyi wasiwasi.

**KADI YA RUZUKU YA SERIKALI** (SOCIAL SECURITY CARD): Kadi inayotolewa na serikali na namba ya mtu ya social security zilizo chapishwa juu yayo. Namba ya ruzuku ya serikali ni muhimu kwa sababu inahitajika kwa kupata kazi, na kupokea misaada mingine na huduma za serikali.


**MSAADA WA MUDA KWA JAMAA ZENYE MAHITAJI** (TEMPORARY ASSISTANCE TO NEEDY FAMILIES [TANF]): Mpango wa serikali ambayo inatoa msaada wa muda kwa wazazi wenye watoto wanao wategemea.


**SHIRIKA LA WAKIMBIZI LA UMOJA WA MATAIFA** (THE UN REFUGEE AGENCY [UNHCR]): Shirika la kimataifa ambalo inasimamia ulinzi wa wakimbizi na inafanya kazi ya kutafuta ufumbuzi wa matatizo yanayo athiri wakimbizi duniani kote.


**OFISI YA HUDUMA ZA URAIA NA UHAMIAJI MAREKANI** (U.S. CITIZENSHIP AND IMMIGRATION SERVICES [USCIS]): Shirika la serikali ambayo inasimamia uhamiaji halali nchini Marekani. USCIS inawatolea pia wakimbizi taarifa na zana wanayohitaji kwa kuwa mkaji wa kudumu (LPRs) na raia.


## NYUSO ZA HISIA


Unaweza kuwa na shida ya kujiteteya wakati mwingine. Nyuso zilizo hapa chini zinaweza kukusaidia. Tambua baadhi ya jinsi hizi za kujisikia unazozitarajia katika njia yako ya makazi mapya.



Mwenye asira



Asikuwa na cha kufanya



Mwenye kufadhaika



Mwenye udadisi



Mwenye  kusisimka



Mzuri



Mwenye furaha



Mwenye bilasubira



Mwenye kutukaniwa



Mwenye wasiwasi



Mwenye kujivuna


Mwenye huzuni


Mwenye uoga


Mwenye kushangazwa


Mwenye shukrani


Mwenye wasiwasi


CAL COR Cultural Orientation Resource Center

# Karibu
# MAREKANI

***Karibu Marekani: Kitabu cha Mwongozo kwa Wakimbizi*** kina taarifa muhimu kwa kusaidia wakimbizi kujitayarisha kwa miezi michache za kwanza nchini Marekani. Kinakueleza kuhusu mambo ya kuyataraji kama wakimbizi walio patanishwa mahali mapya pa kuishi, kutafuta kazi, kukutana na watu Merikani, na kujirekebisha kwa utamaduni na jamii Marekani. Katika mada zinazohutubiwa kuna:

Safari ya Makazi Mapya

Marekani na Utamaduni wa Marekani

Kusafiri Marekani

Shirika la Makazi Mapya

Nyumba

Huduma za Jamii

Usafiri

Huduma za Afya

Matumizi ya Fedha

Kujirekebisha Utamaduni na Kubadilisha Wajibu

Haki na Majukumu chini ya Sheria nchini Marekani

Kazi

Kujifunza Kiingreza

Elimu

Safari Inayoendelea

Kitabu cha mwongozo hiki kina mazoezi mbalimbali, tathmini ya kipekee, na maneno na misemo za kiingereza zinazo tumiwa kwa kawaida.

CAL **Cultural Orientation Resource Center** | Funded by the U.S. Department of State, Bureau of Population, Refugess, and Migration ©2014 | **www.culturalorientation.net**
ISBN: 978-0-87281-096-9